# Nipashe

Alhamisi Julai 4, 2019 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

ISSN 0856 • Na. 0579961

www.ippmedia.com

MWANGA WA JAMII

www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US




## Shahidi kesi ya Mbowe adai kutishwa mihemko Chadema

UKURASA 3




UKURASA 13

# CAG ataja dawa kumaliza rushwa

• **Afichua** mikataba, sheria ya ununuzi, asema bila hivyo... *Endelea ukurasa 2*



Mtuhumiwa Godfrey Nkwambi, anayekabiliwa na kesi ya mauaji ya mkewe, akiwa chini ya ulinzi wa askari magereza katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, jijini Dar es Salaam jana, baada ya kumaliza kusikiliza ushahidi wake. Habari uk. 3. **PICHA: HELLEN MWANGO**

## YALIYOMO


UKURASA WA 2

**WAGONJWA HOMA DENGUE WAPUNGUA**

WAZIRI wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, jana aliwaongoza wakazi Manispaa ya Ilala jijini...

UKURASA WA 4

**MAJALIWA AIPIGIA CHAPUO VIETNAM KUNUNUA KOROSHO**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewakaribisha wafanyabiashara kutoka nchini humo kununua korosho nchini ambazo amesema...


## Ajali Hiace yaua wanne

UKURASA 3

## Ukaguzi mikataba ajira za madereva Julai 15

UKURASA 2


**MICHEZO** AZAM WAAHIDI KURUDI NA KAGAME LAO UK.31

**MAONI, KATUNI** UK.6

# CAG Assad ataja dawa kumaliza rushwa

**Na Elizabeth Zaya**

MDHIBITI na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), Prof. Mussa Assad, amesema mwarobaini wa rushwa nchini ni kuweka wazi na hadharani mifumo yote ya ununuzi na mikataba yote ambayo serikali inaiingia kila sekta.

Prof. Assad alitoa kauli hiyo jana jijini Dar es Salaam katika kongamano la kujadili namna ya kupambana na rushwa lililoandaliwa na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) kwa kushirikiana na Mamlaka ya Maendeleo ya Biashara Tanzania (Tantrade).

Alisema sababu zinazochangia rushwa ni mambo nyingi, hususan mikataba kufanyika katika hali ya usiri kuanzia hatua ya mwanzo kuingia katika mikataba au ununuzi hadi mwisho, hivyo njia ya kudhibiti ni kuweka utaratibu ambao kila mwananchi atakuwa na uwezo wa kupata taarifa zote wakati wowote.

"Mimi nafikiri ili kupambana vizuri na suala la rushwa, tunatakiwa kuhakikisha kwamba tunaweka utaratibu wa kuwapo na uwazi hasa katika upande wa ununuzi, mikataba yote na mambo yote yanayofanyika ndani ya nchi, na taarifa zote ziwekwe kwenye website ili

INAENDELEA UK. 8

## Wagonjwa wa dengue wapungua

**Na Romana Mallya**

WAZIRI wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, Ummy Mwalimu, jana aliwaongoza wakazi wa Manispaa ya Ilala jijini Dar es Salaam kupulizia dawa ya kuua mazalia ya mbu waenezao ugonjwa wa dengue na kueleza kuwa idadi ya waliougua imepungua kutoka watu 2,759 mwezi Mei hadi wagonjwa 790 mwezi uliopita.

Waziri Ummy alimpongeza Mkuu wa Wilaya ya Ilala, Sophia Mjema, Mkurugenzi na Mbunge wa jimbo hilo, kwa hatua walizochukua za kukabiliana na ugonjwa huo.

"Nimeridhishwa na hatua mlizochukua za kununua mashine mpya 14 za kupulizia dawa, wamenunua viuadudu kutoka kiwandani Kibaha lita 3,980 kwa Sh. milioni 53, wamenunua lita 210 za kuua mbu wapevu na upuliziaji unaendelea katika Kata 25," alisema.

Waziri Ummy alisema matokeo ya jitihada walizofanya zimeanza kuonekana kwa sababu idadi ya wagonjwa wilayani humo imepungua kutoka 527 mwezi Mei hadi 207 mwezi uliopita.

"Ninawataka na kuwahimiza wananchi kushiriki kikamilifu katika kutokomeza mbu," alisema.



Rais mstaafu wa awamu ya tatu, Benjamin William Mkapa, akikata utepe kuzindua safari ya miaka mitano ya Chuo Kikuu cha Mt. Augustino cha Tanzania (SAUT), kuelekea Jubilei ya miaka 25 tangu kuanzishwa chuo hicho, mwaka 1998, katika hafla iliyofanyika jijini Mwanza juzi. Kulia kwake ni Rais wa Baraza la Maaskofu Tanzania (TEC) ambaye pia ni Mwenyekiti wa Baraza la Chuo hicho, Askofu wa Jimbo Katoliki la Geita, Flavian Kassala na (kushoto kwake) ni Makamu wa Mkuu wa Chuo, Balozi Prof. Costa Ricky Mahalu na (kulia), ni mkuu wa mkoa huo, John Mongella. **PICHA: ELEUTERI MANGI-SAUT**

# Ukaguzi mikataba ajira za madereva Julai 15

**Romana Mallya**

SERIKALI imetangaza kuwa itafanya ukaguzi wa mikataba ya ajira za madereva ili kuangalia utekelezaji wa Sheria ya Kazi baada ya kubainika baadhi ya kampuni za usafirishaji kufanya udanganyifu.

Kwa mujibu wa taarifa ya Katibu Mkuu wa Ofisi ya Waziri Mkuu, Kazi, Vijana, Ajira na Wenye Ulemavu, ukaguzi huo utafanyika Julai 15, mwaka huu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi Kitengo cha Usalama Barabarani na Mamlaka ya Usafiri wa Ardhi (LATRA).

Taarifa hiyo ilisema kuwa baadhi ya kampuni zinazomiliki vyombo vya usafirishaji zimekuwa zikifanya udanganyifu kwenye mikataba ya ajira, malipo ya mishahara na posho mbalimbali.

"Kwa upande wa utekelezaji wa Sheria za Kazi, changamoto zimeendelea kujitokeza katika masuala ya mikataba ya ajira, malipo ya mishahara na posho mbalimbali ambapo imebainika zipo kampuni chache zinazolenga kuchafua kazi nzuri inayofanywa na sekta hii," ilisema.

Taarifa hiyo ilisema kampuni hizo chache zimekuwa zikifanya udanganyifu kwenye mikataba ya ajira za madereva wao yanapofanya maombi ya leseni za usafirishaji.

"Katika jitihada za kuzipatia ufumbuzi changamoto hizo, ofisi yangu kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi na LATRA tutafanya ukaguzi kwa lengo la kukagua mikataba hiyo na kuangalia utekelezaji wa sheria kwa ujumla," ilisema.

Aidha, taarifa hiyo iliwataka wamiliki wa vyombo vya usafirishaji, wafanyakazi, madereva na umma kuhakikisha mikataba ya madereva inakuwapo katika maeneo yao ya kazi.

"Madereva mhakikishe mnakuwa na nakala za mikataba yenu mnapokuwa katika kazi zenu ili iwe rahisi kwa wakaguzi kuiona. Ukaguzi huu ni endelevu na utahusisha pia sekta nyingine nchini," alisema.

Pia ilisema kuwa katika kutimiza azma ya kufikia uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025, serikali inaendelea pamoja na mambo mengine, kuimarisha mazingira ya uwekezaji na ufanyaji biashara katika sekta mbalimbali ikiwamo ya usafirishaji.

"Sekta hii ni miongoni mwa sekta zenye mchango mkubwa katika kukuza uchumi na kuongeza mapato ya serikali. Imekuwa ikichangia pia kuzalisha ajira kwa vijana wetu katika nafasi mbalimbali kama vile madereva, mafundi na kada nyingine," ilieleza.

Taarifa hiyo ilisema kuwa pamoja na mchango mkubwa unaotolewa na sekta hiyo, zipo changamoto kadhaa ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi na serikali kwa kushirikiana na wadau.

Taarifa hiyo ilifafanua zaidi kuwa, ukaguzi huo utafanyika kwa namna mbili, maofisa kazi waliopo katika ofisi za kazi kupita katika kampuni zote za usafirishaji na nyingine ni timu maalum ya maofisa kazi wa kushirikiana na viongozi wa vyama vya wafanyakazi madereva, LATRA na Jeshi la Polisi kukagua mikataba kwenye vituo vikuu vya ukaguzi.

"Vituo hivi ni kama vile kituo cha mabasi Ubungo, kituo cha kuegesha malori cha Misugusugu na vituo vingine vinavyofanana na hivyo hapa nchini," alisema.

Pia, taarifa hiyo ilieleza kuwa ukaguzi huo utakwenda sambamba na viongozi wa vyama vya wafanyakazi, madereva na vyama vya waajiri kupatiwa elimu kuhusu haki na wajibu wao katika kutekeleza sheria hiyo.

"Napenda kutoa wito kwa wamiliki vyombo vya usafirishaji, viongozi wa vyama vya wafanyakazi, madereva pamoja na madereva wote kutoa ushirikiano wa kutosha kwa wakaguzi wakati wote wa ukaguzi, ili kutoathiri utoaji wa huduma kwa wananchi kwa namna yoyote ile," ilisema.


JAMHURI YA MUUNGANGO WA TANZANIA
WIZARA YA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO

Simu: +255 26 2324455.
Fax: +255 26 2323233.
Barua Pepe: ps@mow.go.TZ.
Tovuti: www.mwtc.go.TZ.

Mtaa wa Moshi
S.L.P 2888,
40470DODOMA

**TANGAZO**

1. Ndugu wananchi mnatangaziwa kuwa siku ya Alhamisi tarehe 4/7/2019 kampuni ya **SUMMER COMMUNICATION LTD YA NJOMBE** itasafirisha Mzigo wake wenye vipimo vikubwa kutoka **LUJEWA kuelekea KYELA,** gari hilo lenye namba za usajili:

**T 552 DKN/ T 960 CMQ**

2. Gari hilo lina vipimo vifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| **Urefu** | - | mita | 17 |
| **Upana** | - | mita | 3.5 |
| **Kimo** | - | mita | 5.2 |

3. Njia itakayotumika: UBALUKU hadi UYOLE KYELA, Gari zitasafiri muda wa mchana tu (kuanzia saa 12:30 Asubuhi mpaka saa 12.00 jioni)

*Tunaomba radhi kwa usumbufu utakaojitokeza.*

115308702



**KADI YA GARI IMEPOTEA**

**CAROLINE GABRIEL LOIBANGUTI** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 779 AZK** Aina yake **TOYOTA SPRINTER,** Yenye chasis namba AE1100109986 na Engine namba **5AG871689.** Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **MOR/MOR/RB/84986/2019.**

115308302



**KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI.**

**HAMISI SAIDI HAMISI** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **TVS** yenye namba za usajili **MC415BGB** Chassis namba **MD6M14PK8G4A35932** Engine namba **DK4AG4314032.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi **RB/DOM/TR/2348/2019.**

115308202



**KUPOTEA KWA KADI YA GARI**

**SHUKURU OSWARD MAHENGE** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI YENYE NAMBA ZA USAJILI MC 441 AYH AINA YA KINGLION RANGI NYEKUNDU.CHASSIS NAMBA **LTBPK8BG9F214951** ENGINE NAMBA **KL157FMI15J14618.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MKT/RB/436/2019.**

115307702

HABARI KITAIFA



Waziri Mkuu, Kassim Majaliwa, akizungumza na Balozi wa Vietnam hapa nchini, Nguyen Doanh, ofisini kwa Waziri Mkuu, Magogoni, jijini Dar es Salaam, jana. **PICHA: OWM**

# Shahidi adai alikimbia mihemko ya Chadema

**Na Hellen Mwango**

KOPLO Charles wa Ofisi ya Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai Mkoa wa Kipolisi Kinondoni, amedai mahakamani katika kesi ya uchochezi inayowakabili viongozi na wafuasi wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema) kwamba mihemko ya wafuasi wa chama hicho, ilisababisha akimbilie kwenye gari la jeshi hilo kunusuru kamera yake ya video.

Aidha, alidai kuwa mihemko hiyo ilisababishwa na hamasa aliyoitoa Mwenyekiti wa Chadema, Freeman Mbowe, kutoa kauli ya kuwapandikiza chuki wafuasi hao dhidi ya serikali.

Ushahidi huo aliutoa jana katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, iliyoketi chini ya Hakimu Mkazi Mkuu Thomas Simba, wakati akisikiliza ushahidi wa Jamhuri dhidi ya vigogo tisa wa Chadema akiwamo Mbowe.

Katika ushahidi huo, jopo la Jamhuri liliongozwa na Mawakili wa Serikali Wakuu, Faraja Nchimbi, Paul Kadushi, Dk. Zainabu Mango, Mawakili wa Serikali Jacqueline Nyantori, Wankyo Simon na Salim Msemo.

Akiongozwa na Wakili Kadushi, shahidi alidai kuwa Februari 16, 2018 alipangiwa kazi kama mwandishi wa habari kuripoti habari za mkutano wa kufunga kampeni wa Chadema katika viwanja vya Buibui vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam.

Alidai kuwa alijiandaa na vitendea kazi vyake ikiwamo kamera ya kupiga picha za video na ilipofika saa 10 jioni, alifika katika viwanja hivyo kwa ajili ya kuanza kazi.

"Nilipofika watu walianza kukusanyika na mshereheshaji alitangaza kwamba viongozi wakuu wa chama wameshafika. Baada ya muda wabunge na viongozi wakuu walipanda jukwaani nilimsikia Mbowe akitoa kauli za kufanya hamasa ya kuichukia serikali,"

INAENDELEA UK. 8

# Wanne wafariki ajali ya Hiace

**Na Said Hamdani,** LINDI

WATU wanne wamefariki dunia papo hapo na wengine sita kujeruhiwa baada ya gari walilokuwa wakisafiria aina ya Toyota Hiace kuligonga lori la Kampuni ya Saruji ya Dangote.

Ajali hiyo ilitokea juzi katika kijiji cha Mto Mkavu, Tarafa ya Mchinga wilayani Lindi, barabara kuu ya Kibiti-Lindi, majira ya saa 2:00 usiku.

Wakizungumza na waandishi wa habari katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa ya Sokoine mkoani hapa, baadhi ya majeruhi, Yusufu Chapuchapu, Selemani Sabiini na Shufaa Matola, walisema wakiwa wanatoka Kilanjelanje, Wilaya ya Kilwa kwenda mjini Lindi, gari lao Toyota Hiace liliigonga lori la Dangote.

Hiace hiyo yenye namba za usajili T239 DMA iliyokuwa ikiendeshwa na Mohamed Makame, iliigonga lori hilo lenye namba T 747 DKA, lililokuwa limeegeshwa pembeni mwa barabara na dereva wake akiwa anaangalia hitilafu iliyokuwa imejitokeza.

Aidha, dereva Makame anadaiwa kukimbia muda mfupi baada ya kutokea ajali hiyo.

Abiria hao ambao kwa sasa ni majeruhi na wako hospitalini, walisema chanzo cha ajali hiyo ni mwendo kasi wa dereva Makame aliyekuwa amepokea gari kutoka kwa dereva mwenzake (jina halijafahamika) na kwamba walitembea masafa mafupi na kupata ajali.

Kaimu Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Sokoine, Dk. Jumanne Shija, alithibitisha kupokea miili ya watu wanne wote wakiume na majeruhi sita.

Alitaja majina ya marehemu kuwa ni Hassan Msata (42) mkazi wa Mbagala jijini Dar es Salaam, Abdallah Mussa (19) wa Mmumbu, Muhibu Mbaraka (25) mkazi wa Kariakoo mjini Lindi na Samuel Rioba (33) mwenyeji wa Mwanza.

Dk. Shija pia aliwataja majeruhi kuwa ni Robson Molen (26), Sabiini (60) aliyeumia usoni na bega la kushoto, Chapuchapu aliyeumia kichwani, Aziz Mkeka (41), Abdallah Mambo (36), Said Ismail (28), Mwanaidi Ahmed (5), Shufaa Matola (24), Ally Ngele (41) na mwingine ambaye jina lake halikufahamika mara moja, wote wakazi wa Manispaa ya Lindi.

Alisema katika majeruhi hao, wawili akiwamo dereva wa Kampuni ya Dangote, Ally Ngele na Abdallah Mambo, wamehamishiwa Hospitali ya Taifa Muhimbili, Dar es Salaam kutokana na kuumia vibaya maeneo ya kichwani na maeneo mengine ya miili yao.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP) Pudenciana Protas, alipopigiwa simu ili kupata kauli yake, alisema yuko kwenye kikao na kumtaka mwandishi aende kesho ofisini kwake.

# Mtoto adai alimwona baba wa kambo akimuua mamaye

**Na Hellen Mwango**

MTOTO Hassan Hussein (10) amedai mahakamani katika kesi ya mauaji ya mama yake mzazi, Bahati Hussein, kwamba alimwona baba yake wa kambo, Godfrey Nkwambi, akimnyonga mama yake na kumwamuru asipige kelele.

Ushahidi huo aliutoa jana mbele ya Naibu Msajili wa Mahakama Kuu, Pamela Mazengo, katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu, Dar es Salaam, iliyopewa mamlaka ya kusikiliza kesi za mauaji.

Hassan ambaye alilala chumbani kwa mama yake (wakati huo akiwa na miaka mitano), alidai kuwa siku ya tukio alimwona baba yake wa kambo ni mshtakiwa katika kesi hiyo, alitoa madai hayo wakati akitoa ushahidi dhidi ya mauaji hayo.

Akiongozwa na Wakili wa Serikali, Erick Shija, shahidi huyo alidai siku ya tukio akiwa amelala chumbani kwa mama yake chini kwenye godoro pamoja na mdogo wake aliyemtaja kwa jina la Ibrahim, kwa kawaida mama yake na baba yake wa kambo walikuwa wakilala kitandani.

Siku ya tukio, alidai kuwa usiku alishtuka na alimuona mshtakiwa (baba wa kambo) akimnyonga mama yake na alimwambia asipige kelele na mama yake alikuwa akitikisa miguu huku akitoa sauti kwa mbali.

"Nililala lakini niliposhtuka nilimwona mshtakiwa akifanya hivi halafu hivi (alionyesha mahakama mikono ya mshtakiwa ilivyokuwa imeshika kichwa na kidevu na kukizungusha). Mama alikuwa akipiga miguu kitandani na kutoa kelele kwa mbali, God aliniambia nisipige kelele, mimi nikanyamaza, nikamwona akitoka nje sikujua kilichoendelea kwani niliendelea kulala hadi asubuhi," alidai Hussein.

Alidai kuwa asubuhi alimwacha mama yake akiwa bado amelala, yeye akatoka nje kupiga mswaki na baadaye alikwenda kucheza.

"Siku hiyo sikumwona Godfey na sikujua alikokwenda lakini baadaye nilisikia watu wakilia nyumbani kwetu, ndugu zangu wakaniambia mama yetu mzazi amefariki (dunia)," alidai shahidi huyo na kusababisha ndugu wa marehemu waliofika mahakamani kusikiliza kesi hiyo kuanza kutoa machozi.

Shahidi mwingine ni mtoto wa marehemu, Khadija Abibu (15),

INAENDELEA UK. 8

ACB
AKIBA COMMERCIAL BANK PLC

TAARIFA YA KUAHIRISHWA KWA MKUTANO MKUU WA MWAKA KWA WANAHISA WA AKIBA COMMERCIAL BANK PLC

Kwa Wanahisa Akiba Commecial Bank Plc

Notisi hii imetolewa kuwataarifu kuwa mkutano mkuu wa mwaka wa Wanahisa wa Akiba Commercial Bank Plc uliopangwa kufanyika Jumamosi ya tarehe 27 Julai 2019 umeahirishwa mpaka Jumamosi ya tarehe 9 Novemba 2019.

Maelezo zaidi kuhusiana na kikao yatatolewa baadaye.

215307202

www.acbtz.com
benki kwa maendeleo yako

# Hasunga sasa ataka kilimo hifadhi

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

WAZIRI wa Kilimo, Japhet Hasunga, amesema ili Tanzania ifikie uchumi wa kati ifikapo mwaka 2025 ni lazima iwekeze katika kilimo hifadhi na kuhamasisha matumizi ya teknolojia za kisasa.

Hasunga aliyasema hayo jana jijini hapa wakati akifungua warsha ya wadau wa kilimo hifadhi Tanzania.

"Serikali itaendelea kuweka mazingira rafiki. Mfano tumefuta kodi nyingi lakini ni lazima tuhamasishane matumizi ya teknolojia za kisasa ambazo ni rafiki, ni muhimu tujadiliane pamoja kuruhusu sheria kwani hatuwezi kufika uchumi wa kati bila kufikia kilimo imara na chenye tija," alisema.

"Lazima kuimarishwe mafunzo kwani kilimo nchini bado kiko chini. Pia tuongeze utafiti kwa

INAENDELEA UK. 8



Wafanyabiashara wadogo wakiwa wamepanga bidhaa zao katika eneo la waenda kwa miguu katika Barabara ya Uhuru, eneo la Ilala Mchikichini, jijini Dar es Salaam jana na kusababisha kupita kwenye barabara ya magari jambo ambalo ni hatari kwa usalama barabarani. **PICHA: GETRUDE MPEZYA**

# Majaliwa aipigia chapuo Vietnam kununua korosho

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa, amewakaribisha wafanyabiashara kutoka nchini humo kununua korosho nchini ambazo zipo za kutosha.

Pia amewataka wenye uwezo kutoka nchini humo, kujenga viwanda vya kuchakata korosho na kuahidi kuwa serikali iko tayari wakati wowote kuwasaidia pamoja na uwekezaji katika sekta zingine ikiwamo ya viwanda.

Majaliwa aliyasema hayo jana alipokutana na kufanya mazungumzo na Balozi wa Vitemam nchini, Balozi Nguyen Doanhm, ofisini kwa Waziri Mkuu, Magogoni jijini Dar es Salaam.

Waziri Mkuu alisema Rais John Magufuli ameanzisha Wizara ya Uwekezaji iliyo chini ya Ofisi ya Waziri Mkuu kwa ajili ya kuifanya Tanzania kuwa mahali bora na salama kwa wawekezaji na wafanyabiashara.

Alisema ununuzi wa mazao ya kilimo kama vile pamba, korosho, kahawa na tumbaku ni fursa nyingine ya kibiashara ambayo wafanyabiashara wa Vietnam wanakaribishwa kuichangamkia.

Pia alitumia fursa hiyo kuwaalika wafanyabiashara na wawekezaji kutoka Vietnam kuwekeza katika sekta ya viwanda hususani vile vinavyotumia malighafi za mazao ya kilimo zinazopatikana nchini na kwamba hatua hiyo itawawezesha wakulima wa Tanzania kuwa na soko la uhakika la mazao yao.

"Serikali imeendelea kuondoa vikwazo vya kuanzisha na kuendesha biashara kwa kupitia upya sheria, kanuni na taratibu za biashara na kuzifuta zile ambazo zimethibitika kuwa zinayafanya mazingira ya biashara na uwekezaji kuwa magumu," alisema.

Kwa kuwa Vietnam imepiga hatua kubwa katika ujenzi na uendeshaji wa viwanda vya nguo, alisema Tanzania ingefurahi kuona viwanda vya aina hiyo vinajengwa nchini na wawekezaji kutoka nchi hiyo.

Kwa upande wake, Balozi Doanh alimweleza Waziri Mkuu juu wa ujio wa Naibu Waziri Mkuu wa Vietnam, Trinh Dinh Dung, anayetarajiwa kufanya ziara yake ya kikazi nchini kuanzia Julai 9 hadi 11, mwaka huu.

Alisema Naibu Waziri Mkuu huyo anatarajiwa kuambatana na wafanyabiashara wasiopungua 20 kutoka kampuni kubwa za Vietnam. Nchi za Vietnam na Tanzania zilianzisha uhusiano wa kidiplomasia mwaka 1965 na mwaka 1984, Vietnam ilifungua ofisi ya ubalozi wake hapa nchini kwa muda na kuufungua upya mwaka 2003.




# Waziri aanika sababu foleni mizigo bandarini

**Na Mary Geofrey**

WAZIRI wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Isack Kamwelwe, amesema mrundikano wa malori ya mizigo katika Bandari ya Dar es Salaam unasababishwa na baadhi ya taasisi zinazofanya kazi na Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari Tanzania (TPA) ambazo hazijaanza kufanya kazi kwa saa 24 kama ilivyoelezwa.

Tangu Septemba 18, 2017 serikali ilipitisha sheria ya kuzitaka taasisi zote za umma, kufanya kazi kwa saa 24, lakini baadhi hazijadai agizo hilo, hivyo kusababisha kuchelewa kutolewa kwa mizigo.

Kamwelwe aliyaeleza hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akizungumza na waandishi wa habari katika mkutano wake na wachimbaji wakubwa wa madini duniani na wafanyabiashara waliokutana kwa lengo la kujadili changamoto zinazokwamisha kupitisha mizigo katika bandari hiyo kwa asilimia 100 na kiwango cha utoaji mizigo ni asilimia 25 hadi 40.

"Kumekuwapo na upotoshaji mkubwa kuwa mzani uliopo katika Bandari ya Dar es Salaam unasababisha foleni ya malori kutoka bandarini. Hilo si kweli kwani kuna mizani miwili na zinafanya kazi vizuri bila matatizo yoyote na kwa sekunde 55 yanapimwa malori mawili tena inafanya kazi kwa saa 24," alisema.

"Kinachosababisha foleni ni changamoto zetu wenyewe watu wa TPA na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) na mamlaka zingine zinazofanya kazi na bandari ambazo zinatakiwa kufanya kazi kwa saa 24 lakini hazifanyi hivyo," alisema.

Kamwelwe alisema ili kumaliza changamoto hiyo, ameshamwandikia barua Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Philip Mipango, ili watumishi wa wizara hiyo wafanye kazi katika bandari hiyo ambayo ina jengo refu linaloweza kutosha watumishi wa idara zote.

Kuhusu mkutano huo, Kamwelwe alisema walikutana na wawakilishi wa zaidi ya kampuni 10 zikiwamo za Bridge Shipping, Acess World, Impala Terminals, Trafigula and Reload Logistics ambazo zinasafirisha madini kwenda nchi mbalimbali duniani, ikiwamo China. Alisema katika mkutano huo wafanyabiashara hao wamelalamikia mizigo kuchelewa kutoka bandarini, kuwapo kwa sera ambazo hazina uwiano na nchi zingine wanazoshirikiana nazo hasa usawa wa mizigo.

Kamwelwe alisema wameahidi kuzifanyia kazi changamoto hizo ikiwamo kushirikiana na taasisi zingine kufanya kazi kwa saa 24 katika bandari hiyo na watakutana tena mwezi ujao kujadili kama wameridhishwa na maboresho yanayofanywa.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa TPA, Deusdedit Kakoko, alisema tangu Jumapili iliyopita, zaidi ya malori 300 yameshapimwa na kupita katika mzani huo hali inayoonyesha mzani si changamoto.

# Ugomvi wa panga wadaiwa chanzo mauaji ya bibi kizee

**Na Said Hamdani,** LINDI

JESHI la Polisi mkoani Lindi, linamshikilia mkazi wa Kijiji cha Rondo-Ntene, mkoani hapa, Aisha Mshamu (65), kwa tuhuma za kumuua Zainabu Mikumbi (80) kwa madai ya ugomvi unaoelezwa ulisababishwa na kugombea panga lililopotea mwaka jana.

Habari kutoka kijijini huko na kuthibitishwa na uongozi wa kijiji zimedai kuwa ugomvi wa wawili hao ulianza tangu Desemba, mwaka jana, hadi Juni 29, mwaka huu, saa 10:00 alasiri kwa Zainabu kufa kwa kupigwa na Aisha wakiwa shambani.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Rondo-Ntene, Hamisi Mohamed, amekiri kwamba mabibi hao kutokuwa na maelewano mazuri kuanzia wakati huo.

"Mwaka jana Desemba mabibi hawa walishafika ofisini kwangu wakiwa na ugomvi. Niliwasuluhisha lakini inavyoonekana bado walikuwa na vinyongo," alisema.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Lindi, Kamishna Msaidizi (ACP), Pudenciana Protas, alithibitisha kuwapo taarifa za mauaji hayo na kutaja chanzo kuwa ni ugomvi uliotokana na Mikumbi kupoteza panga lake Desemba, mwaka jana.

"Mwaka jana Zainabu (Mikumbi) akiwa anatoka shambani kwake njiani alikutana na Aisha Mshamu na kumweleza amepoteza panga lake na kama ataliona ampelekee," alisema Kamanda Protas.

Alisema ilipofika Juni 29, mwaka huu, saa 10 alasiri, Mikumbi akiwa na jembe mkononi, alikwenda shambani kukata nyasi za kuezekea nyumba yake wakati Mshamu alikuwa amekwenda huko kwa lengo la kuchimba dawa na kuanza ugomvi.

Kamanda Protas alisema katika ugomvi wao huo, Mshamu alichukua jembe la Mikumbi na kumpiga nalo kichwani na shingoni na hatimaye kuanguka chini na kupoteza fahamu.

Alisema baada ya kutenda jambo hilo, Mshamu aliondoka na kwenda katika Ofisi ya Mtendaji wa Kijiji cha Rondo-Ntene na kupatiwa barua kwenda Kituo cha Afya cha Rondo kwa ajili ya kutibiwa.

Wakati akienda kutibiwa, Mtendaji wa Kijiji akaagiza askari mgambo kwenda kumkamata Mikumbi, lakini wakiwa njiani walikutana na ndugu zake wakiwa wamembeba kwenye machela kumpeleka Kituo cha Afya cha Rondo kwa matibabu kutokana na majeraha aliyoyapata.

"Zainabu (Mikumbi) baada ya kufikishwa kituoni hapo alibainika kuwa ameshafariki dunia," alisema Kamanda Protas.

Kutokana na tukio hilo, alisema polisi wanamshikilia Mshamu kwa mahojiano kutokana na tuhuma za mauaji ya bibi kizee huyo na anatarajiwa kufikishwa mahakamani kujibu shtaka linalomkabili baada ya kukamilika kwa upelelezi.

# Serikali yashauriwa kupitia upya Sheria ya Wakimbizi

**Na Mwandishi Wetu**

SERIKALI imeshauriwa kupitia upya Sheria ya Wakimbizi ya mwaka 1998, Sera 2003 na Kanuni zake ili ziweze kuona na mikataba mbalimbali ya kimataifa ambayo nchi imeingia.

Ushauri huo umetolewa na Mhadhiri Mwandamizi wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM) Kitivo cha Sheria Profesa Khoti Khamanga wakati wa semina kwa wadau wa sekta binafsi na Serikali iliyofanyika jijini Dar es Salaam.

Prof.Kamanga ambaye aliwasilisha mada kuhusu hali ya wakimbizi na umuhimu wa kuwa na nyaraka kwa kundi hilo alisema Sheria ya 1998 na Sera 2003 hazina oani jambo ambalo linaenda kinyume na mikataba mbalimbali ambayo nchi imesaini.

Alisema Tanzania imesaini mkataba wa Umoja wa Mataifa wa Wakimbizi wa mwaka 1951, Mkataba wa Umoja wa Afrika 1969 na Mkataba wa Maziwa Makuu 2006 ambayo maelekezo yake hayawezi kutekelezwa kwa Sheria na Sera iliyopo.

"Sheria yetu ni mwaka 1998 Sera ya 2003 lakini kiutaratibu huwa inaanza Sera ndio sheria jambo ambalo halipo. Lakini pia ndani ya Sheria na Sera inahitajika kuona mikataba ya kimataifa ikiwa ndani jambo ambalo halipo," alisema

Alisema katika eneo hilo la wakimbizi ipo mchangamoto za kikahuni hivyo Serikali inatakiwa kuangalia kwa jicho pana.

Mhadhiri huyo alisema ushauri mwingine ambayo anautoa kwa Serikaki ni kuwarasimisha wakimbizi ili wawe na faida kwa nchi kwa kuongeza mapato kwa kulipa kodi.

Alisema bila sheria kuona na mikataba mbalimbali ambayo nchi imeingia inayopata hasara ni Serikali.

Aidha, alisema idadi ya wakimbizi wanaokimbilia nchi za nje imepungua ambapo kwa sasa wapo milioni 25 huku wakimbizi zaidi ya milioni 40 wakiwa wanakimbia ndani ya nchi husika.

Prof.Kamanga alisema taarifa zinazooneshwa kuwa wakimbizi kutoka nchi za Afrika kuingia Ulaya sio za kweli kwani idadi kubwa wanakimbilia nchi za Afrika.

"Inakadiriwa kwa sasa wakimbizi wa nje wamepungua ila wa ndani ya nchi wameongezeka. Lakini pia kwa miaka ya sasa Serikaki hazitaki kujali wakimbizi kama zamani," alisema.

Kwa upande wake Mkurugenzi Msaidizi Wizara ya Mambo ya Ndani anayeshughulikia Makambi na Makazi ya Wakimbizi Nsato Marijani alisema semina hiyo iliyoandaliwa na Taasisi ya Dignity Kwanza imekuja wakati muafaka kwao ili kupata uelewa kuhusu uwepo wa nyaraka sahihi kwa kundi hilo.

Alisema iwapo idadi ya wakimbizi itafahamika

INAENDELEA UK. 8

**THE UNITED REPUBLIC OF TANZANIA**
**MINISTRY OF EDUCATION, SCIENCE AND TECHNOLOGY**
**AGENCY FOR THE DEVELOPMENT OF EDUCATIONAL MANAGEMENT (ADEM)**

**Tender No. AE/014/2019/20/NC/01**
**for**
**Provision of catering services for students**

**Invitation for Tender**

**Date: 04th July, 2019**

1. This Invitation for Tenders follows the General Procurement Notice for this Project which was advertised in PPRA website.
2. The Government of Tanzania has set aside funds for the operation of the Agency for the Development of Educational Management (ADEM) during the financial year 2019/20. It is intended that part of the proceeds of the fund will be used to cover eligible payment under the contract for the provision of catering services for students.
3. The Agency for the Development of Educational Management now invites sealed Tenders from eligible National providers of catering services for students.
4. Tendering will be conducted through the National competitive bidding procedures specified in the Public Procurement Act No. 7 of 2011 and Regulations, 2013 – Government Notice No. 446 and is open to all Tenderers as defined in the Regulations.
5. Interested eligible Tenderers may obtain further information from and inspect the Tendering Documents at the office of the **Secretary, ADEM Tender Board** near Roman Catholic Church, **P.O.Box 71, Bagamoyo, COAST REGION from 9.00am to 3.00 pm** on Mondays to Fridays inclusive except on public holidays.
6. A complete set of Tendering Documents in English language and additional sets may be purchased by interested Tenderers on the submission of a written application to the address given under paragraph 5 above and upon payment of a non-refundable fee of Tanzanian shillings fifty thousand only **(50,000/=)**. Payment should either be by Cash deposit or Banker's Cheque, payable to **Control Number 991250003022 at any bank and submit bank deposit slip for receipt.**
7. All Tenders must be accompanied by a Tender Securing Declaration in the format provided in the Tendering Documents.
8. All Tenders in one original plus two copies, properly filled in, and enclosed in plain envelopes must be delivered to the address below on or before **Friday, 26th July, 2019, 11.30** morning. Tenders will be opened promptly thereafter in public and in the presence of Tenderers' representatives who choose to attend in the opening at the **ADEM BOARD ROOM (MAB), near Roman Catholic Church.**
9. Late Tenders, portion of Tenders, electronic Tenders, Tenders not received, and not opened and not read out in public at the Tender opening ceremony shall not be accepted for evaluation irrespective of the circumstances.

**CHIEF EXECUTIVE**
**ADEM**

**Chief Executive,**
**ADEM Tender Board,**
**Opposite Roman Catholic Church,**
**P. O. Box 71 Bagamoyo,**
**COAST REGION.**

215308802

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA**
**WAKALA WA MAENDELEO YA UONGOZI WA ELIMU (ADEM)**

**TANGAZO LA ZABUNI**

**ZABUNI YA KUENDESHA MADUKA NA HUDUMA YA KURUDUFU (CONSUMABLE SHOPS AND SECRETARIAL SERVICES) KATIKA KAMPASI YA BAGAMOYO KWA MIAKA YA FEDHA 2019-2020 NA 2020-2021.**

**04/07/2019**

1) Mtendaji Mkuu wa Wakala wa Maendeleo ya Uongozi wa Elimu (ADEM) anawatangazia wafanya biashara wenye uwezo wa kutoa huduma za maduka na huduma za kurudufu (Consumable shops & Secretarial services) katika Maduka manne yaliyopo katika Kampasi ya Bagamoyo kwa muda wa miaka miwili unaoanzia tarehe 01/08/2019 hadi tarehe 30/6/2021 kama Ilivyoainishwa hapo chini:-

2) Nafasi zInazotangazwa kwa kIpindi hicho ni kama zifuotazo:-

**ZABUNI ZA MIAKA MIWILI(2)**

| NAMBA YA ZABUNI | JINA LA ZABUNI |
|---|---|
| EA/014/2019/2020/NC/02 | Ukodishaji wa maduka (Consumable shops), nafasi 2 (Lot 1 & 2) |
| EA/014/2019/2020/NC/03 | Ukodishaji wa maduka ya kurudufu (secretarial services) nafasi 2(Lot 1 & 2) |

3. MASHARTI YA MWOMBAJI.
i) Awe na kampuni au jina la Biashara lillyosajiliwa na Mamlaka husika
ii) Awe na Leseni, TIN na VAT hai ya biashara husika
iii) Awe na risiti ya EFD iliyosajiliwa na Mamlaka ya Mapato (TRA) kwa jina la biashara au kampuni husika.
iv) Ada ya maombi ya zabuni ni Tshs. 50,000/= kwa zabuni, ambazo hazitarudishwa.
v) Hairuhusiwi kuomba loti zaidi ya moja
vi) Wafanyabiashara wenye mikataba na Wakala wa Manunuzi ya Umma (GPSA) kwa huduma hizo watakuwa na sifa za nyongeza japo sio kigezo cha lazima
vii) waombaji wanaruhusiwa kukagua maeneo ya biashara kabla ya kununua kabrasha la zabuni.
4. Vitabu vya Zabuni na maelezo mengine vinapatikana Ofisi ya Mtendaji Mkuu - ADEM, S.L.P. 71, Bagamoyo, Barabara ya Miembe Misafa, Mkabala na Kanisa Katoliki,(Kitengo cha Ununuzi na Ugavi) kuanzia Saa 3.00 asubuhi mpaka Saa 9.00 alasiri Jumatatu — Ijumaa isipokuwa siku za sikukuu kwa malipo yasiyorejeshwa ya shilingi 50,000/=. kwenye akaunti ya ADEM kwa kutumia namba ya kumbukumbu 991250003022 kwa benki yoyote na kuwasilisha nakala ya benki ya malipo hayo kwa kupatiwa risiti (Bank deposit slip)
5. Nyaraka za maombi ziwe na nakala mbili pamoja na nakala halisI moja iliyofungwa kwa LAKIRI, iandikwe juu ya bahasha "NAMBA NA JINA LA ZABUNI ILIYOOMBWA PAMOJA NA LOTI NAMBA na zitumbukizwe katika sanduku la zabuni lililoko Ofisi ya Manunuzi (PMU) Kampasi ya Bagamoyo baada ya kusajiliwa. ziwe na anwani ifuatayo: MTENDAJI MKUU ADEM, S.L. P. 71, BAGAMOYO.
6. Mwisho wa kupokea maombi ya zabuni ni tarehe 26/07/2019 saa tano na nusu asubuhi (5:30) siku ya Ijumaa. Zabuni zitafunguliwa muda huo huo katika ukumbi wa mikutano wa Bodi (MAB) uliopo katika Kampasi ya Bagamoyo na waombaji mnakaribishwa katika ufunguzi kwa gharama zenu.

**Dr. Siston M. Mgullah**

215308802

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ni wakati mwafaka wakazi wa Kipunguni kulipwa fidia

**SASA** ni zaidi ya miaka 22 tangu Serikali ilipofanya tathmini ya kuwahamisha wakazi wa eneo la Kipunguni kupisha upanuzi wa Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere (JNIA) jijini Dar es Salaam.

Hatua hiyo ya Serikali imewaweka kwenye wakati mgumu wakazi wa eneo hilo, baada ya kushindwa kuwalipa kwa wakati fidia zao, huku ikiwa imeweka zuio la kutoendelezwa ikiwamo shughuli za ujenzi wa aina yoyote.

Tathmini ilifanywa mwaka 1997 wakati huo Serikali ilikuwa inaongozwa na Rais wa awamu ya tatu, Benjamin Mkapa, kisha alipokelewa kijiti na Rais Jakaya Kikwete mwaka 2005 -2015 alipompisha Rais John Magufuli.

Ni jambo linalosikitisha jinsi ambavyo wakazi hao wameishi miaka yote hiyo katika hali ya kuzuiliwa kufanya maendeleo kwenye makazi yao, pia kunyimwa kupata huduma muhimu ikiwamo kuunganishiwa mabomba ya maji.

Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, juzi alipohojiwa na Nipashe kuhusu fidia hiyo, alijibu kuwa ni suala linalopaswa kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Majibu ya Waziri yanazua maswali ikiwamo ni sheria ipi inayoelekeza malipo hayo yacheleweshwe kwa miaka yote hiyo, huku wananchi wakizuiliwa kuendeleza ujenzi katika maeneo ya makazi yao. Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano Mei mwaka 2017, ilielieza Bunge kuwa imetenga Sh. bilioni 30 katika mwaka wa fedha 2017/2018 ili kukamilisha malipo ya fidia kwa wananchi wa Kipunguni wanaopisha upanuzi wa uwanja huo wa ndege.

Aliyekuwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Edwin Ngonyani, alilijulisha Bunge kuwa kutokana na gharama za fidia na uhaba wa fedha, Serikali imekuwa ikilipa fidia kwa wakazi hao kwa awamu.

Katika mwaka 2013/14 Serikali ililipa Sh. bilioni 1.2 ikiwa ni fidia kwa wakazi 59 kati ya wakazi 801 kwa eneo la Kipunguni ambapo wakazi 742 ndio hawajalipwa fidia zao.

Je, fedha hizo ambazo Serikali ilitangaza kuwalipa wakazi hao zilikwenda wapi hadi hawajalipwa? Na kama imekwama kuwalipa kwa nini isiwaruhusu waendelee kufanya shughuli za maendeleo?

Ajabu katika jambo hili ni kwamba pamoja na wakazi hao kukwamisha kufanya shughuli za maendeleo katika maeneo hayo, wamelalamika kuwa pia hawajapewa leseni za makazi hivyo wanashindwa hata kupata mikopo ya kuwawezesha wajikwamue kiuchumi.

Serikali ya awamu ya tano tayari imefanya mambo mengi ya maendeleo chini ya uongozi wa Rais Magufuli, tunaamini kwamba sasa itaona umuhimu wa kuhakikisha ahadi ya kulipwa kwa fidia kwa wakati wa eneo la Kipunguni inatekelezwa.

Kadhalika, serikali ya sasa imekuwa ikisisitiza kuwa lazima viongozi wahakikishe wanashughulikia na kutafutia ufumbuzi kero mbalimbali zinazowakabili wanyonge, hivyo tunaamini kuwa wahusika hususan wizara watamaliza suala hilo haraka.


Wakazi hawa wamekuwa ni watulivu ndani ya maumivu mengi ikiwamo kushuhudia maeneo ya wenzao yakistawi kwa maendeleo wakati katika maeneo yao nyumba zina mwonekano wa kuchakaa ikiwamo mabati kujaa kutu. Pia wengine wamekufa wakiwa wanasubiri utekelezaji wa ahadi hiyo.

Tunaamini kuwa hatua ya kuwalipa fidia yao ikitekelezwa itawafanya nao waweze kujiendeleza kiuchumi hivyo kuleta maendeleo kwenye familia zao, mkoa na taifa kwa ujumla.

Kadhalika, ufumbuzi huo utawaondolea usumbufu viongozi mbalimbali wakiwamo wawakilishi wa wananchi, ambao kila uchao wamekuwa wakihangaikia suala hilo.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Meneja Matangazo:** Kauthar D'souza, 0767 223311.
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Tumieni fursa hii kujipima dengue



Na Sabato Kasika

**MEI** mwaka huu, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dar es Salaam Dk. Yudas Ndugile, aliwataka wakazi wa jijini kuchukua tahadhari kipindi cha mvua kwa kusafisha mitaro na maeneo yanayowazunguka, ili kujiepusha na ugonjwa wa dengue.

Dk. Ndugile anasisitiza juu ya uvaaji wa mavazi marefu yanayoziba sehemu ya mikono na miguu ili kuwaepusha na maambukizi ya ugonjwa huo unaoletwa na vimelea vinavyosambazwa na mbu aina ya Aedes Egyptae.

Kwa mujibu wa Dk. Ndugulile, mbu huyo hupendelea kuishi karibu na makazi ya watu na huweza kuuma binadamu mchana na usiku, hatimaye kumsababisha ugonjwa huo.

Mbali na hayo, anawataka wananchi kuwahi katika vituo vya afya mapema pale wanapohisi dalili za ugonjwa huo, badala ya kunywa dawa kiholela, hali ambayo inaweza kuwaletea madhara zaidi.

Dalili za ugonjwa huo zimeshawekwa wazi kuwa ni homa kali ya ghafla, maumivu makali ya kichwa, macho kuuma, maumivu ya viungo, kichefuchefu, kutapika, vipele ambavyo hutokea siku nne baada ya homa kuanza na kutoka damu puani, kwenye fizi na kuchubuka kirahisi.

Nikirejea kwenye hoja ni kwamba serikali imeamua kutolewa bure vipimo vya ugonjwa huo kwenye vituo vya afya vya umma ili kupambana nao usiendelee imepoteza maisha ya Watanzania.

Lakini kama kawaida ya baadhi ya Watanzania, inawezekana baadhi wakazembea kutumia fursa hiyo ya kwenda kwenye vituo hivyo ili kupima ugonjwa huo wanapobaini dalili zake. Kwa kuwa serikali imeshatangaza kwamba vipimo vya ugonjwa huo ni bure, basi kila mmoja hana budi kuchukua hatua ya kwenda kwenye kituo cha afya cha umma kuliko kuzembea na kujikuta akipoteza maisha.

Inaelezwa kuwa mara nyingi dalili huwa sio kali na wengi hudhani ni homa ya mafua au maambikizi mengine ya virusi na kwamba dalili hizo huanza kutokea baada ya wiki mbili, lakini kwa wengi huchukua wiki moja ya kwanza na tayari ataanza kuona dalili za dengue.

Lakini kwa sababu tayari kila kitu kimeshaweka wazi, sidhani kwamba kuna haja ya kuzembea kama ambavyo baadhi ya watu wamekuwa wakizembea hata kwenye ugonjwa wa kipindupindu.

Kwa mfano kwenye suala la kujikinga na ugonjwa wa kipindupindu, watu wamekuwa wakihimizwa kuzingatia usafi ili kuepuka ugonjwa, lakini baadhi yao hawako makini.

Unaweza kukuta wakitiririsha majitaka mitaani, kutochemsha maji ya kunywa au kwa ujumla wake kutozingatia kanuni za afya na kusababisha ugonjwa huo kuendelea kuwanyemelea.

Inawezekana ni kutokana na kutozingatia maelekezo ya wataalamu wa afya au kutojua chochote, lakini jambo la msingi hapa ni kuwa makini kwa kufuata kile kinachoelekezwa.

Wakati mwingine inawezekana hata uamuzi uliochukuliwa na serikali wa kupima watu bure homa ya dengue ukawapita wengine ndio maana nikasema hiyo fursa ichangamkiwe.

Mtindo wa kuzembea mambo ya msingi haupaswi kupewa nafasi. Hili suala la homa ya dengue wasiwapo watu kuzembea pale wanapohisi kuwa na dalili za homa hiyo wakajikuta kwenye hatari ya kupoteza maisha.

Hii ndio inanifanya niwakumbushe kuwa serikali imeshaamua kutoa bure vipimo vya homa ya dengue, hivyo ni vyema fursa hiyo isipite bure bali waitumie ili kujihakikishia usalama wa afya zao.

Kama alivyosema bungeni hivi karibuni, Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, Ummy Mwalimu aliweka wazi kuwa mbali na kutoa vipimo bure, wizara imeshanunua lita 60,000 za viua vidudu.

Kwamba lita hizo zimesambazwa kwenye mlipuko wa ugonjwa huo ikiwamo halmashauri tano za Mkoa wa Dar es Salaam, Geita, Kagera, Kigoma, Lindi, Mtwara, Pwani, Morogoro, Tanga na Singida.

Aidha, anasema serikali imeshaagiza mashine kubwa sita kwa ajili ya kupulizia mbu, ambazo zinatarajiwa kufikishwa nchini mwishoni mwezi huu.

Pamoja na hayo suala la msingi ni kwamba hatua ya kuruhusu watu kupimwa bure homa ya dengue ni ya msingi hasa kutokana na hali ya wengi wao kiuchumi siyo hivyo ni muhimu kuchangia fursa hiyo ya kupmwa bure.

Kila mmoja akizingatia kile kinachoelezwa na wataalamu wa afya kujikinga na ugonjwa huo na pia kwenda kwenye vituo vya afya, mapambano dhidi ya dengue yanaweza kuwa na mafanikio makubwa.

## TANGAZO

# FARM AFRICA

## PUBLICATION OF FINANCIAL STATEMENTS

In accordance with Non-Government Organisations (Amendment) Regulation, 2018 Farm Africa is pleased to publish its financial statements and funding status for the period ended 31 December 2018.

### STATEMENT OF INCOME AND EXPENDITURE FOR THE YEAR ENDED 31 DECEMBER 2018

| | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|
| **Income** | | |
| Receipts from Donors and Trust | **5,719,961,109** | 5,664,870,234 |
| Other Income | **470,440,930** | 787,691,222 |
| **Total Income** | **6,190,402,039** | 6,452,561,456 |
| **Expenditure** | | |
| Capital Expenditure | **1,386,500** | 25,924,798 |
| Staff Costs | **1,407,285,470** | 1,447,185,291 |
| Support Costs | **50,284,767** | 143,979,155 |
| Support to local partners | **3,025,078,529** | 2,672,520,800 |
| Training | **202,466,890** | 388,091,266 |
| Programme Development | **26,963,290** | 130,221,019 |
| Marketing and Advertising | **11,534,333** | 49,545,774 |
| Monitoring and Supervision | **609,990,645** | 803,709,447 |
| Dissemination | **212,660,908** | 70,285,663 |
| Project Running | **421,615,673** | 482,941,882 |
| **Total Expenditure** | **5,969,267,005** | 6,214,405,095 |
| **Operating surplus for the year** | **221,135,034** | 238,156,360 |

### STATEMENT OF FINANCIAL POSITION AS AT 31 DECEMBER 2018

| | 2018 TZS | 2017 TZS |
|---|---|---|
| **ASSETS** | | |
| **Current assets** | | |
| Debtors and Accrued Income | 1,483,911,098 | 202,798,377 |
| Bank and Cash | 795,545,573 | 130,867,049 |
| **TOTAL ASSETS** | **2,279,456,671** | 333,665,426 |
| **LIABILITIES** | | |
| **Current liabilities** | | |
| Creditors | 2,718,697,523 | 994,041,312 |
| | **2,718,697,523** | 994,041,312 |
| **NET LIABILITIES** | **(439,240,852)** | (660,375,886) |
| **GRANT FUND** | | |
| At 1 January | (660,375,886) | (898,532,246) |
| Surplus for the year | 221,135,034 | 238,156,360 |
| **At 31 December** | **(439,240,852)** | (660,375,886) |

### Funding Analysis for the year ended 31 December 2018

| | Food Trade Project | Country Office | Nutrition Project | Sesame III Project | Sunflower Project | Food Trade Extension Project | Grand Total |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **EXPENDITURE** | | | | | | | |
| Capital expenditure | | 1,386,500 | | | - | | 1,386,500 |
| Dissemination | 148,346,884 | 670,400 | | | - | 63,643,624 | 212,660,908 |
| Monitoring and Supervision | 171,898,063 | 36,357,551 | 55,582,050 | 78,973,938 | 44,086,595 | 223,092,448 | 609,990,645 |
| Programme Development | 7,280,000 | 9,379,360 | | | 10,303,930 | - | 26,963,290 |
| Project Running | 23,589,256 | 213,550,540 | 3,540,000 | 11,982,930 | 31,867,005 | 137,085,942 | 421,615,673 |
| Staff costs | 149,587,861 | 412,803,374 | 47,201,950 | 89,202,975 | 281,723,386 | 426,765,924 | 1,407,285,470 |
| Support costs | 11,485,000 | | | | 2,839,767 | 35,960,000 | 50,284,767 |
| Training | 21,230,000 | | 16,834,000 | 24,036,888 | 76,920,062 | 63,445,940 | 02,466,890 |
| Support to local partners | 452,683,480 | | 176,288,101 | 327,204,893 | - | 2,068,902,055 | 3,025,078,529 |
| Marketing and Advertising | 805,000 | | | | - | 10,729,333 | 11,534,333 |
| **Grand Total** | **986,905,545** | **674,147,725** | **299,446,101** | **531,401,624** | **447,740,745** | **3,029,625,266** | **5,969,267,005** |
| **INCOME** | | | | | | | |
| Project Recharges Income | | 423,444,590 | | | | | 423,444,590 |
| Other Income | | 23,762,731 | | | | | 23,762,731 |
| AMDT Income | | | | | 231,365,902 | | 231,365,902 |
| Big Lottery Fund Income | | | 343,410,087 | | | | 343,410,087 |
| Comic Relief Income | | | | 370,858,411 | | | 370,858,411 |
| DFID/DAI Income | 1,805,611,314 | 23,233,609 | | | | 2,968,715,395 | 4,797,560,318 |
| **Grand Total** | **1,805,611,314** | **470,440,930** | **343,410,087** | **370,858,411** | **231,365,902** | **2,968,715,395** | **6,190,402,039** |
| **Surplus/(Deficit)** | **818,705,770** | **(203,706,795)** | **43,963,986** | **(160,543,213)** | **(216,374,843)** | **(60,909,871)** | **221,135,034** |

The financial statements were authorised for issue by the Management on April 2019 and were signed on its behalf by: Farm Africa Management

**Tanzania Country Office:**
**Amverton Tower, Plot no. 1127 2nd Floor**
**Chole road-Msasani Peninsular**
**P.O Box 105181,**
**Dar Es Salaam, Tanzania**

E : infotanzania@farmafrica.org
W : www.farmafrica.org
T : 255 222 927 802

215307602

# Shahidi adai alikimbia mihemko ya Chadema

**INATOKA UK. 3**

alidai.

"Wanachama walipata hamasa na mihemko iliyosababisha wapate jazba ya kuichukia serikali na vyombo vya ulinzi na usalama. Wananchi waliokuwa wamekaa walinyanyuka na kuhamasika, mimi na waandishi wenzangu tulitawanyika pale tuposimama karibu na jukwaa, nilikimbilia kwenye gari la polisi kunusuru kamera," alidai Koplo Charles.

Aliendelea kudai kuwa alifika ofisini salama na alikwenda kumpa taarifa Mkuu wa Upelelezi wa Makosa ya Jinai wa Mkoa (RCO) na akamwagiza kutunza picha za video alizopata kwenye mkutano huo kwa kuwa atatumia kama kielelezo na kwamba tayari bosi wake huyo alishafungua kesi dhidi ya vigogo wa Chadema.

Jopo la utetezi liliongozwa na Wakili Profesa Abdallah Safari, Peter Kibatala, John Mallya na Hekima Mwasipu.

Mbali na Mbowe, washtakiwa wengine ni Mbunge wa Bunda, Ester Bulaya; Mbunge wa Tarime Mjini, Esther Matiko; Katibu Mkuu wa Chadema, Vicent Mashinji; Mbunge wa Iringa Mjini, Peter Msigwa, Naibu Katibu Mkuu Zanzibar, Salum Mwalimu, Mbunge wa Kibamba, John Mnyika; Mbunge wa Kawe, Halima Mdee na Mbunge wa Tarime Vijijini, John Heche.

Katika kesi ya msingi, washtakiwa hao wanadaiwa kuwa kati ya Februari Mosi na Februari 16, mwaka huu Mbowe na wenzake wakiwa Kinondoni, Dar es Salaam kwa pamoja walikula njama na wengine ambao hawapo mahakamani ya kutenda kosa la jinai ikiwamo kuendelea na mkusanyiko isivyo halali na kusababisha chuki na uchochezi wa uasi. Ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana, Bulaya alishawishi kutenda kosa la jinai katika viwanja vya Buibui vilivyoko Kinondoni, Dar es Salaam kwa kuwataka wakazi wa eneo hilo kufanya maandamano yenye vurugu.

Pia ilidaiwa kuwa Februari 16, mwaka jana katika barabara ya Kawawa eneo la Kinondoni Mkwajuni kwa pamoja washtakiwa na wenzao zaidi ya 12, walifanya mkusanyiko na kukaidi amri halali ya ofisa wa Jeshi la Polisi Gerald Ngiichi na kusababisha kifo cha Akwilina Akwiline na askari polisi wawili Konstebo Fikiri na Koplo Rahim Msangi kujeruhiwa.

Ilidaiwa siku ya tukio la kwanza na la pili, katika viwanja vya Buibui, kwenye mkutano wa hadhara, Heche alitoa lugha ya kuchochea chuki alitamka matamshi kwamba: "Kesho patachimbika upumbavu ambao unafanywa kwenye nchi hii...wizi unaofanywa na serikali ya awamu ya tano... watu wanapotea... watu wanauawa wanaokotwa kwenye mitaro lazima ukome...", ambayo yanadaiwa yalielekea kuleta chuki kati ya serikali na Watanzania. Washtakiwa wote waliposomewa mashtaka yao kwa nyakati tofauti walikana.

# CAG Assad ataja dawa kumaliza rushwa

**INATOKA UK. 2**

kila mwananchi awe na access ya kuona," alisema Prof. Assad na kuongeza:

"Kila mtu aone kwamba katika mradi fulani fedha iliyotumika ni kiasi fulani, na naamini tukifikia hatua hiyo, hakuna mtu atakayechukua rushwa, lakini tukiendelea na utaratibu wa kwamba watu wachache tu na wengine hawapati, tatizo la rushwa litaendelea.

"Nasema hivyo kwa sababu siku moja nilipata shida moja, niliandika barua kupeleka ubalozini na nilifikiri ni siri, lakini cha ajabu Balozi aliniambia kwa mujibu wa sheria za nchi yao, kila kitu kinachofanyika katika nchi yao lazima mwananchi akione na kama itabidi kumficha ni lazima muende mahakamani kueleza sababu za kuficha." "Sasa na sisi tukifika hapo nchi itakwenda kwa sababu kila mtu atakuwa anaona kila kitu kinachofanyika kwa sababu kila mtu atakuwa amepewa uwezo huo na kila mtu atakuwa anaogopa kuchukua au kutoa rushwa."

Pia Prof. Assad alisema suala la kupambana na rushwa siyo tu katika sekta binafsi tu bali hata katika sekta ya umma.

Pia alisema taasisi za serikali zinapaswa kutii sheria katika kusaidia kudhibiti vitendo vya rushwa badala ya kufanya mambo kwa ujanjaujanja.

**KAULI YA MKUCHIKA**

Kwa upande wake, serikali imesema utafiti mbalimbali unaonyesha kuwa Tanzania imeanza kufanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa na utawala bora.

Utafiti huo umefanywa na taasisi za ndani na nje, na umeonyesha kuwa Tanzania imeanza kufanya vizuri katika mapambano dhidi ya rushwa, huku ikiimarisha utawala bora.

Kauli hiyo ilitolewa na Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais (Utumishi wa Umma na Utawala Bora), Mkuchika, wakati wa kongamano hilo.

Alisema serikali inatumia nguvu kubwa kupambana na rushwa ili kuiletea maendeleo nchi na kutekeleza Ilani ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

"Mipango yote ya serikali ya kuifikisha nchi katika uchumi wa kati kupitia sekta ya viwanda ya hauwezi kufikiwa pasipo na mapambano dhidi ya rushwa, ndiyo maana tumekuwa wakali sana, ili kuwe na mapambano ya rushwa, lazima kuwapo na utashi wa kisiasa," alisema Mkuchika.

Alisema matokeo ya mapambano hayo ni kuongezeka kwa wigo wa upatikanaji wa huduma kwa Watanzania ikiwamo elimu bure.

**MKURUGENZI TANTRADE**

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Tantrade, Edwin Rutageruka, alisema rushwa imekuwa kikwazo kikubwa kwa uwekezaji kwa kuwa wengi wanakata tamaa na kuondoka kutokana na kushindwa kuhimili milolongo.

Alisema wawekezaji wengi wanahofia kupoteza muda mwingi wa ufuatiliaji, matumizi makubwa ya rasilimali fedha hatimaye kumaliza mitaji.

Alisema milolongo ya ruhwa kwa wawekezaji ndiyo sababu ya wananchi kukosa huduma ya bidhaa bora na kusababisha uingizwaji wa bidhaa kwa njia zisizo rasmi.

**DK. BASHIRU ALLY**

Katibu Mkuu wa CCM, Dk. Bashiru Ally, alisema Ilani ya CCM iliweka lengo la kukabili mambo manne ikiwamo ajira, umaskini, rushwa na ufisadi pamoja na usalama na amani ya nchi, ndiyo maana kumekuwa na upungufu wa matukio ya rushwa nchini. Alitaja sehemu ambazo zimeghubikwa na rushwa zaidi ni vyama vya ushirika, migogoro ya mirathi na ndoa, migogoro kazini, migogoro ya ardhi, kodi na usalama barabarani sambamba na shughuli za uchaguzi.

# Mtoto adai alimwona baba wa kambo akimuua mamaye

**INATOKA UK. 3**

aliieleza mahakama kuwa mama yake alifariki dunia Juni 21, 2014 na kwamba Juni 20 alipotoka kucheza alikuta baba yake (mshtakiwa), mama yake na watu wengine wakiwa wamekaa katika mkeka nyumbani kwao Ulongoni.

Alidai kuwa dada yake anayeitwa Hadija Shabani, alimwambia kuwa kulikuwa na ugomvi kati ya baba na mama yake ambao ulisuluhishwa na kwisha na baadaye alimshuhudia mshtakiwa akimpa fedha mama yake akanunue mboga kwa ajili ya chakula cha usiku.

Alidai kuwa majira ya saa 5:00 usiku, alikwenda kuwalaza wadogo zake, Hassan na Rahim, chumbani kwa mama yao na kisha akaenda kulala chumbani kwake pamoja na mtoto wa mama yake mdogo.

"Usiku nilishtuka nikasikia mama na Godfrey wanagombana. Mtoto wa mama mdogo alikuwa anaogopa, nikamwambia yataisha sisi tulale, tukabaki macho kitandani. Mtoto wa mama mdogo akabanwa na haja ndogo, hivyo tukatoka nje kujisaidia," alidai Khadija.

Alidai kuwa walipotoka nje walimwona Godfrey akiwa amekaa katika kochi sebuleni akiwa amevaa kipensi, shati begani huku akitokwa na jasho na kuwahoji wanakokwenda.

"Sisi tulimjibu tunaenda kujisaidia, akasema haya. Tuliporudi tukasikia Godfrey akifunga mlango wa sebuleni na kutoka nje, sisi tulijificha nyuma ya mlango wa sebuleni, tulimsikia Godfrey akimgongea mpangaji wa chumba cha nje na kumuuliza kama alisikia kelele, yule mpangaji akamwambia hakusikia kelele," alidai shahidi.

Shahidi huyo alidai, baadaye walienda kulala, asubuhi aliamshwa na mama mwenye nyumba ambaye alimtaka achukuwe beseni la vyombo apeleke chumbani kwa mama yake. Huku akitokwa na machozi, shahidi huyo alidai aligonga mlango lakini mama yake hakuitikia na alipoingia ndani alimkuta mama yake amelala akiwa amefunikwa shuka jeupe na kanga kichwani, alimtikisa hakuamka na kutoka nje huku akipiga kelele.

"Nilikuta mama kalala, niliendelea kumwamsha bila mafanikio, nikamfunua alikuwa hajavaa nguo, nikamshika kifua kuona kama roho yake inadunda, ilikuwa haidundi, nikatoka nje nikipiga kelele. Mama mwenye nyumba aliniuliza nikamwambia mama yangu hahemi amefunikwa nguo, majirani walikuja na kumwangalia, wakasema atakuwa amezimia, wakamvalisha nguo na kumpeleka hospitalini," alidai. Khadija alidai kuwa watu waliorudi kutoka hospitalini walimwambia kuwa mama yake amekufa na alinyongwa. Alidai kuwa mama yake alinyongwa na Godfrey kwa sababu alishawahi kumtamkia kuwa atamuua yeye na familia yake kwa kuwa hataki kuiona.

"Mama pia alishawahi kunambia kwamba, 'mwanangu nikifa Godfrey ndiye kaniua,'" alidai.

Naye shahidi Khadija Shabani, ambaye alikuwa akimwita marehemu shangazi, aliieleza mahakama kwamba wawili hao walikuwa na ugomvi na kwamba Godfrey alikuwa akimtuhumu Bahati kuwa na uhusiano wa kimapenzi na jirani yao.

# Kenyatta kuja nchini kesho

**Na Mwandishi Wetu**

RAIS wa Kenya Uhuru Kenyatta, kesho atafanya ziara binafsi ya siku mbili nchini kwa mwaliko wa Rais John Magufuli.

Kwa mujibu wa taarifa ya Kurugenzi ya Mawasiliano ya Rais Ikulu jana, Rais Kenyatta atatua katika Uwanja wa Ndege wa Chato mkoani Geita asubuhi kisha kuelekea nyumbani kwa Rais Magufuli katika Kijiji cha Mlimani wilayani Chato.

Akiwa Chato, Rais Kenyatta atafanya mazungumzo na mwenyeji wake, Rais Magufuli.

# Serikali yashauriwa

**INATOKA UK. 5**

itarahisisha Serikali kujipanga na kuwahudumia bila kubahatisha.

Kamishna Marijani alisema kwa mujibu wa takwimu zilizopo Tanzania ina wakimbizi zaidi ya 300,000 huku kila wiki wakirejesha wakimbizi zaidi ya 2,000 makwao kwa hiari.

"Serikali inahitaji ushirikiano na wadau mbalimbali katika kukabiliana na wakimbizi hivyo niwapongeze Dignity Kwanza kwa uamuzi wao wakukutanisha kujadili njia sahihi ya kuwepo kwa nyaraka kwa kundi hilo," alisema. Akizungumzia semina hiyo Mwanasheria wa Dignity Kwanza, Jovin Sanga alisema wamekutanisha wadau mbalimbali wa sekta binafsi na Serikali kujadiliana namna sahihi ya kuwahudumia wakimbizi na waomba hifadhi.

Alisema semina hiyo itaweka mipango na namna ya kukabiliana na changamoto zinazowakumba wakimbizi na waomba hifadhi.

Sanga alisema wakimbizi wanakabiliwa na changamoto mbalimbali zikiwamo kutotambuliwa kwa taaluma na vipaji vyao hivyo semina hiyo inaweza kuwa chachu ya kujua njia za kukabiliana nazo.

"Tumeamua kukutanisha wadau mbalimbali wakiwemo Serikaki sababu kubwa ni kuangalia namna ya kuwafanya wakimbizi wajione ni watu kama wazawa kwa kuonesha vipawa vyao na ujuzi," alisema.

Mwanasheria huyo alisema wapo watu wengi wanaingia nchini katika mazingira ambayo sio ya kikimbizi hivyo wanahitajika kujulikana walipo ili waweze kupata msaada stahiki.

# Hasunga ataka kilimo

**INATOKA UK. 4**

kuwa bila utafiti hakuna kilimo na lazima ijulikane kilimo gani kitumike, pembejeo gani zitumike, pia tuongeze uzalishaji wenye tija," aliongeza.

Hasunga pia alibainisha kuwa serikali inakuja na mkakati wa bima kwa wakulima lengo likiwa ni kumsaidia mkulima pindi mazao yake yatakuwa yanapoharibika shambani.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji, Mahmoud Mgimwa, alisema kama serikali itawekeza katika kilimo hifadhi, sekta ya kilimo itafika mbali.

Mgimwa ambaye ni Mbunge wa Mufindi Kaskazini (CCM) aliiomba serikali kuongeza bajeti katika sekta ya kilimo hasa katika utafiti.

Alisema matatizo yanayowakabili wakulima ni pamoja na masoko na miundombinu hivyo kuitaka serikali kuangalia sera na sheria zilizopo kwa kuwa nyingi zimetungwa wakati wa ukoloni.

HABARI KITAIFA

# Wauzaji ramani kiholela washukiwa

**Na Grace Semfuko,** MAELEZO

BODI ya Usajili wa Wabunifu Majengo na Wakadiriaji Majenzi (AQRB), imewataka wafanyabiashara wa ramani za majengo nchini kuacha kuuza ramani hizo mara moja kwani zimekuwa ni chanzo kikubwa cha ujenzi holela usiozingatia viwango vya ubora.

Bodi hiyo imesema kumekuwa na matatizo ya kuporomoka kwa majengo, nyumba kuwa na nyufa pamoja na ujenzi unaoziba miundombinu mingine.

Kwamba hali inayotokana na wenye nyumba wengi kutofuata sheria za ujenzi pamoja na viwango vya ubora.

Mwenyekiti wa Bodi hiyo, Dk. Ludigija Bulamile, alisema watu wanaouza ramani hawaangalii wala kupima viwango vya ujenzi unaotakiwa mahali husika maana wataalamu wa masuala hayo kabla ya kukushauri aina ya jengo linalohitajika kutokana na hali ya udongo.

"Wauza ramani wote wa nchini muache mara moja kuuza ramani hizo, hamna utaalamu wa kumshauri mtu kuhusiana na jengo linalohusika, mnauza ramani ovyo watu nao wananunua tu, hii inasababisha nyumba nyingi kupata ufa na kubomoka hii inahatarisha maisha ya watu," alisema Dk. Lidigija.

Alisema kuna maeneo hayaruhusiwi kujenga nyumba za ghorofa au nyumba kubwa kutokana na ardhi iliyopo, na wakati mwingine ardhi inakuwa na maji, hivyo kuhitaji msingi mkubwa na mchanganyiko wa zege imara. Lakini watu wananunua na kujenga kwenye maeneo hayo bila kuzingatia athari zinazoweza kutokea.

"Nawashauri wakati wa kujenga mtumie wataalamu waliosomea fani ya ubunifu na ukadiriaji majenzi ili kuepukana na hasara ya kujenga nyumba mara mbili, unajua usipotumia wataalamu hawa eti unasema unaokoa gharama matokeo yake unajikuta unatumia gharama mara mbili zaidi kwani yanabomoka, au wanapindisha nyumba, hawazingatii viwango na mchangayiko mzuri wa nyenzo za ujenzi," alisema.

Makamu Mwenyekiti wa Bodi hiyo Dk. Geraldine Kikwasi, alisema wakadiriaji majenzi wamekuwa na mchango mkubwa wa kuhakikisha majengo yanakuwa imara na hivyo kuwaomba Watanzania kuwatumia ili kuimarisha sekta hiyo.

"Wakadiriaji majenzi ni watu muhimu sana, ni muhimu kuwatumia, nashauri halmashauri zote kuajiri watu hawa ili kupangilia miji yetu na majengo kwa ujumla," alisema Dk. Kikwasi.

Naye mbunifu majengo ambaye pia ni Mjumbe wa Bodi hiyo, Mbaraka Igangula, alisema utafiti uliofanywa na bodi hiyo hivi karibuni umebaini kuwapo kwa zaidi ya asilimia 90 ya makazi jijini Dar es Salaam kutokuwa na ubora kutokana na kutotumia wataalamu wa ujenzi katika kujenga makazi yao.

Alisema kuanzia sasa watahakikisha majengo makubwa yote nchini yanajengwa kwa kufuata sheria za ujenzi ikiwamo kutumia wataalamu wa ubunifu majengo na ukadiriaji majenzi ili kujenga majengo imara.

Albert Munuo ni Kaimu Msajili wa AQRB, alisema wataalamu hao hivi sasa ni wachache nchini, hivyo kuwaomba wanafunzi wengi zaidi kusomea fani hiyo ili kuongeza wataalamu katika sekta hiyo.




Wajasiriamali wanaojishughulisha na ususi 'wakiuchapa' usingizi wakati wakisubiri wateja katika eneo la Ilala Boma, jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JOHN BADI**

# RC aiagiza h'shauri kuzijibu hoja za CAG bila ubabaishaji

**Na Happy Severine,** MEATU

MKUU wa Mkoa wa Simiyu, Anthony Mtaka, ameitaka Halmashauri ya Wilaya ya Meatu kujibu hoja za ukaguzi zilizoibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), kuhakikisha wanazijibu kwa wakati.

Aidha, wametakiwa kutozijibu kwa ubabaishaji, huku akiwataka kutoa ushirikiano kwa mkaguzi wa ndani.

Kadhalika, Mtaka alisema miaka ya nyuma halmashauri hiyo ilikuwa ikipata hati chafu kutokana na baadhi ya watumishi wake kutofanya kazi ipasavyo, hivyo aliwataka wakuu wa idara kutoa ushirikiano kwa mkaguzi wa ndani ambaye ndiye jicho la halmashauri.

Aliyasema hayo jana wakati akizungumza kwenye kikao cha Baraza Maalumu la Madiwani kilichokuwa kikijadili ajenda moja ya hoja 21 za ukaguzi zilizoibuliwa na CAG. Mtaka pia amemtaka mkaguzi wa ndani wa halmashauri hiyo kuwa jicho ili aisaidie halmashauri wakati wakitekeleza miradi mbalimbali, huku akisisitiza hoja zijibiwe kwa wakati bila ubabaishaji zikienda sambamba na viambatanisho vya vielelezo vinavyojitosheleza.

"Hakuna sababu ya kutumia siku nyingi mpaka kufikia hatua ya kukumbushwa,... mkaguzi kama utahitaji ufafanuzi kwa ngazi ya mkoa njoo utupe taarifa tukusaidie," alisema Mtaka.

Pia aliitaka halmashauri kuiheshimu taarifa ya mkaguzi na mapendekezo yaliyotolewa yatekelezwe na kufanyiwa kazi.

Naye Fabian Manoza, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri hiyo, aliahidi kuyafanyia kazi maelekezo yaliyotolewa na Mtaka, na kuhakikisha wanatoa ushirikiano wa kutosha kwa mkaguzi wa ndani.

Mwenyekiti wa Halmashauri, Pius Machungwa, alisema kwa mwaka 2016/2017, CAG aliibua hoja za ukaguzi 91, na kuwa walipata hati ya shaka, hivyo kwa mwaka huu wametekeleza baadhi ya mapendekezo ili wapate hati safi.

Alisema kwa mwaka (2017/18) mkaguzi aliibua hoja za ukaguzi 24 na kuifanya halmashauri hiyo kupata hati safi, huku akiahidi kusimamia miradi ili waendelee kupata hati safi na pia kumtumia mkaguzi wa ndani katika usimamizi wa miradi.

Manoza alisema hoja nyingi zilitokana na mambo ya ndani ambayo watendaji walitakiwa kuyadhibiti hasa yatokanayo na ukusanyaji wa mapato ambapo wameanza kukusanya mapato kwa mfumo wa kielektroniki (EFD).

Manoza alisema watamtumia mkaguzi wa ndani wanapotekeleza miradi ili endapo akibaini kuna upungufu aweze kuwajulisha na wayafanyie kazi.

# DC afunda watumishi wa forodha

**Na Zanura Mollel,** LONGIDO

SIKU chache baada ya Mkuu wa Wilaya ya Longido mkoani Arusha, Frank Mwaisumbe, kwa kushirikiana na Jeshi la Polisi mpakani Namanga kukamata madini zaidi ya kilo 36 ya aina tofauti yaliyokuwa yakitoroshwa kuelekea Kenya, ametoa wito kwa wafanyakazi wa kituo kimoja cha forodha upande wa Tanzania (OSBP) kufanya kazi kwa kushirikiana.

"Kikao hiki ni cha kutathmini kazi zinazofanyika katika kituo hiki cha pamoja na kupanga mikakati mipya ya mwaka wa fedha na kuhakikisha changamoto zilizopo zinatatuliwa ipasavyo," alisema Mwaisumbe.

Mwaisumbe alisema, kituo hicho kinafanya kazi kwa saa 24 kutoa huduma kwa wageni wanaoingia nchini na wanaokwenda nje ya nchi pamoja na huduma kwa wafanyabiashara wanaopita katika mpaka wa Namanga.

"Hapa kuna idara 14 na idara zote zinafanya kazi kwa kushirikiana... hii yote ni kurahisisha shughuli za watu wanaotumia mpaka huu," alisema Mwaisumbe.

Alisema kuna changamoto kwa baadhi ya idara zina upungufu wa watumishi na vifaa, atashirikiana na wizara zenye dhamana pamoja na ngazi ya mkoa kuhakikisha changamoto hizo zinatatuliwa ili kurahisisha shughuli katika mpaka huo.

"Serikali inafanyakazi kubwa sana, na hata sasa kuna idara zimepata vifaa ikiwamo idara ya mionzi, mmeletewa kifaa hapa, usumbufu wa kwenda Dar_es_Salaam kupeleka bidhaa sasa hakuna hayo mengine tutayatatua... msiogope fanyeni kazi kwa bidii," alisema Mwaisumbe.

Hata hivyo alipongeza Mamlaka ya ya Mapato (TRA) chini ya ofisa mfawidhi katika kituo hicho, Paul Kamukuru, kwa makusanyo ya kuridhisha yaliyovuka lengo kwa mwaka wa fedha uliomalizika 2018/2019 na kuwataka kuhakikisha kasi ya ukusanyaji wa mapato inaongezeka.

## Abuni mtambo kufua umeme

**Na Elizabeth Zaya**

MKAZI wa Sumbawanga mkoani Rukwa, George Ulaya, amebuni mtambo wa kufua umeme unaotumia upepo wenye kilovoti 50,000, ambao utatumika kuendesha viwanda na matumizi ya nyumbani.

Ulaya akiwa chini ya Tume ya Taifa ya Sayansi na Teknolojia (COSTECH) aliweza kuelezea jinsi alivyoanza ubunifu huo akiwa Sumbawanga na sasa anasambaza teknolojia hiyo katika mikoa mbalimbali nchini.

Akiwa katika Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa Sabasaba banda la COSTECH alisema alianza na kutengeneza mashine ya kufua umeme kwa njia ya upepo wa kilovoti 300, lakini baada ya kuwezeshwa na COSTECH anatengeneza pia mashine ya kisasa inayotoa umeme wa kilovoti 50,000.

Alisema umeme wake unatumiwa na idadi kubwa ya watu na kwamba hata umeme wa gridi ya taifa ukikatika mashine yake ina uwezo wa kutunza nguvu ya umeme kwa muda mrefu.

"Nawashukuru COSTECH baada ya mwaka 2010 kunipa tuzo ya ubunifu huu na kunisaidia sasa nimepaa nipo kiteknolojia zaidi kwa maana natumia nyenzo mbalimbali za kisasa na nimekuwa mbunifu mkubwa wa kutengeneza mashine mbalimbali," alisema Ulaya.

Alisema mashine hiyo ina uwezo wa kutumika hata viwandani mbali na matumizi ya majumbani na inaweza kutumiwa na takribani na watu 400 kwa wakati mmoja.

# TIRDO yabuni mtambo maalumu kudhibiti sumukuvu kwenye mazao

SHIRIKA la Maendeleo ya Viwanda (TIRDO), katika kuhakikisha mazao mbalimbali nchini yanakaushwa kwa kiwango kinachokubalika kitaalamu ili kuepuka magonjwa, limebuni mtambo maalum wa kuondoa sumukuvu.

Akizungumza na Nipashe katika Maonyesho ya Biashara ya Kimataifa ya Sabasaba, Mtafiti wa TIRDO, Ester Lazaro, alisema mtambo huo ambao unatumika sambamba na biogesi utasaidia kukausha mazao hayo hasa mahindi na karanga na kuepukana na unyevunyevu.

Alisema mazao mengi yamekuwa hayakauki vizuri kwa sababu ya hali ya hewa jambo ambalo lina athari kiafya.

"Ili kuondoa tatizo hili tumeona ni vyema tukapanga mikakati na kuunda mfumo ambao ni rafiki unaotumia masalia ya mimea kukaushia mazao," alisema Ester.

Ester alisema kadri siku zinavyokwenda, mtambo huo wa kijani kibichi umejizolea wateja wengi kwani wanaamini utasaidia kuondoa changamoto ya ukaushaji mazao kwa wakati.

Alisema wanaendelea kutengeneza mtambo huo ili uwe mkubwa ambao utakidhi mahitaji ya wananchi wengi hapa nchini.

Pia alisema wamegundua dawa nyingine inayojulikana kama Leather Processing Enzemy yenye uwezo wa kuondoa manyoya kwenye ngozi ya mnyama bila kumwathiri. Alisema dawa hiyo imetengenezwa kwa vitu vya asili na haina madhara isipokuwa inaua pia viluilui vya malaria.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan, akikabidhi kikombe cha ushindi wa jumla katika uunganishaji wa magari na uuzaji wa mitambo, kwa Mkurugenzi wa Kampuni ya GF Trucks, Ali Jawad Karmali, wakati wa ufunguzi wa Maonyesho ya 43 ya Biashara ya Kimataifa ya Dar es Salaam juzi. **PICHA: MIRAJI MSALA**

## Wito kuwezesha vijana teknolojia

JAMII imetakiwa kuwawezesha vijana kwa kuwajengea uelewa kuhusu teknolojia mbalimbali ili kupata wataalamu wanaokidhi soko la uchumi wa kati kupitia viwanda.

Akizungumzia na Nipashe, Mratibu wa Mafunzo ya Ujenzi wa Kituo cha Intergrated Mining Technical Training Project (IMTT), Theresia Mosha, alisema, chuo hicho kimekuwa kikitua mafunzo mbalimbali kwa vijana kwa sababu ya mahusiano mazuri waliyojiwekea baina yao, kampuni za madini na chakula. Alisema kwa sababu ya mahusiano hayo, kampuni zaidi ya 12 huwawezesha wafanyakazi wao kwa kuwagharamia mafunzo ili kuwajengea uwezo zaidi.

"Kituo chetu kila mwaka huchaguliwa kuwa kituo cha Mafunzo IMTT Tanzania kwa sababu kimejijengea mazingira bora ya miundombinu ya chuo pamoja na ufundishaji," alisema Theresia.

Alitaja kozi wanazofundishwa kuwa ni pamoja na utengenezaji mfumo wa magari, umeme wa viwandani, ufundi wa magari pamoja na uchongaji vifaa vya magari.

Alisema kwa mwaka huu wamekuja na teknolojia mpya ya umeme wa magari ya dizeli ambayo imekuwa kivutio kwa watu wengi.

Aidha, alisema malengo yao makuu ni kuhakikisha jamii kubwa ya vijana wa Kitanzania wanapata elimu ya ufundi ambayo itachagiza kuibuliwa kwa viwanda vingi hapa nchini na hatimaye kufikia uchumi wa kati.

# Posta yaanzisha duka jipya la biashara kwa mtandao

KATIKA kuendana na soko la ushindani, Shirika la Posta Tanzania, limeanzisha duka jipya la biashara za kimtandao maarufu kama 'Posta Shop Tz'.

Akizungumza katika Viwanja vya Maonesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam (DITF) yanayofanyika katika Viwanja vya Mwalimu Julius Nyerere, Meneja wa Biashara za Kielektroniki (E-commerce), Amina Salum, alisema ni duka ambalo linauwezo wa kuuza, kununua na kutangaza biashara kwa wateja ambao wamejisajili.

"Mjasiriamali yeyote anaweza kujiunga kupitia website yetu au kuingia kwenye website ya shirika," alisema Salum.

Alisema wameamua kuanzisha mfumo huo kwa sababu biashara za kimtandao kwa sasa ndio zinatumika kwa kiwango kikubwa.

"Vijana wengi sasa hivi wananunua bidhaa online, kwa kuwa shirika linafanya biashara na linaaminika zaidi hivyo tukaona na sisi tuje na duka hili, ambapo mtu yeyote anaweza kujiunga nasi bure na lengo ni kutoa fursa kwa idadi kubwa ya watu kufanya biashara," alisema.

Aliongeza kuwa katika maonyesho ya mwaka huu mwamko umekuwa mkubwa kwa Watanzania kutembelea banda lao na kutaka kujifunza mambo mbalimbali ya shirika hilo.

Alisema kuwa shirika hilo limejipanga kiushindani kama ilivyo kwa kampuni nyingine na kwamba wanafanya kazi na kampuni zote za simu nchini kwa sasa katika kurahisisha kufanyika kwa miamala ya kifedha kwa ajili ya biashara.

**HABARI ZOTE NA ELIZBETH ZAYA**

HABARI ARUSHA

# Wadau waomba kutowekwa VAT kwenye taulo za kike

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WADAU mkoani Arusha wameiomba serikali kutoweka kodi ya ongezeko (VAT) kwenye taulo za kike kwani zitasababisha kuongezeka kwa gharama na kupelekea baadhi yao kushindwa kumudu gharama.

Hayo yalisemwa jana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Jivita inayofanya kazi na vijana walioko shuleni na wasiokuwa shuleni katika kutatua changamoto zinazowakabili hususani suala zima la ajira, Raymond Mashambo, wakati akizungumza katika hafla fupi ya kukabidhi taulo hizo kwa wanafunzi wanaosoma katika Shule ya Sekondari Elizabeth iliyopo eneo la Kia.

Alisema kitendo cha kuwekwa kodi hiyo kwenye taulo hizo kutachangia wanafunzi wengi kutomudu gharama hasa wanaotoka katika mazingira magumu kutokana na kiwango hicho kuwa juu kulingana na kilichokuwapo kabla ya kodi ya ongezeko hilo ya VAT.

Raymond alisema wamekuwa wakitekeleza programu ya kusambaza taulo hizo kwa wanafunzi wanaotoka katika mazingira magumu waliopo kwenye shule za serikali ambapo, na kuwa walifikia hatua hiyo baada ya kuona uhitaji mkubwa katika shule nyingi.

"Programu hii ya utoaji wa taulo hizi za kike ipo chini ya mradi wa Mwanao, ambapo hadi sasa hivi tumeshatoa taulo hizo katika wilaya za Longido, Monduli, Karatu, Arusha Mjini na Arumeru katika shule za sekondari mkoani Arusha ambapo tumelenga kufikia halmashauri zote hasa tukilenga wasichana wanaotokea kwenye mazingira magumu," alisema.

Aliongeza mwaka jana ongezeko la VAT lilitolewa, hivyo kusaidia kupunguza gharama na taulo hizo kuuzwa kwa Sh.750 hadi Sh.1,000 kwa bei ya jumla, hivyo kuwasaidia kununua na kuwapelekea watoto, na kuwa hivyo kama kiwango cha VAT kitawekwa tena, kuna uwezekano mkubwa ikauzwa Sh.1,500 hadi Sh. 2,000, na hivyo itakuwa vigumu wao kuzipata.

Naye Mwalimu Mkuu wa Shule ya Elizabeth, Sister Bernadetha Kessy, aliiomba serikali kutoweka VAT kwa sababu itawawia vigumu watoto kumudu gharama hasa wanaotoka katika mazingira magumu ambao wamekuwa wakiwezeshwa na shule hiyo.

Aliiomba serikali kusikiliza kilio chao kwa kuwa kitendo cha kuwekwa VAT kwenye taulo hizo kutachangia watoto kujiingiza kwenye vishawishi ili waweze kupata fedha ya kununua kutokana na watoto wengi familia zao kutokuwa na uwezo.

Nao baadhi ya wanafunzi hao waliokabithiwa taulo hizo, Victoria Simba na Neema John, walishukuru na kusema walikuwa wakikabiliwa na changamoto ya ukosefu wa taulo hizo, na kwamba wakati mwingine husaidiwa na uongozi wa shule kutokana na mazingira wanayotoka.



Mbunge wa Arusha Mjini, Godbless Lema, akihutubia mkutano wa hadhara wa wananchi wa Jimbo la Arusha Mjini jana, akiwaelezea kuhusu kazi za maendeleo alizozifanya katika jimbo lake, kwa mwaka fedha wa bajeti ya 2018/ 2019. **PICHA: ALLAN ISACK**

# W'biashara walalamikia Jiji kuwafungia maduka, vizimba

**Na Allan Isack,** ARUSHA

WAFANYABIASHARA wa Soko Kuu jijini hapa, wamelalamikia uamuzi wa Halmashauri ya Jiji kufunga baadhi ya maduka na vizimba kadhaa vya biashara, kwa walichodai kuwa wameshindwa kulipa ushuru na kusababisha halmashauri kukosa mapato.

Wakizungumza na Nipashe, kwa niaba ya wenzao, Venderine Alphonce, Juma Maico na Farida Mshana, walimlalamikia mkuu wa soko hilo, Magige Makuri, kwa kuchukua hatua hiyo, inayokinzana na maelekezo ya Rais John Magufuli ya kutaka wafanyabiashara wasifungiwe biashara zao kwa kushindwa kulipa kodi.

"Ni kweli tunadaiwa na hatujakataa kulipa, lakini hatua ya kufunga biashara zetu tutawezaje kulipa, tunachoomba watufungulie biashara zetu ili tuendelee kuuza na kulipa madeni tunayodaiwa," alisema Farida.

Walidai mkuu wa soko amekuwa akiwanyanyasa wafanyabiashara na hataki kuwasikiliza na amekuwa akitumia nguvu kuwafungia vizimba.

Ofisa Biashara wa Halmashauri hiyo, Godfrey Edward, alisema halmashauri hiyo, haina ugomvi na wafanyabiashara, hivyo aliwataka wenye malalamiko kuyawasilisha kwa Mkurugenzi wa Jiji.

Alisema Mkurugenzi yupo tayari kukaa meza moja na wafanyabiashara hao kwa lengo la kufikia makubaliano yatakayowawezesha kulipa madeni yao.

Hata hivyo, alisema hana taarifa ya kufungwa kwa vizimba, lakini alisema taarifa hiyo itafanyiwa kazi kwa ajili ya kubaini ukweli wa jambo hilo.

Alisema wafanyabiashara wameeleza kuwa madeni wanayodaiwa yametokana na hali ngumu ya biashara pamoja na kupungua wateja, hivyo wamekuwa wakishindwa kufanya biashara kama ilivyokuwa vipindi vilivyopita.

Pia walimweleza kuwa sababu nyingine iliyowafanya kushindwa kulipa kodi kwa wakati imetokana na mkuu wa soko kushindwa kuwasilisha kwa wakati fedha walizokuwa wanadaiwa na halmashauri.

Wafanyabiashara hao wanadaiwa malimbikizo mengi ya kodi ya vizimba na kila mwezi wanatakiwa kulipa Sh. 30,000, lakini baadhi wamejikuta wakilimbikiza na kufikia Sh. 800,000, hivyo halmashauri kuamua kufunga biashara zao.

# Lema atamani kumshauri JPM

**Na Allan Isack,** ARUSHA

MBUNGE wa Arusha Mjini (Chadema), Godbless Lema, amesema akipata nafasi ya kumshauri Rais John Magufuli, atamweleza namna viongozi walivyoshindwa kumsaidia kutokana kuwa na hofu.

Akizungumza katika mkutano wa hadhara kwenye viwanja vya Soko Kuu la Arusha, Lema, alisema akipata nafasi hiyo, atamweleza Rais namna viongozi aliyowateua wanavyofanya maamuzi bila ya kufuata katiba na sheria za nchi, kutokana na hofu ya kulinda nafasi zao serikalini.

"Tusiwe na hofu katika mapambano ya haki na haki haijawahi kushindwa na anayefahamu kesho itakuwaje ni Mungu pekee," alisema Lema.

Alisema hofu inapoingia au kupandikizwa kwa watu inawaondolea hekima, kutokuwa na ubunifu, kutokuwa na fikra chanya na vitu hivyo vikikosekana taifa haliwezi kupiga hatua kimaendeleo.

"Mtu mwenye hofu hawezi kuwa mgunduzi na anaweza kukimbia hata kivuli chake mwenyewe... na hofu hii iliyowaingia watu inaweza kuvunja mahusiano na pia inaweza kuligawa taifa," alisema Lema.

Hata hivyo, Lema alidai kuwa kuhama kwa baadhi ya wabunge na madiwani wa Chadema kujiunga na Chama Cha Mapinduzi (CCM) siyo kigezo cha wao kukata tamaa ya kurudi nyuma katika harakati za kupigania demokrasia nchini.

Lema alisema amesikitishwa na kitendo cha Kamanda wa Polisi Mkoa wa Arusha, Jonathan Shana, akihamasisha kwa kupiga makofi na kuzungumza katika mkutano wa CCM uliofanyiwa mwisho wa wiki katika kituo cha Mikutano cha Kimataifa cha Arusha (AICC).

"Unapokuwa Mkuu wa Jeshi la Polisi umepewa mamlaka yote ya kuwaweka pamoja askari polisi wakubwa kwa wadogo kuwa kitu kimoja, lakini cha kusikitisha, Shana anakwenda kwenye mkutano wa kisiasa na alisema yeye na CCM ni kitu kimoja, kwa mantiki hiyo askari wadogo wataona wapinzani katika mkoa huu kama maadui," alidai Lema.

"Waacheni CCM na Chadema wapambane kwa sera na ilani, nyie polisi kaeni pembeni kulinda usalama," aliongeza.



Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akizungumza na walimu wa wilaya hiyo juzi, katika kikao kazi cha kutatua kero za kiutendaji na kimaslahi. **PICHA: JAMES LANKA**

# Ujio wa ndege ya KLM KIA wamwibua DC

**Na Godfrey Mushi,** HAI

MKUU wa Wilaya ya Hai, Lengai Ole Sabaya, amesema hatua ya Shirika la Ndege la Kimataifa la KLM kuipa heshima kubwa Tanzania, kutua kwa mara ya kwanza katika ardhi ya Kilimanjaro kwa ndege yake mpya ya Boeing 787-10 inawafunga 'midomo' viongozi waliozoea kuishi kama mafarisayo.

Ndege hiyo ambayo ni toleo jipya la ndege ya Bombadier, ilitua juzi usiku katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA) Wilaya ya Hai ikiwa na watalii 334 ikielekea Dar es Salaam na Amsterdam, Uholanzi.

"Hii ndio sehemu ya kwanza KLM kutua hapa Tanzania na ni nchi ya nne duniani inatua, na hapa Tanzania ndiko sehemu ambayo KLM inapata faida zake, huu ni ushahidi wa wazi kabisa," alisema.

Alisema kutua kwa ndege hiyo kubwa ya KLM ni ushahidi mwingine kuwa Tanzania kama nchi inazidi kupata heshima kubwa, inaonyesha na inathibitisha kwamba angalao bado nchi hii inaendelea kukubalika na kuaminika na diplomasia yake imekua kimataifa kutokana na mazingira yaliyoboreshwa kwa ajili ya utalii, miundombinu yake na usalama wa anga.

Aidha, Ole Sabaya alisema dunia nzima bado inaendelea kuiamini Tanzania kama ambavyo KLM inavyofanya wakati inakamilisha miaka 100 toka kuanzishwa kwake. Ndege hiyo ilizinduliwa wiki iliyopita na Rais wa Uholanzi katika Jiji la Amstadam.

Pia, Ole Sabaya ameonya baadhi ya viongozi hao, akisema ifike mahali iwe basi kwa maisha ya kuhukumu kila siku kwamba katika serikali hakuna jambo lolote limefanywa na watu wengine na wao wanaona na kuamini wanastahili zaidi.

Zaidi Mkuu huyo wa Wilaya amesisitiza kuwa: "Huu ni ushahidi kabisa kwamba nchi hii inaendelea kuaminika kimataifa na hii ni heshima tumepewa kama nchi na labda huo wasiwasi unaosemekana labda ni ule wasiwasi waliouzoea wa zamani ambapo wao kila siku ambapo wao kulikuwa na mashindano ya Watanzania au viongozi kupishana juu ya anga wakitumia kodi za Watanzania.

Au wasiwasi mwingine unatokana na mazingira ya wao, inawezekana labda ni hasira, walikwenda labda Dodoma wakidhani wanakwenda kununua urais na mabegi, labda huo ndio wasiwasi tunaouzungumzia.

Awali akizungumza na marubani na watalii hao, Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, alisema ujio wa ndege hiyo utafungua fursa za utalii na kutengeneza uhusiano mzuri kati ya Uholanzi na Tanzania.

"Nimezungumza nao hasa hao marubani na wamenihakikishia watakuja pia na familia zao kutembelea hifadhi zetu, huyo mmoja alishapanda Mlima Kilimanjaro lakini pia KLM wametualika kwao Oktoba 19, mwaka huu, siku ambayo wanaadhimisha miaka 100 tangu kuanzishwa shirika hilo la ndege," alisema.

# Serikali yapeleka mil. 850/- ukarabati Sekondari Ashira

**Na Godfrey Mushi,** MOSHI

WAZIRI wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), Selemani Jafo, amepeleka zaidi ya Sh. milioni 851.95 katika Shule ya Sekondari ya Wasichana ya Ashira kwa ajili ya kuanza kwa ukarabati miundombinu na mabweni yaliyoungua moto Mei 23, mwaka huu.

Taarifa iliyotolewa jana na Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Wilaya ya Moshi, Kastory Msigala, imeeleza kuwa fedha hizo zimeelekezwa kutumika kurejesha miundombinu ya shule hiyo kongwe nchini ambayo iliharibika vibaya.

"Ni kweli, Halmashauri ya Wilaya ya Moshi imepokea kiasi cha Sh. 851,955,447 kutoka Tamisemi kwa ajili ya ukarabati wa Shule kongwe ya Ashira Sekondari. Mabweni mawili ya Japan na Muungano katika shule hiyo ya kitaifa ya wasichana ambayo hayategemeani kwa nishati ya umeme yaliteketea kwa moto, huku yakiacha wanafunzi zaidi ya 224 wakipoteza vifaa vyao zikiwamo sare za shule na nguo mbalimbali.

Mabweni hayo ni miongoni mwa majengo yatakayofanyiwa ukarabati mkubwa na fedha hizo ili kuruhusu wanafunzi wa kidato cha tano kuendelea na masomo yao.

Mei 25, mwaka huu, Jafo alipozuru katika shule hiyo aliahidi kuingiza Sekondari ya Ashira fedha za ukarabati kupitia mpango wa dharura wa serikali wa ukarabati wa shule kongwe.

Kwa mujibu wa Msigala, halmashauri hiyo inaendelea na taratibu za mifumo kuruhusu kiasi hicho cha fedha kuanza kutumika na ukarabati kuanza mara moja.

"Lengo la serikali katika utaratibu huu wa ukarabati wa shule kongwe ni kuboresha mazingira ya kujifunzia na kufundishia ili kuwa rafiki kwa watumishi na wanafunzi kwa ujumla sambamba na kurudisha au kuongeza hadhi ya shule hizo," alieleza mkurugenzi huyo.

Hadi sasa, jumla ya shule mbili kongwe ndani ya Halmashauri ya Wilaya ya Moshi ambazo ni Umbwe Sekondari na Ashira Sekondari zimekwishaingia kwenye mpango huo wa serikali wa kukarabati shule kongwe na tayari zimepatiwa fedha.

Aidha, Umbwe Sekondari imepewa kiasi cha Sh. 969,669,148 kwa ajili ya ukarabati.

# Migogoro ya ardhi kikwazo cha uchumi

**Na Godfrey Mushi,** ROMBO

UKATILI wa kingono, kimwili na migogoro ya ardhi katika Kijiji cha Lesoroma, Tarafa ya Useri, Wilaya ya Rombo inadaiwa kuathiri kwa kiasi kikubwa shughuli za kiuchumi kwenye eneo hilo, huku ikiacha makovu ya athari za kisaikolojia kwa watoto na wanawake.

Ofisa Mtendaji wa Kijiji cha Lesoroma, Ema Mosha, aliyasema hayo kijijini hapo, wakati akizungumza na viongozi wa Shirika la kiraia la Kwieco na maofisa wa timu ya ufuatiliaji na tathimini ya Mfuko wa LSF waliotembelea vikundi vya ujasiriamali katika Tarafa ya Useri na Mkuu na kujionea kazi zinazofanywa na wasaidizi wa kisheria.

LSF ni mfuko wa fedha unaotoa ruzuku kwa asasi za kiraia na taasisi binafsi zinazojishughulisha na shughuli za utoaji wa msaada wa kisheria nchini.

"Tunajaribu sana kukemea hali ya ukatili unaoendelea katika jamii yetu hasa vipigo kwa wanawake, ubakaji, ulawiti, uporaji wa ardhi, mimba na ndoa za utotoni, lakini tatizo kubwa zaidi linalojitokeza ni shimo linalotokana na athari za kiuchumi pamoja na athari za kisaikolojia kuathiri idadi kubwa ya watoto na wanawake," alisema mtendaji huyo.

Mwenyekiti wa kikundi cha ujasiriamali (vicoba) cha Lesoroma, Gabriel Mahedi, alisema katika kijiji hicho wamefanikiwa kuwashawishi wanawake na wanaume wakiwamo wasaidizi wa kisheria kujiunga katika vikundi vya Umoja, Ushirikiano na Upendo ili kupunguza makali ya maisha na migogoro isiyo ya lazima inayotokana na kipato duni.

Katika ziara hiyo ya ufuatiliaji na tathmini, ofisa ufuatiliaji na mratibu wa mradi wa kusaidia wasaidizi wa kisheria wa Shirika la Kwieco, Peter Mashingia, alisema wasaidizi wa kisheria pamoja na wananchi waliojiunga na vikundi vya ujasiriamali wamekuwa chachu kubwa ya kuhamasisha jamii kukabiliana na umasikini.

Mashingia alieleza kuwa lengo la miradi hiyo ni kujenga uelewa mpana juu ya changamoto mbalimbali za kisheria zinazotokea kwenye jamii na maisha ya kila siku ya wananchi hususani wanawake.

Pia, alisema nia ya kufanya hivyo ni kujenga uelewa juu ya rasilimali (shughuli za kiuchumi) mbalimbali zinazopatikana katika eneo husika ambazo zinaweza kutumiwa na wanajamii katika upatikanaji wa haki.

Pamoja na mambo mengine, Mashingia alisema lengo jingine la kuhimiza utatuzi wa matatizo ya jamii ni kujenga uelewa wa pamoja juu ya rasilimali (watu na taasisi) mbalimbali zinazopatikana katika eneo husika ambazo zinaweza kutumiwa na wanajamii katika upatikanaji wa haki.

ama
ALHAMISI JULAI 4, 2019
AFYA NA MAZINGIRA



Ukurasa 20

**Wananchi walivyobuni mkakati wa kujijengea hospitali**



Ukurasa 17

Ndege wanatishiwa afya na sigara



Ukurasa 14

**'Meseji' zinazohamasisha mwenza ni afya ya ndoa**



## MCHANGO DAMU MANYARA

# Wanafunzi wachangia 85% kunusuru wadogo zao , kinamama wajawazito

Ukurasa 16

# 'Meseji' zinazohamasisha mwenza



LEO kila mmoja anasema jinsi ambavyo ndoa zimekuwa ndoano. Japo ni kweli lakini haimaanishi kuwa kila ndoa ni mbaya zipo nyingine ni raha tupu.

Tunasikia zaidi ubaya wa ndoa badala ya upande mwingine wenye mafanikio.

Kubwa na la msingi kwa sasa ni kuhakikisha kuwa ndoa yako inakuwa na mafanikio kwa hiyo ufanye nini?

Kwanza kuwa mpole ni vyema kila mmoja akiwa mpole, anayemheshimu, kumpenda, kumthamini na kumjali mwenza wake.

Kama ulikuwa umeanza kutoka nje ya mstari unawawaza watu wengine badala ya kujikita kwenye kuongeza mahaba kwa mwenza wako rudi haraka.

Mambo yanayoweza kuinasua ndoa isiwe ndoano ni pamoja na kumbusu mwenza kabla ya kwenda kazini au kwenye mihangaiko.

Pia inapofika mchana tuma ujumbe wa kumchangamsha na kumchekesha mwenza wako,Mvunje mbavu ajisikie mujarabu. Ni vizuri pia kujali ukiona mwenza wako anajisikia vibaya au kapooza. Muulize kuna nani?

Ukiona kuna jambo linakukera mwambie mwenza wako, mfahamishe kwa njia iliyo bora ili kuepusha malumbano.

Usijidai kusema niko poa wakati unajua kabisa unajisikia vibaya kutokana na aliyokufanyia ama ulichoona, pengine kusikia akisema au unaumwa. Usimwachie mwenza kubuni kuwa una tatizo, liseme.

Si hivyo tu , pengine kuna imani miongoni mwa watu kuwa ili wanandoa waonekana kuwa wanapendana ni lazima wawe pamoja muda wote kama kumbukumbu. Si lazima. **BBC**

AFYA

# Vifo vya wazazi, utoaji mimba usiosalama unahusika...



Watoto ni wasikivu na waelewa. Iwapo watafundishwa maadili mema nyumbani, shule na kwenye jamii wanazoishi, matatizo ya mmomonyoko wa maadili unayosababisha mimba za udogoni na utoaji mimba usio salama yanaweza kupungua. **PICHA: MTANDAO**

**Na Mwandishi Wetu**

UKISIKILIZA hoja na ujumbe unaotolewa katika mikusanyiko iwe makanisani, misikitini na kwenye majukwaa ya kijamii ni kawaida kusikia wadau wakizungumzia siasa, demokrasia, maendeleo, amani na umaskini, lakini hakuna anayetaja 'kitanzi' cha utoaji mimba kinavyoangamiza wanawake wa Tanzania.

Ni tatizo linalowahusu wengi, lakini jambo hili halisikiki. Si shuleni ambako mabinti na vijana wanajamiiana na mabinti wengi hupata ujauzito pasipo na wakuwasaidia kuanzia kwenye familia watoto hao wanapolelewa.

Ndiyo maana pengine ni wakati wa kuzungumza kuhusu athari za utoaji mimba na kuwafahamisha

> **Shule inamtumia daktari huyu kutupima ujauzito kila wakati. Akikugundua kama una fedha kidogo anakusaidia.**

wanawake , mabinti, vijana na wanaume kuhusu changamoto zake ili kuvunja ukimya.

Aiye Nduru ni binti wa miaka 19, mkazi wa Mwanza, anayezungumza na Nipashe kuhusu utoaji mimba kienyeji, anasema ni mhanga wa tatizo hilo. Binti huyo, anaishi Makaroboi jijini humo, anasema maisha ni magumu, anafanya ngono ili kujikimu. Anasema katika umri wa miaka 19, amekutana na wanaume kadhaa na kutoa mimba tatu.

"Nikiwa na miaka 14 nilijiingiza kwenye uhusiano wa kingono na mwanafunzi wa sekondari jirani ambaye tulidumu kwa miaka mitatu. Ana fedha na ananipatia fedha. Pamoja naye nilishirikiana na wanaume wengine. Katika uhusiano huu nimetoa mimba mara tatu," anasema.

Mwanafunzi huyo anakiri kuwa anafahamu kuwa utoaji mimba ni jinai na hairuhusiwi, lakini hakuwa na mbadala. Katika shule anayosoma mmoja wa madaktari katika chuo jirani (jina linahifadhiwa) anawasaidia kutoa mimba kwa gharama ndogo ambayo wengi humudu.

"Shule inamtumia daktari huyu kutupima ujauzito kila wakati. Akikugundua kama una fedha kidogo anakusaidia. Lakini hata ukimwendea na kumweleza anakusaidia kuharibu ujauzito" anasema Aiye na kuongeza kuwa mimba zote tatu ziliharibiwa na daktari huyo.

Tanzania kama zilivyo nchi nyingi za Afrika kama Kenya, Uganda na Nigeria utoaji mimba ni kosa la jinai na hufanyika tu kwa minajili ya kuokoa maisha ya mjamzito.

Hata hivyo, katika mazingira hayo mimba zaidi ya 405,000 hutolewa kila mwaka tena nyingi zikitolewa kienyeji na katika mazingira hatarishi, lakini pia idadi ya vifo vya wanawake vinavyohusiana na uzazi nchini ni kubwa ikifikia 556 kwa kila vizazi hai 100,000. Kwa mujibu wa takwimu za utafiti wa makazi na afya (DHS) ya mwaka 2015/16.

Vifo hivyo hutokana na changamoto kama ukosefu wa huduma, utokaji damu kupindukia, kujifungulia nyumbani pamoja na utoaji mimba usio salama. Hivi hali hiyo haiwalazimishi watu kuzungumzia jambo hilo?

Kadhalika, mkoa unaoongoza kwa vifo hivyo ni Dar es Salaam na Mwanza ni wa pili, kwa mujibu wa takwimu za vifo vya wazazi zilizokusanywa kutoka katika hospitali za Tanzania na Waratibu wa Afya ya Uzazi na Mtoto wa Tanzania Bara, mwaka 2018.

Dokta Anna Temba, mbobezi wa tiba ya afya ya uzazi, akizungumza na Nipashe kuhusu tatizo la utoaji mimba usio salama nchini, ananukuu utafiti uliofanywa na chama cha madaktari bingwa wa wanawake na afya ya uzazi Tanzania (AGOTA) na Shirika la Amref Health Africa wa mwaka 2016, kuwa takribani mimba 405, 000 huharibiwa kila mwaka nchini kwa njia zisizo salama.

Idadi hiyo ni kubwa kwa kuwa karibu wanawake nusu milioni wanatoa mimba kwa njia ambazo si salama zinazohatarisha maisha kila mwaka kwa mujibu wa takwimu hizo.

Kwa kuwa tatizo hilo ni kubwa na wanawake wengi wanahusika njia mojawapo ya kuwasaidia ni kuzungumzia na kuhamasisha uelewa na mambo ya kujamiiana na kupata mimba miongoni mwa watoto (jamii ya watu walio chini ya miaka 20) ili wawe na ufahamu.

Kama anavyosema mtaalamu huyo kuwa mimba 400,000 hutolewa kila mwaka huenda idadi ni kubwa kwasababu hakuna anayejua ukweli kwa vule hufanywa kwa kificho mno.

Katika maelezo ya Aiye anasema wanapewa dawa na mganga, lakini pia wapo waganga wa mitaani

AFYA

# Vifo vya wazazi, utoaji mimba usiosalama unahusika...

na wa kienyeji wanaowasaidia mabinti na wanafunzi kuharibu mimba. Anakiri kuwa alijiingiza katika mahusiano bila kujua athari za kujamiiana, kupata mimba na kuzitoa . Yote hiyo ni kwa sababu si wazazi wala walezi waliomweleza.

**ELIMU IANZE SASA**

Ili kuondoa pengo hilo muuguzi na mkunga, Joanes Sanga, wa Hospitali Teule ya Rufaa Tumbi, mkoani Pwani, anashauri taifa liamke sasa lianze kufundisha watoto na vijana athari za utoaji mimba usio salama pamoja na kuhamasisha vijana kuacha kujamiana katika umri mdogo.

"Watu hawajui athari na utoaji mimba kwani hufanyika kwa usiri mno na wakati mwingine mganga hao si wataalamu, wanatoboa wanawake mfuko wa uzazi, utumbo na kibofu. Yote haya yanaathiri afya, utaratibu wa viungo vya uzazi na hata kuleta kifo." Anasema Sanga.

Anashauri kuwa na uharaka katika kutengeneza utaratibu na mifumo ya kuwafundisha vijana, kusisitiza maadili, elimu ya kujitambua , kuacha kufanya ngono za ututoni na kuthamini afya zao ili wafunzwe shuleni, nyumbani na kwenye semina na mafundisho ya kidini.

"Kama taifa tunahitaji kuwaeleza watoto wetu kuwa utoaji mimba ni hatari kwa kuwafahamisha mabinti na wanawake na vijana kuwa utoaji unapofanywa kwa njia zisizo salama hata kwa kupewa dawa ambazo dozi hazifahamiki ni hatari. Wakati mwingine zinaweza kuchana mfuko wa kizazi, kuleta kutokwa damu nyingi na mwisho ni kufa kama hakuna huduma." Anasema Sanga.

Anakumbusha kuwa kila mara mama anapobeba mimba kizazi huwa dhaifu, hivyo kuhitaji uangalizi wa kitaalamu na kuonya kuwa kuwapa wanafunzi mara kwa mara dawa za kutoa mimba kama Mesoprostal ni hatari kwani waganga wa mitaani hawafahamu hali ya kizazi cha mhusika, ndiyo maana vifo vinatokea.

Sanga anaonya kuwa wapo watu wanaotumia dawa hizo 'kienyeji' kwa mfano kutumia dozi kubwa kwa kumeza, kuweka sehemu ya haja kubwa na vidonge vingine kwenye njia ya uzazi. Hii ni hatari mno. Kwani dozi ni kubwa kupindukia inayoweza kusababisha kupasuka sehemu za haja kubwa, mfuko wa kizazi na kutoka damu nyingi, kuharibika viungo vya uzazi na wakati mwingine kupoteza maisha.

Muuguzi na mkunga huyo aliyefanyakazi kwa zaidi ya miaka 15, anasema tatizo hilo ni matokeo ya dawa kuchochea uchungu kwa nguvu kubwa kwenye misuli ya mfuko wa kizazi na sehemu nyingine.



Mabinti wakiachwa bila maonyo na kuhamasishwa kuachana na mienendo ya maadili maovu huishia kufanya maasi mitaani ikiwamo kuuza miili yao. Pichani ni baadhi ya wasichana kwenye miji mikuu ya Afrika wakingoja wateja kwa ajili ya biashara ya ngono. **PICHA: MTANDAO.**

> **Kabla ya kufikiria kubadili sheria ni lazima kuwafundisha wanawake, mabinti na jamii athari za jambo hili. Jukumu hilo halijafanyika.**

Muuguzi anawakumbusha wanawake na mabinti kuwa kupata maambukizi ya utoaji mimba huleta magonjwa na makovu yanayosababisha mirija ya mayai kuziba. Aidha kizazi nacho huwa na makovu ambayo husababisha ugumba.

**SHERIA**

Muuguzi na mkunga Sanga, akizungumzia sheria anasema siyo tatizo. Anasema sheria inaharamisha utoaji mimba, labda ikiwa ni kuokoa maisha ya mjamzito ni muhimu iendelee kuwepo ili kulinda uhai.

"Kabla ya kufikiria kubadili sheria ni lazima kuwafundisha wanawake, mabinti na jamii athari za jambo hili. Jukumu hilo halijafanyika. Wanawake na kila mmoja anafahamu kuwa kutoa mimba kuna adhabu ya kifungo jela, lakini kuna aliyewafundisha kuhusu athari na ubaya wa utoaji huo ?" anahoji.

Ibara ya 230 ya Sheria ya Mwenendo wa Makosa ya Jinai Tanzania inaruhusu utoaji mimba kufanyika ili kuokoa maisha ya mjamzito yanayoweza kuhatarishwa na mimba aliyobeba na sivinginevyo.

Aidha, ibara ya 16 ya sheria hiyo kuanzia kifungu cha 150 hadi 152 inakataza kutoa mimba na adhabu kwa anayepatikana na hatia ni kifungo cha miaka saba jela na yeyote aliyesaidia kufanikisha mchakato huo, anafungwa jela miaka mitatu.

Sanga anasema ni wakati wa kuandaa mikakati ili kufundisha masuala ya uzazi na pia athari za utoaji mimba huo kwani mabinti, wanawake na pia wana ndoa wanapoteza maisha kutokana na tatizo hiyo badala ya kufikiria kubadili sheria.

**DAWA ZA ASILI**

Katika mazungumzo kuhusu dawa za asili zinazotumiwa kuharibu mimba, wanawake wanataja juisi ya mwarobaini, chai ya rangi, aloivera na majani ya migomba na kwamba kuna aina nyingine nyingi za majani machungu yanayoweza kutumiwa kuchochea uchungu na kuharibu mimba.

Lakini, ni kweli dawa hizo hutoa mimba? Nipashe inahojiana na Mkurugenzi wa Taasisi ya Tiba za Asili katika Chuo Kikuu cha Muhimbili jijini Dar es Salaam, Dk. Joseph Otienno, ili kuujua ukweli.

Mtaalamu huyo anakiri kuwa hakuna utafiti uliofanywa na taasisi hiyo kuhusu nguvu ya dawa hizo, hivyo hawezi kuthibitisha au kukanusha.

Lakini anaonya kuwa huenda aloivera au mwarobaini hazifanyi kazi hiyo.Anasema japo kuna watafiti wa kigeni walishafanya uchunguzi kwenye eneo la utoaji mimba usiosalama kwa kutumia dawa za asili, taasisi yake haifanya utafiti akieleza haja ya kufanya hivyo ili kuuelimisha umma.

Dk. Ottieno, anasema hana uhakika kuwa uchungu unaopatikana kwenye mimea hiyo inaweza kuwa ni chanzo cha kuharibu mimba na kueleza kuwa huenda kuna imani miongoni mwa wanajamii kuwa dawa hizo zina athari, lakini kinachohitajika ni kutafiti na kulinganisha kemikali zilizoko kwenye aloivera, mwarobaini na zilizomo kwenye dawa nyingine za kitaalamu zinazofungua njia ya uzazi ili kuujua ukweli na kuondoka gizani.

Dawa zinazotumiwa rasmi kufungua njia za uzazi na kuanzisha uchungu ni mesoprostal, ambayo katika nchi zenye sheria inayoruhusu kutoa mimba inatumiwa bila kikwazo.

AFYA

MCHANGO DAMU MANYARA

# Wanafunzi wachangia 85% kunusuru wadogo zao, kinamama wajawazito

• Mratibu ageuka kachero kusaka wanaouza • Wanakijiji wajitolea, wafunguka ya kwao

**Na Jaliwason Jasson, BABATI**

KATIKA kuhakikisha binadamu anakuwa na afya njema, damu mwilini ni hitaji muhimu, ikisafirisha hewa safi sehemu mbalimbali, kulisha viungo vya mwili na kuuwezesha kufanya kazi na hatimaye kuwa na afya bora.

Kwa binadamu, upekee wake unashuhudiwa pale awe mtu mzima au mtoto anapopungukiwa na hususan kwa mtoto mwenye umri chini ya miaka mitano inakuwa mtihani mkubwa wa kiafya, vivyo hivyo kwa wajawazito na majeruhi wa ajali.

Mratibu wa Mpango wa Damu Salama wa Mkoa wa Manyara, Japhet Peter, anaitafsiri damu salama ni ile iliyopimwa na ikakutwa haina kasoro yoyote, hivyo kufaa kwa ajili ya wahitaji wengineo.

Peter anayataja magonjwa manne, ambayo hupatikana zaidi kwenye damu wanazozipima, akiyataja kuwa ni: Virusi vya Ukimwi; kaswende; na homa ya ini (Hepatitis B na C) ambazo ndizo zinaoongoza.

Anasema kuna mashine maalumu ya kupima damu hiyo inayoitwa 'Elisa' ambayo inatumika katika upimaji wa damu salama kwa Mkoa wa Manyara, ulioko katika kanda ya Moshi, ambako ndiko uhakiki unafanyika na kwenye benki ya uhifadhi wa damu hiyo.



Wataalamu wa damu salama wakiwa katika maabara ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara. **PICHA ZOTE: JALIWASON JASSON**

### HALI YA MANYARA

Mtaalamu huyo wa damu, anasema hali ya damu ni nzuri sana, akifafanua kuwa mahitaji ya damu kwa mwezi ni chupa 410 kwa mujibu wa takwimu za mwaka jana na anaongeza: "Hospitali yetu ya mkoa matumizi ya awali yalikuwa chupa 60 na sasa hivi ni chupa 83 kwa mwezi na kufuatana na idadi ya watu kwa kila Halmashauri ndani ya mkoa, tunatakiwa kukusanya chupa 818 kwa mkoa mzima,"anaeleza Peter

Anasema, kila halmashauri ya Manyara inatakiwa ikusanye asilimia moja ya damu ya watu wake, katika kuchangia kuokoa maisha ya watu wahitaji wake wa damu.

Peter anataja makundi muhimu yanayokuwa na mahitaji ya damu ni, mama wajawazito, watoto walio chini ya miaka mitano na majeruhi wa ajali mbalimbali zinazojitokeza.

Mratibu huyo anatoa mfano akirejea taarifa ya mwezi Mei mwaka huu, kuwa watoto 80 chini ya umri wa miaka mitano katika mkoa mzima, waliongezewa damu, lakini anatoa angalizo kuwa kadri umri unavyoongezeka na ndivyo matumizi yanavyoongezeka.

Kwa mujibu wa mtaalamu huyo wa damu, anashukuru juhudi za uchangiaji damu kutoka kwa umma, kwamba imekuwa msaada muhimu kuokoa maisha ya wahitaji hao 494.

> **kila halmashauri ya Manyara inatakiwa ikusanye asilimia moja ya damu ya watu wake, katika kuchangia kuokoa maisha ya wahitaji wake wa damu.**



Damu salama ikiwa kwenye jokofu katika maabara ya Hospitali ya Rufaa ya Mkoa wa Manyara.

### WANAKOPATA DAMU

Peter anasema, kiasi kikubwa cha damu wanazipata kutoka michango ya shule za sekondari, vyuo vya ufundi stadi wanaochangia damu kwa asilimia 85. Kilio chake ni kwamba, shule zinapofungwa huwa benki ya damu inapata shida kukusanya damu.

Anataja vyanzo vilivyobaki ni kutoka kanisani na misikitini na kuna timu walizounda kutoka halmashauri za mkoa zilizopewa majukumu ya kukusanya damu kadri wawezavyo, ili iweze kuisaidia jamii inayohitaji hospitalini.

Mratibu anasema faida za kuchangia damu ni kupimwa afya bure, kujua kundi lako la damu na kupata kadi na kutambulika kila sehemu ya nchini.

Kuhusu kundi muhimu la damu analitaja kuwa 'O' chanya (O positve) ndilo linawasaidia sana wahitaji wa damu kuliko makundi mengine ya damu.

Je nini umri wa mwisho wa damu iliyohifadhiwa, Peter anaiambia Nipashe kuwa ni siku 35 tangu itolewe kwa mchangiaji wa damu, ikihifadhiwa vizuri kwenye sehemu ambayo isiyo na joto la ziada.

"Damu haitupwi, huwa ikibaki siku saba kuharibika huwa tunawaagiza waratibu wetu damu wa halmashauri zote kuileta damu ambayo imebakiza siku hizo hapa hospitali ya mkoa. Sisi tunaikagua na kuwasiliana na mikoa mingine jirani yenye uhitaji na kuwapatia. Hata sisi hivyo hivyo huwa wanatupatia tukihitaji," anafafanua

Anasema ikitokea Mratibu wa Damu Salama wa Halmashauri, akagundua damu aliyohifadhi imebakia siku chache zaidi kuharibika ndio akatoa taarifa huyo, mtaalamu anasema anawajibishwa kwa uzembe wa kusababisha mali hiyo ya umma kuharibika.

### DAMU INAUZWA?

Mratibu Peter, anakiri kuwapo malalamiko ya wananchi kuuziwa damu, pindi alipopewa nafasi hiyo mwaka mmoja uliopita, ila anasema katika kipindi chake hajasikia kuwapo uuzaji huo wa damu kwa wagonjwa, ambao ni haki yao kupewa bure.

Peter anajitetea kwamba, amekuwa akifanya uchunguzi kubaini matukio hayo, akifuatilia hadi kuhoji vijijini kupata ukweli huo kwa wananchi ambao ndio wahitaji.

Pia, anapinga malalamiko ya wachangiaji wa damu, kwamba inapotokea ndugu zao wanakataliwa kupewa huduma hiyo, akifafanua kuwa sharti la mtu anayechangia damu kumpa ndugu yake wameainisha kuwa kama ni kwa mwenye familia anatakiwa ampeleke mke wake au watoto wake ndio wasaidiwe kuongezewa na siyo nje ya hapo mfano ndugu yeyote.

Hivyo, anatumia fursa ya mazungumzo yake na Nipashe kuomba ndugu sahihi waliokubaliana wawachangie siyo kila mtu. Anafafanua kanuni ya kiafya ya kuchangia damu ni wanaume wanaochangia ni kila baada ya miezi mitatu na wanawake kila baada ya miezi minne.

Anasema miongoni mwa changamoto zinazowakabili ni pamoja na baadhi ya halmashauri kukosa usafiri, bajeti ya kitengo cha damu haipewi kipaumbele na jiografia ya eneo husika, mfano wafugaji wanatumia nguvu nyingi kuwashawishi kuchangia, kutokana na mfumo wao wa maisha.

Ushauri wake wa kitaalamu ni kwamba, ili mtu awe na damu ya kutosha, ni vizuri akala mboga za majani na vyakula vya kuwapatia lishe bora huku akiwaomba viongozi wa kisiasa hasa wakuu wa wilaya na mkuu wa mkoa kuiweka kuwa ni ajenda ya kudumu katika mikutano yao kuhusu damu ili jamii iamke na kuchangia damu.

### WANANCHI JE?

Mkazi wa Nangara, Mustafa Rwamcho, anasema damu ni kitu muhimu katika mwili wa binadamu hivyo anawasihi Watanzania kujenga tabia ya kuchangia damu, ili iwasaidie watoto walio na umri chini ya miaka mitano, kwa maana ya kujenga Taifa la kesho.

Binafsi akijitambulisha kuwa mchangiaji mzuri, anasema watu wanapenda kuchangia damu, ila wanaogopa kwa kuwa wengine wakichangia damu inaenda kuuzwa na inakuwa haiwasaidii walengwa kama watoto na wajawazito, hivyo inawakatisha tamaa ya kuchangia, ila anadai kuwa mchangiaji ni vizuri unapimwa na magonjwa mengine.

Kuhusu wanaouza damu inayochangiwa na watu mbalimbali, anashauri wakibainika wataalamu wa namna hiyo wawajibishwe kwa hatua kali za kisheria.

Mkazi wa Hangoni, Sylivester John, anasema watu wanaochangia damu wanafanya vizuri kwa kuwa wanasaidia kuokoa maisha ya watu wakiwemo watoto wadogo wanaokua na wajawazito.

John anadai, aliwahi kuchangia ndugu yake damu hivyo anaona kuchangia damu kuna faida kubwa kwa watu wenye mahitaji na kuhusu wanaouza damu anasema wachukuliwe hatua kali za kisheria na ikiwezekana wawekwe kizuizini, maana ni wezi kama wezi wengine wa mali za umma.

Mkazi wa Riroda, Juma Ramadhan, anasema anaogopa kuchangia damu kwa kuwa damu itakuwa inamsumbua kuwa anaitoa kila mara, lakini anaogopa anaweza kuambiwa ana virusi vya ukimwi, hivyo kumfanya aishi kwa hofu ni bora akae hivyo hivyo.

Neema Hiiti mkazi wa Magugu, Babati, anasema hajawahi kuchangia damu, ila anafahamu kuwa damu inahitajika kwa ajili ya kuwaongezea watoto wadogo wanaopungukiwa na damu, pamoja na wajawazito ila anasema elimu ya kuchangia bado haitolewi ipasavyo hasa kwa maeneo ya vijijini.

> **Kwa kipindi cha mwaka 2016 mpango wa Taifa wa Damu Salama ulikusanya chupa 196,735 sawa na asilimia 40 ya mahitaji.**

Mwingine, Lilian Sanka mkazi wa Dudiye, anasema ili damu ipatikane kwa wingi, wataalamu wa damu waweke utaratibu wa kukutana na wananchi vijijini kuwaelimisha faida za kuchangia damu, ili jamii iamke na kutoa huduma hiyo.

Bahati Herman, maoni yake ni kwamba serikali iwahamasishe wananchi kuchangia damu itakayosaidia vituo vya afya na zahanati pasipo usumbufu wowote, hivyo anashauri wataalamu wajipange vizuri kuvuna damu ya Watanzania.

Kwa mujibu wa Shirika la Afya Duniani (WHO), linapendekeza ili kukidhi mahitaji ya damu, nchi inatakiwa kukusanya chupa 10 kwa kila wananchi 1000 sawa na asilimia moja ya wananchi kwa mwaka husika na ndio maana WHO, limeweka utaratibu wa kuadhimisha Siku ya Uchangiaji Damu kila mwaka.

Kwa kipindi cha mwaka 2016 mpango wa Taifa wa Damu Salama ulikusanya chupa 196,735 sawa na asilimia 40 ya mahitaji.

Mwaka 2017 ziliongezeka chupa hadi 233,953 sawa na asilimia 45 ambapo kwa taarifa za kitaifa za Mpango wa Damu Salama za Mwaka 2017, mikoa iliyoongoza kwenye makusanyo ya damu kulinganisha na malengo ni Katavi (94%); Lindi (79%) na Pwani(66%) na huku mikoa ambayo haikufanya vizuri ni Songwe (16%), Mbeya (20%); Tabora (22%).

## Ndege wanatishiwa afya na sigara

MPIGA picha za wanayamapori amepiga picha ya ndege aliyekuwa akimlisha kinda kipande cha sigara kilichobaki baada ya kutumika, katika ufukwe mjini Florida nchini Marekani.

Katika ukurasa wa Facebook, Karen Mason, anasema aliwaona ndege hao mwezi uliopita. "Kama utavuta sigara, tafadhali usiache mabaki ya sigara."

Taasisi ya kutunza mazingira ya hifadhi nchini Uingereza imesema picha hiyo "inasikitisha".

Mason alipiga picha nyingine ya kinda akiwa amebeba kipande cha mabaki ya sigara mdomo wake.

Ndege hufanya makosa kuwalisha makinda vipande vya sigara kwa kudhani ni chakula.

"Ndege wengi wana shauku kuhusu vitu ambavyo tunavitupa, na mara nyingi huchunguza kwa kuvijaribu ili kujua kama ni chakula au la," msemaji wa taasisi ya kulinda ndege aliiambia BBC.

"Inasikitisha, mzazi huyu ameamua kuwa mabaki ya sigara kuwa kitu cha kumlisha kinda wake.



"Viumbe hawa wanajaribu kuendana na vitu tunavyofanya duniani; kila mwaka, tunaona wanyama wengi wakinasa, wakijeruhiwa na hata kufa kutokana na vitu vinavyosababishwa na binadamu.Huwa tunawaona wanatumia takataka kutengeneza viota vyao.

"Kwa bahati mbaya kwa watu wengi, takataka zinaonekana kama hazina madhara, lakini hufanya eneo kuwa chafu; hatahivyo, picha za kusikitisha zikionyesha madhara ya takataka kwa viumbe."

Vichujio vya sigara vinatengenezwa kwa nyuzi nyuzi za plastiki, hivyo huchukua miaka kuoza kwenye mazingira.

Mabaki ya sigara ni miongoni mwa aina ya takataka zinazokusanywa kwa wingi kwenye fukwe za bahari duniani, kwa mujibu wa wanaharakati wa mazingira. **BBC.**

AFYA

# Nkasi inavyobadilisha kwa kasi sura ya huduma za afya



Mkuu wa Wilaya ya Nkasi, Said Mtanda, akizungumza na waandishi wa habari (hawapo pichani) ndani ya wodi ya kituo cha afya cha wilaya hiyo. **PICHA: MARY GEOFREY.**

**Na Mary Geofrey, aliyekuwa**

**Nkasi**

MOJAWAPO ya masuala pasua kichwa yanayotikisa sekta ya afya si Tanzania tu bali mataifa mengi yanayoendelea ni vifo vya wazazi na watoto.

Tanzania kwa upande mwingine vifo hivyo viko juu vikifikia wanawake 556 kwa kila vizazi hai 100,000, hivyo ili kuondoa changamoto hiyo serikali inaweka mikakati mbalimbali ya kupunguza idadi hiyo ili ifikie chini ya 70 ifikapo mwaka 2030.

Sera ya Mpango wa Maendeleo wa Afya ya Msingi (MMAM) iliyoanza kutekelezwa mwaka 2007 hadi 2017 kila kijiji kinapaswa kuwa na zahanati na kila kata kuwa na kituo cha afya ili kuhudumia wananchi wa ngazi zote kuanzia vijijini hadi kwenye rufani.

Katika kutekeleza hilo, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi), imeandaa mipango mkakati ya kuboresha huduma hizo ili kuhakikisha Sera ya MMAM inatekelezwa kwa vitendo.

Moja ya mikakati iliyowekwa ni kuboresha huduma za afya ngazi ya msingi katika zahanati na vituo vya afya ambako ndiko walipo wananchi wengi. Malengo yaliyowekwa na nchi ni kwamba ifikapo mwaka 2020 vifo vitokanavyo na uzazi vipungue hadi kufikia 292 katika vizazi hai 100,000.

Aidha, makubaliano ya Umoja wa Mataifa ya Maendeleo Endelevu(SDG), ambayo nchi wanachama zimeyaridhia ikiwamo Tanzania, yanayaelekeza mataifa hayo kupunguza vifo vya wazazi hadi kufikia chini ya 70 katika vizazi hao 100,000 ifikapo mwaka 2030.

> **Maji hayatoshelezi hivyo kuiomba serikali kuwafikishia maji ili kazi ziweze kufanyika wa urahisi na kwa wingi zaidi.**

Ndiyo maana katika kutekeleza mipango ya kuboresha afya za wananchi, Wilaya ya Nkasi iliyopo mkoa wa Rukwa ni moja ya halmashauri ambazo zimejizatiti kuhakikisha wanaboresha huduma za afya kwa wananchi wake na kufikia azma ya MMAM.

Mkuu wa wilaya hiyo, Said Mtanda, anapotembelewa na wanahabari waliofika ofisini kwake ili kufahamu miradi ya maendeleo inayotekelezwa na wilaya hiyo, kubwa analolionea fahari na kuwaeleza ni ujenzi wa kituo cha afya cha Nkomolo.

"Nawezasema wilaya hii tunatekeleza miradi mingi ya maendeleo lakini mradi mkubwa ambao naona fahari kuuzungumzia au kuwaeleza na mpate fursa ya kuutembelea ni huu wa kituo cha afya cha Nkomolo," anasema Mtanda.

Anaeleza kuwa kituo hicho ambacho kipo tarafa ya Namanyere, kilianzishwa mwaka 1999 baada ya kupandishwa hadhi kutoka katika huduma za afya ya mama na mtoto (RCH) na kuwa kituo cha afya kwa lengo la kuboresha na kutoa huduma za afya kwa wananchi.

Mtanda anasema kituo hicho ni miongoni mwa vituo vya afya saba vilivyopo katika Halmashauri ya Wilaya ya Nkasi na kinahudumia zaidi ya wananchi 22,937 walio katika eneo la kazi la kituo (Catchment Area).

Anasema wananchi wanaohudumiwa na kituo hicho wanatoka katika kata tano za Nkomolo, Namanyere, Majengo, Isunta na Kipundu.

"Pamoja na kuhudumia kata hizi kituo kinatoa huduma za afya ya uzazi kwa akina mama wajawazito kutoka katika maeneo mbalimbali ya wilaya hiyo, takribani kinamama wajawazito 4, 550," anasema Mtanda.

Anaeleza pia kuwa wateja wengine wa rufani wanapokelewa kutoka katika zahanati za Msilihofu, Kizi, Miombo, Isale, Mtenga, Ntuchi, Kate, Ntatumbila, Mkole na zahanati nyingine kutoka mwambao wa Ziwa Tanganyika.

### HUDUMA ZINAZOTOLEWA

Mganga Mkuu wa kituo hicho, Everada Sanane, anasema wanatoa huduma za uzazi salama ikiwa ni pamoja na upimaji wa wajawazito, ushauri nasaha na kuzuia maambukizi ua VVU kutoka kwa mama kwenda kwa watoto.

Anasema pia wanatoa huduma za kuzalisha, upasuaji, uchunguzi wa X-Ray, ultrasound, huduma ya kuhifadhi maiti, maabara, upimaji wa watoto chini ya miaka mitano na kutoa chanjo kwa magonjwa yanayozuilika kwa chanjo.

Anasema pia wanatoa tiba kwa wagonjwa wa nje na ndani, huduma ya tohara kwa wanaume, huduma ya kinywa na meno na huduma za upimaji wa VVU na huduma za tiba na matunzo kwa wagonjwa wanaoishi na Virusi Vya Ukimwi.

Mganga huyo anasema kituo hicho ni miongoni mwa vituo vya afya 44 vilivyopatiwa fedha na Tamisemi kupatia mpango wa Sh. milioni 500 kwa ajili ya kuinua kituo.

"Fedha hizi ziliingia kwenye akaunti ya afya tangu Septemba mwaka 2017 na hadi sasa shughuli za ujenzi zimekamilika na huduma mbalimbali zinaendelea kutolewa hadi sasa," anasema Sanane.

Anasema fedha zililenga ujenzi wa jengo la upasuaji, wodi ya kina mama na watoto, ujenzi wa maabara, kliniki ya baba, mama na mtoto, jengo la matibabu kwa wagonjwa wa nje na jengo la kuhifadhia maiti.

"Kwa ujumla majengo yote yamekamilika na yameanza kutumika kwa ajili ya kuhudumia wananchi wa kata hii na kata jirani," anasema.

Anasema kufuatia kukamilika kwa kituo hicho cha afya, wamefanikiwa kutoa huduma bora za matibabu kwa urahisi, kuongeza wateja wanaofika katika hospitali hiyo wakiwamo akina mama wajawazito.

### KUHIFADHI MIILI

Adha, Sanane anasema kwa mara ya kwanza wamejenga jengo maalumu la kisasa la kuhifadhia maiti lenye majokofu katika kituo hicho tangu kilipoanzishwa miaka 45 iliyopita.

Anasema tangu wilaya hiyo ilipoanzishwa mwaka 1974, haikuwa na chumba maalumu cha kuhifadhia maiti chenye majokofu, lakini sasa kimejengwa katika kituo hicho na tayari kimeanza kazi kikiwa na miili ya watu waliofariki wanaosubiri taratibu za maziko.

Sanane anasema chumba hicho kina uwezo wa kuhifadhi miili sita kwa muda mrefu kwa kuwa kina majokofu tofauti na awali.

### CHANGAMOTO

Sanane anasema kituo hicho kina changamoto kubwa ya njia ya kupitisha wagonjwa kutoka jengo moja kwenda jengo jingine hali inayosababishwa kubebwa na wahudumu jambo ambalo ni hatari kwa wagonjwa.

"Hatuna 'walkways' hivyo wagonjwa wanalazimika kubebwa na watoa huduma za afya jambo ambalo ni hatari, wanawaza kudondoka au kumuumiza mgonjwa wakati wa kumuhamisha kutoka sehemu moja kwenda nyingine," anasema Sanane.

Anaeleza changamoto nyingine ni upatikanaji wa maji unaopelekea ugumu wa utendaji kazi kwa baadhi ya idara ikiwamo ya upasuaji na uzazi.

Anasema maji hayatoshelezi hivyo kuiomba serikali kuwafikishia maji ili kazi ziweze kufanyika wa urahisi na kwa wingi zaidi," anasema.

Kadhalika anasema changamoto nyingine ni uhaba wa vyoo kwani vilivyoko havitoshelezi na kuzitaja sehemu zenye uhaba kuwa wodi za kliniki, maabara na sehemu ya kuhudumia wagonjwa wa nje.

### MAFANIKIO

Mganga Mkuu wa Kituo Dk. Everada Sanane, anasema mbali na kuwapo kwa changamoto hizo, kituo hicho cha afya kina idadi ya watoa huduma 52 kati ya watumishi 55 wanaohitajika na hilo ni fanikio.

Anasema pia katika kuimarisha utawala bora kituo hicho kina kamati ya uendeshaji yenye wajumbe nane kati yao wanaume watano na wanawake watatu kwa kuzingatia miongozo.

Anasema kamati hiyo inafanya vikao vyake vya kisheria kila baada ya miezi mitatu na hukutana panapotokea dharura.

MAZINGIRA

MABADILIKO TABIANCHI

# Ulaya yaachana na hewa ukaa, nchi changa ziko njia panda



Mkurugezi wa Kitengo cha Wataalamu wa Nishati na Hali ya Hewa kutoka Umoja wa Mataifa, Richard Black (kushoto) akizungumza na waandishi wa habari mjini Bonn. Kulia ni Mkurugenzi wa Hali ya Hewa na Nishati nchini Uingereza, Archieng Young. **PICHA: JENIFER JULIUS**

**Na Jenifer Julius, Bonn**

MKUTANO mdogo wa hali ya mabadiliko ya tabianchi umemalizika wiki iliyopita jijini Bonn, Ujerumani na tayari nchi zilizoendelea 17 zimeingia makubaliano ya kuondoa kabisa uzalishaji wa hewa chafu inayoongeza joto duniani.

Taarifa hiyo ilitolewa na Mkurugezi wa Kitengo cha Wataalamu wa Nishati na Hali ya Hewa kutoka Umoja wa Mataifa, Richard Black, alipofanya mkutano na waandishi wa habari.

Akitaja nchi ambazo zimeshaanza utekelezaji huo, Richard alisema ni Bhutan and Suriname tayari zinanyonya mara mbili zaidi ya oksjeni inayozalishwa huku Norway na Sweden zimejiwekea mikakati ya kisheria ya kupunguza hewa ya ukaa mpango mingine kadha ipo njiani.

"Inaleta faraja kuona kuwa nchi hizo na mikoa yake 11 pamoja na majiji 23 yana mipango ya kuondoa kabisa uzalishaji wa hewa ukaa," alisema Black akiwa na uso uliojaa matumaini.

**JITIHADA ZA UINGEREZA**

Uingereza imeshaanza utekelezaji wa kuzuia uzalishaji wa hewa ukaa kwa asilimia 100 kwa kuachana na matumizi ya makaa ya mawe katika shughuli mbalimbali za viwandani, majumbani na maeneo mengine yaliyokuwa yanategemea nishati hiyo.

Ni kwa mujibu wa Archieng Young, Mkurugenzi wa Hali ya Hewa na Nishati nchini Uingereza. Akizungumza katika mkutano huo na wanahabari alisema wakazi wa nchi yake wameshaanza kusahau matumizi ya makaa ya mawe na wamejikita kwenye umeme wa vyanzo vingine kwa matumizi ya nyumbani.

"Mwanzoni utekekelezaji ulikuwa wa tabu sana, ilikuwa vigumu kuwashawishi wananchi kuacha kutumia makaa ya mawe, lakini serikali iliongeza nguvu ya uhamasishaji na uelimishaji na sasa tupo katika nafasi nzuri," alisema Young.

> "Unapoongelea suala la kuondoa uzalishaji wa hewa hii kwa nchi zinazoendelea nadhani halitawezekana kwa sasa, Ina maana ziachane na biashara kama vile ya mafuta, makaa ya mawe na gesi ambayo ndio chanzo cha nishati kwa maendeleo yao.

**CHANGAMOTO**

Ingawa mataifa yamekubaliana kuzuia uzalishaji wa hewa ukaa katika nchi zao, matokeo yanaweza kutofautiana kutokana tofauti za kiitikadi na kiuongozi anaeleza Black.

Moja ya sababu aliyoitaja ni tofauti ya sheria na taratibu za nchi husika, akihusisha vipaumbele ilivyojiwekea, mfano wakati Uingereza imeshapitisha sheria ya kutotumia makaa ya mawe, wakati Sweden ndio inatengeneza muswada wa kuzuia uzalishaji wa hewa hiyo.

Sababu ya pili ni shughuli za kiuchumi kutegemea nishati ya makaa , ukizingatia kuwa nchi nyingi zilizoendelea zinategemea viwanda ambavyo ndiyo chanzo kikuu cha hewa ya kabon kwa hivyo kunahitajika teknolojia mbadala kuzuia hewa hiyo kuzalishwa.

Anataja sababu ya tatu kuwa ni utofauti wa sera baina ya nchi moja hadi nyingine, wakati será ya nchi moja imeipa kipaumbele sayansi na teknolojia katika kuzuia uzalishwaji wa hewa chafu mfano matumizi ya nishati jadidifu, nchi nyingine mipango imeegemea kwenye kupanda miti mingi ili kusafisha hewa.

**NCHI ZINAZOENDELEA**

Kwa upande wa nchi zinazoendelea, Black alisema zitakubali kuingia makubaliano ya kumaliza kabisa uzalishwaji wa kaboni ikiwa tu kutakuwa na uhakika wa kupewa msaada wa kifedha kusaidia miradi itakayopelekea kupunguza uzalishaji wa hewa ukaa.

Hoja hii ilijikita kwenye sababu kuwa nchi zinazoendelea bado hazijasimama imara kuzuia uzalishaji wa hewa chafu kwa asilimia 100 kwa kuwa zinatakiwa kutumia nguvu nyingi kujiendeleza ili zikue kiuchumi.

"Ili nchi izuie uzalishaji wa hewa chafu kwa asilimia 100 na kufikia lengo la kiwango cha sifuri -'zero net' inahitaji kuzuia miradi mingi ya kimaendeleao kama vile kutumia makaa ya mawe, gesi na mafuta, vitu ambavyo nchi zinazoendelea zinavihitaji kwa sasa ili kupiga hatua kimaendeleo", alisema Michael Richard, mmoja wa wajumbe wa mkutano huo, uliomalizika Juni 27, mwaka huu huko Bonn, Ujerumani.

Naye mmoja wa wajumbe kutoka Japan, Joeng Chin, alisema kama nchi zinazoendelea zitapata fedha hizo ni vyema kuwekeza katika miradi itakayosaidia kujikinga na athari za mabadiliko ya tabianchi kama vile nishati jadidifu na miradi ya kaboni.

Mjumbe mwingine kutoka nchi zinazoendelea ambaye hakutaka jina lake liandikwe, alisema haoni sababu ya mataifa yenye uchumi unaokua kujikita katika kuondoa kabisa kuzalisha hewa ya kaboni kwa sababu zipo nyuma kimaendeleo na zinahitaji nishati inayotokana na nguvu za makaa ya mawe, mafuta na gesi ili kuendelea .

"Unapoongelea suala la kuondoa uzalishaji wa hewa hii kwa nchi zinazoendelea nadhani halitawezekana kwa sasa, Ina maana ziachane na biashara kama vile ya mafuta, makaa ya mawe na gesi ambayo ndio chanzo cha nishati kwa maendeleo yao. Mimi nadhani hili tuwaachie nchi zilizoendelea kwa sababu wenzetu wapo vizuri kiuchumi, sisi tuangalie kwanza maendeleo ya nchi zetu labda kama tutapatiwa fedha za kutosha," alisema .

Lengo la makubaliano hayo ni kuhakikisha kuwa joto la dunia haliongezeki kufikia nyuzi joto 1.5 kama ilivyotabiriwa katika ripoti ya jopo la wanasayansi lijulikanalo kama IPCC lililofanyia uchunguzi wa kisayansi mwenendo wa mabadiliko ya tabianchi, ukizingatia kuwa kwa sasa nyuzi joto ya dunia imefikia moja.

Mkutano mkubwa wa hali ya athari ya mabadiliko ya tabianchi ujulikanao kama Cop 25, unatarajiwa kufanyika Novemba nchini Chile ambapo hoja mbalimbali zitajadiliwa zikiwamo ambazo hazijapatiwa ufumbuzi katika mkutano uliomalizika Bonn, ikiwamo jinsi ya kuzisaidia nchi zinazoendelea katika kujikinga na athari za mabadiliko ya tabianchi chini ya Makubaliano ya Paris.

**TANZANIA JE?**

Wakati jitihada za kuachana na makaa ya mawe, gesi na nishati ya mafuta Tanzania inajizatiti kuwekeza kwenye uzalishaji wa umeme unaotokana na gesi inayopatikana mikoa ya Mtwara na Lindi.

Aidha, inaandaa mikakati ya kutumia makaa ya mawe ya Mchuchuma na Ngaka, ili kupata umeme wa kutosha wa kuendesha uchumi wa viwanda.

Mapema mwaka huu, serikali ilitangaza nia ya uwekezaji wa kimkakati wa uzalishaji wa umeme wa makaa ya mawe utakaofanywa na Shirika la Mendeleo ya Taifa (NDC) ili kuiwezesha Tanzania kuwa na umeme wa kutosha wa viwanda na matumizi ya kijamii.

Katika mazingira hayo ya kufikia uzalishaji wa kaboni kwa kiwango cha sifuri, taifa lisipopata fedha na teknolojia mbadala pengine kama wataalam walivyosema ni vigumu kuzizuia nchi zinazoendelea kama Tanzania kutumia vyanzo hivyo kupata umeme.

Makaa ya mawe, gesi na mafuta vinapochakatwa kupata nishati huzalisha kiwango kikubwa cha hewa ukaa, inayodhoofisha utando wa ozoni na kuongeza kiwango cha joto duniani hivyo kuleta athari za mabadiliko ya tabianchi zaidi.

AFYA

# Wananchi walivyobuni mkakati wa kujijengea hospitali

• Kila kata yachanga milioni 7.5/-

**Na Sabato Kasika**

KATIKA kuunga mkono juhudi za serikali za kusogeza huduma ya afya karibu na wananchi, wakazi wa Musoma Vijijini mkoani Mara kwa moyo mmoja wamechangia Sh.milioni 157.5 kujenga hospitali ya wilaya.

Ujenzi huo wa majengo nane ya awali, ulianza mwanzoni mwa mwaka huu kwenye kitongoji cha Kwikonero kilichoko katika Kijiji cha Suguti, baada ya serikali kuwachangia Sh. bilioni 1.5 za kuanza ujenzi huo.

Kwa mujibu wa Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney, majengo hayo, ambayo sasa yameanza kuezekwa yatakamilika mwishoni mwa mwezi ujao ni kwamba ni pamoja na maabara, jengo la wagonjwa wa nje (OPD), kliniki ya mama na mtoto, duka la dawa na huduma xray na ultrasound pamoja na jengo la utawala.

"Lengo letu ni kutoa huduma ikiwezekana kuanzia mwezi ujao na itakuwa inahudumia vijiji 68 vinavyounda jimbo hilo la Musoma Vijijini, ambao kwa muda mrefu hawakuwahi kuwa na hospitali ya wilaya," anasema Anney.

Anasema, kwa sasa mafundi wanaezeka majengo matatu na kisha wataendelea na mengine ili kuhakikisha yote yanamalizika kwa wakati na hatimaye hospitali hiyo ianze kutoa huduma ya afya.

"Wananchi wamehamasika wanaunga mkono juhudi za serikali yao ili kufanikisha ujenzi wa hospitali ya wilaya jimboni mwao na wameendelea kuchangia ili kutimiza ahadi yao," anasema Dk. Anney.



Ujenzi wa moja ya majengo ya hospitali ya wilaya ukiendelea. **PICHA: MARY GEOFREY.**

**UTARATIBU UCHANGIAJI**

Dk. Anney anasema utaratibu wa ujenzi wa hospitali hiyo umewekwa na viongozi wa ngazi mbalimbali kuanzia vitongoji hadi kata, ambapo wamehamasishwa na wamekubali.

Anasema kila diwani aliitisha mkutano na kuzungumza na wananchi kuhusu kuchangia ujenzi huo na kwamba mapendekezo ya baraza za madiwani kila kata kuchangia Sh. milioni 7.5 yalikubaliwa na wananchi hao.

Mkuu huyo wa wilaya anasema madiwani wa kata zote 21 kila mmoja anasimamia ukusanyaji wa michango hiyo kwa ajili ya ujenzi, ambao kwa sasa uko katia hatua nzuri.

"Kwa sasa siwezi kutaja kiasi cha fedha hizo ambacho kimeshapatikana, kwasababu bado michango inaendelea kukusanywa...hapa jambo la msingi ni kwamba wananchi wamejitolea kuchangia ujenzi wa hospitali yao," anasema.

Anasema ana uhakika ahadi hiyo ya wananchi itatimia, kwa madai kwamba suala la kuchangia miradi ya maendeleo limekuwa ni la kawaida kwao kuanzia kwenye ujenzi zahanati kila kijijini.

> **Michango yao ikikamilika inaweza kusaidia hata katika ujenzi wa nyumba ya mganga mkuu, hivyo mimi niwashukuru kwa jinsi wanavyojitolea na pia niwaombe waendelee na moyo huo wa kujitolea.**



Jengo la kituo cha afya Mugango

"Michango yao ikikamilika inaweza kusaidia hata katika ujenzi wa nyumba ya mganga mkuu, hivyo mimi niwashukuru kwa jinsi wanavyojitolea na pia niwaombe waendelee na moyo huo wa kujitolea," anasema.

Anasema, kwa moyo huo wa kujitolea, wananchi hao wameshajenga zanahati zaidi ya 20, ambazo sasa zinatoa huduma na wanaendelea kujenga nyingine ili kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati.

"Serikali imeshawahakikishia kwamba inaendelea na utekelezaji wa mpango wa ujenzi wa zahanati kila kijiji, vituo vya afya kila kata na hospitali katika kila wilaya ili kusogeza huduma ya afya karibu nao," kwa mujibu wa maelezo yake.

Anasema, kinachoendelea sasa ni wananchi wenyewe kuunga mkono juhudi hizo, na kwamba ndivyo wananchi wake wamekuwa wakichangia fedha, kusomba, maji, mchango, kokoto ili kufanikisha ujenzi wa zahanati.

"Kwa mwamko walionao, nina uhakika kila kata itafanikiwa kukusanya Sh. milioni 7.5 ambazo wananchi wenyewe wamekubali kuchangia ili zisaidie katika ujenzi wa hospitali hiyo ambayo ni kwa ajili yao," anasema.



Mkuu wa Wilaya ya Musoma, Dk. Vincent Anney

Mkuu huyo wa wilaya anasema kwa miaka mingi wakazi wa Musoma Vijijini wamekuwa wakisafiri umbali wa kilometa zaidi ya 90 kufuata huduma ya afya mjini Musoma na maeneo mengine.

"Lakini sasa hospitali ya wilaya ikikamilika kuna uwezekano mkubwa kwa wananchi hawa kutosafiri umbali mrefu labda iwe ni kwa magonjwa makubwa, ambayo yatasababisha waende hospitali za rufaa," anaeleza Dk. Anney.

Aidha, anasema ili kuepuka changamoto hiyo ya kusafiri umbali mrefu kufuata huduma ya afya hata kwa maradhi yanayotibika hospitalini, wananchi wamekuwa wakijenga zahanati kwa mtindo wa kujitolea.

"Juhudi za kuhamasisha ujenzi wa zanahati kila kijiji zimekuwa zikifanywa na wadau mbalimbali akiwamo mbunge wa Musoma Vijijini Profesa Sospeter Muhongo, ambaye pia anachangia vifaa vya ujenzi," anaeleza.

Anavitaja baadhi ya vifaa hivyo kuwa ni mabati, mbao, nondo, misumari, saruji ikiwa ni njia ya kuhamasisha wananchi kujitolea kuchangia juhudi za kujiletea maendeleo kwenye maeneo yao.

Anasema juhudi hizo zimesaidia pia kuifanya Musoma Vijijini kuwa na vituo viwili vya afya vilivyopo katika kata za Murango na Mugango, ambavyo sasa vinaendelea kutoa huduma kwa wananchi.

"Wakati vituo hivyo vikifanya kazi, zahanati ya Bukima imebadilishwa kuwa kituo cha afya, na sasa inaendelea kuboreshwa ili ianze kutoa huduma, na pia wananchi wa Kata ya Nyambono nao wanajenga kituo cha afya," anasema.

Anasema lengo kuu ni kuhakikisha kila kijiji kinakuwa na zahanati, kila kata inakuwa na kituo cha afya na pia Musoma Vijijini inakuwa na hospitali ya wilaya na kwamba hilo litafanikiwa.



# HABARI MBEYA

## Kanisa sasa kukemea unyanyasaji

**Na Grace Mwakalinga,** SONGWE

KANISA la Tanzania Assemblies Of God (TAG), limedai kuendelea kushirikiana na serikali kukemea vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia dhidi ya watoto na mimba kwa wanafunzi ili waweze kutimiza ndoto zao za kupata elimu.

Hayo yalibainishwa juzi na Katibu Mkuu wa Kanisa la Tanzania Asemblies of God Tanzania TAG, Dk. Boniphace Mgonja, wakati wa maadhimisho ya Idara ya Watoto na Wanafunzi Tanzania ya Miaka 80 ambayo yalifanyika katika Mjini wa Mlowo Halmashauri ya Mbozi mkoani Songwe.

Dk. Mgonja alisema taasisi za dini ikiwamo TAG zinaunga mkono jitihada za serikali za kupinga vitendo vya unyanyasaji wa kijinsia ikiwamo ubakaji na mimba za utotoni ambazo zimechangia kukwamisha jitihada zao za kutimiza ndoto ya kupata elimu.

Alisema ili kutokomeza vitendo hivyo dhidi ya watoto, taasisi za dini hazinabudi kuongeza nguvu ya kupinga vitendo hivyo kwa kuifanya ajenda kwenye nyumba za Ibada.

"Tunapoadhimisha miaka 80 tangu kuanzishwa Idara ya Watoto na Wanafunzi Tanzania katika kanisa letu... tumeangazia suala la unyanyasaji kwa watoto wa kike na mimba tumebaini vimeshamiri lakini watu ni waoga kuripoti kanisa letu tumejihakikisha kupiga vita masuala hayo na tunaungana na serikali kufichua maovu hayo lakini kutoa elimu kwa jamii kupitia ibada zetu," alisema Dk. Mgonja.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Idara ya Watoto na Wanafunzi TAG, Godwin Mujaki, alisema miongoni mwa ajenda katika kuadhimisha miaka 80 tangu kuanzishwa kwa Idara ya Watoto ni kupaza sauti dhidi ya vitendo vya kikatili vya kijinsia kwa watoto.

Mujaki alisema kanisa lao kupitia Idara ya Watoto wameandaa tamasha lenye lengo la kutoa elimu juu ya athari za vitendo vya ukatili kwa watoto na mimba za utotoni.

Mkuu wa Wilaya ya Mbozi, John Pallingo, alisema miongoni mwa sababu zinazochangia vitendo vya ukatili kwa watoto ni tamaa za wazazi kupata mali.

Alisema baadhi ya wazazi kutokana na tamaa za kumiliki mali hulazimika kuwaozesha watoto wadogo kuolewa ili kupata mali.

Alidai wamekuwa wakiwashughulikia wazazi au walezi wanaobainika kukatisha ndoto za wanafunzi kusoma shule kwa kufunguliwa kesi mahakamani na kwamba jitihada hizo zinaendelea.

# Ujenzi wa rada 4 kuongeza pato la taifa

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

SERIKALI imesema ujenzi wa rada nne za kuongozea ndege ambazo zinajengwa kwenye Uwanja wa Kimataifa wa Kilimanjaro (KIA), Dar es Salaam, Mwanza na Songwe, kuongeza pato la taifa kwa kuwa ndege nyingi zitatumia anga ya Tanzania.

Hayo yalibainishwa na Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Mhandisi Isack Kamwelwe, mkoani Mbeya na kutembelea eneo la Lumbila Kata ya Lwanda mkoani Songwe.

Alisema ujenzi wa rada hizo unagharimu Sh. bilioni 67.2 zikiwa ni fedha za mapato ya ndani na kwamba kukamilika kwa rada hizo kusaidia kupanua wigo wa usafiri wa anga pia ajira kwa Watanzania. "Kasi ya ujenzi wa rada inayoendelea mkoani Mbeya inaridhisha, serikali yenu sikivu pia ipo kwenye mpango mkakati wa kununua ndege za mizigo, hii inatokana na wachumi kujiridhisha na upatikanaji wa mizigo kutoka nje ya nchi," alisema Mhandisi Kamwelwe.

Meneja wa Mradi wa Rada, Christon Mwala, alimwahakikishia Waziri Kamwelwe kuwa ujenzi wa rada utakamilika kwa wakati na kuwa na ubora unaokidhi viwango vya kimataifa.

Aliwataka wananchi wanaozunguka mradi wa ujenzi wa rada kutoa ushirikiano katika kulinda miundombinu na vifaa vya ujenzi ili kuhakikisha fedha zilizotolewa zinaendana na thamani ya rada iliyojengwa.

Wakazi wa Kijiji cha Lumbila waliiomba serikali kupitia mradi huo kunufaika na umeme na maji sambamba na kusaidiwa ujenzi wa vyumba vya madarasa.

Japhet Mwashuya, aliipongeza Serikali kwa ujenzi wa rada mkoani Mbeya, na kwamba kupitia mradi huo, fursa mbalimbali za uchumi zitafunguka ikiwamo biashara.



Mkurugenzi Mkuu wa Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), Dk. Geofrey Mkamilo (wa tatu kushoto), akitoa ufafanuzi kuhusu zao la pilipili hoho kwa Naibu Waziri wa Kilimo, Omary Mgumba (kulia), wakati alipotembelea vipando vya mazao vilivyopo katika Kituo cha Utafiti wa Kilimo cha TARI Ilonga, wilayani Kilosa Mkoa wa Morogoro juzi. **PICHA: ASHTON BALAIGWA**

# Vijana, wanawake wakopeshwa mil. 224/-

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

HALMASHAURI ya Wilaya ya Mbeya imetoa mkopo wa zaidi ya Sh. milioni 224, kwa vikundi 14 vya wanawake na vijana, ukiwa ni utekelezaji wa agizo la serikali linalotaka kila halmashauri kutoa asilimia 10 ya mapato yake ya ndani kwa wananchi.

Wanufaika wengine wa fedha hizo ni waendesha bodaboda na wajasiriamali wadogo maarufu kama 'machinga'.

Akikabidhi hundi ya mfano jana, Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri ya Mbeya, Steven Katemba, alisema mpango huo tayari umewanufaisha waendesha boda boda 46 ambao wamenunua pikipiki.

Alisema kupitia mikopo hiyo, makundi mbalimbali ya watu wenye ulemavu, wanawake na vijana yamenufaika na kuanzisha miradi ya maendeleo kwa ajili ya kujiingizia kipato.

Alisema fedha zinazotolewa na halmashauri hazina masharti magumu ukilinganisha na maeneo mengine, na kukusisitiza kuwa watakaonufaika na mikopo hiyo ni wananchi waliokidhi vigezo ikiwamo kujiunga kwenye vikundi na kusajili kikundi na katiba.


"Agizo la serikali la kutaka kila halmashauri itenge Sh. milioni 10 ya fedha zake za ndani kutoa mikopo kwa makundi ya vijana, wenye ulemavu na wanawake limekuwa msaada mkubwa kwenye jamii, kwani wananchi wametimiza ndoto zao za kumiliki biashara na kufungua ajira kwa vijana, tutaendelea kutekeleza ili kuwasaidia wananchi," alisema Katemba. Ofisa Maendeleo ya Jamii Halmashauri ya Wilaya ya Mbeya, Zena Kapama, aliwataka watendaji kujiridhisha na vikundi vitakavyonufaika na mikopo hiyo.

Alisema uhakiki wa vikundi utasaidia kuepukana udanganyifu na kwamba fedha hizo zina lengo la kumnufaisha kila mwananchi mwenye sifa ya kupata mkopo.

Baadhi ya wanufaika wa fedha hizo walisema zimesaidia kutimiza ndoto zao za kumiliki biashara kubwa. Magdalena Mathayo, alisema mkopo huo umemwezesha kumiliki biashara kubwa ya duka la jumla ambalo linamwingizia fedha nyingi ukilinganisha na awali ambapo alikuwa anafanya biashara ya machinga kutembeza bidhaa.

Anrew Anangisye, alisema mkopo huo umesaidia kubadilisha maisha yake kwa kuwa mpaka sasa amefungua biashara kubwa ambaye inamsaidia kuendesha maisha yake kama vile kusomesha watoto na kuhudumia familia.

Makamu Mwenyekiti wa Halmashauri ya Mbeya, Sarali Kalinga, aliwataka watendaji wanahusika na mikopo kuwatembelea wanufaika ili kuangalia biashara zao, na kutoa ushauri namna ya kuboresha ili kuendana na ushindani kwenye masoko.





# Sekta ardhi yatajwa kuwa kinara rushwa

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Dodoma, imetaja sekta ya ardhi jijini Dodoma kuwa ni kinara wa tuhuma za rushwa kwa asilimia 36.

Akizungumza jana, Mkuu wa Takukuru mkoani humo, Sosthenes Kibwengo, alisema takwimu hizo zimepatikana kutokana na uchunguzi waliofanya katika robo ya pili mwaka huu.

Alisema mbali na sekta hiyo, pia serikali za mitaa ni ya pili kwa tuhuma hizo kwa asilimia 31, wakati polisi ikiwa na asilimia nane, ikifuatiwa na kilimo yenye asilimia sita, huku mahakama na ujenzi kila moja ina asilimia nne.

Pia alisema asilimia 11 zilizosalia zilihusu sekta ya maji, maliasili, afya, madini na ukusanyaji mapato binafsi.

Mkuu huyo alisema kutokana na hali hiyo bado wataendelea na uchunguzi katika sekta hizo ambazo zimetajwa na nyingine ambazo hazitajwa ili kuhakikisha wanatokomeza suala zima la rushwa.

Alisisitiza kuwa wamejipanga kutumia mikusanyiko ya Mwenge wa Uhuru kwa ajili ya kutoa elimu ya kuzuia na kupamba na rushwa katika uchaguzi wa serikali za mitaa lengo ni kuwakumbusha wananchi kuhusiana na elimu hiyo ambayo inamuhusu kila mwananchi.

Kibwengo alisema wameamua kufanya hivyo ili kutaka wananchi wapate elimu hiyo ambayo itawasaidia kuchagua viongozi waadilifu wasiojihusisha na vitendo vya rushwa.

"Tumejipanga kutumia mikusanyiko kwa ajili ya kutoa elimu ya mapambano dhidi ya rushwa, tunaamini itawafikia wengi na itasaidia kupunguza mianya ya rushwa katika taasisi mbalimbali zikiwamo zilizotuhumiwa," alisema Kibwengo.

Kadhalika, alisema watafanya uchambuzi juu ya mifumo ya ukusanyaji wa mapato manunuzi ya umma ikiwamo kukagua miradi mbalimbali hasa katika sekta ya elimu.

Aliwataka wananchi kuendelea kutoa ushirikiano ili kukomesha rushwa kwenye taasisi hizo.

"Rushwa si jukumu la Takukuru pekee, bali ni jukumu la kila mmoja kuhakikisha anaipiga vita kulingana na nafasi aliyokuwa nayo," alisema.

Alisema wakifanya hivyo itakuwa rahisi kudhibiti vitendo vya rushwa katika taasisi mbalimbali ambazo zimekuwa zikilalamikiwa na wananchi.

Hata hivyo aliwataka wananchi kutokuwa waoga kutoa taarifa kwa Takukuru kama wanauhakika wameona kuna viashiria vya rushwa.

# Wafanyabiashara wapewa onyo kali uvamizi maeneo

**Na Peter Mkwavila,** DODOMA

WAFANYABIASHARA wa Jiji la Dodoma, wametakiwa kuacha tabia ya kuvamia maeneo ambayo hayaruhusiwi kufanyia biashara kwa kuwa watakuwa wanavunja sheria na kanuni za jiji hilo.

Onyo hilo lilitolewa na Ofisa Masoko wa Jiji la Dodoma, James Yuna, alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari jijini hapa. Alisema kutokana na jiji hilo kuendelea kukua, wafanyabiashara wengi hasa wadogo wadogo wamekuwa wakichangamkia fursa na kufanya biashara kwenye maeneo ambayo hayaruhusiwi.

Yuna alisema pamoja na kuwapo kwa fursa hizo, wanapaswa kuzingatia sheria na kanuni kuhakikisha wanafanya biashara zao kwenye maeneo rasmi yaliyotengwa.

"Kufanya biashara katika maeneo yasiyo rasmi wanaweza kuhatarisha biashara zao pamoja na wao wenyewe, hivyo ni vema wakafanya biashara hizo kwenye maeneo yaliyotengwa rasmi na kuzingatia vigezo vinavyotolewa na jiji," alisema.

Alisema kuwa Halmashauri ya Jiji maeneo ya kufanya biashara yapo mengi sana ya wazi ndani ya masoko yake, hivyo hakuna haja ya kufanya shughuli zao hizo barabarani na kuhataraisha maisha yao na afya zao. Pamoja na hayo, ofisa huyo aliwataka kuboresha biashara zao ili kukabiliana na soko la ndani na nje ya nchi.

"Wafanyabiashara wahakikishe wanakuwa na bidhaa zenye viwango vinavyokubalika na watumiaji na kuzingatia kanuni na sheria ambazo zinazowataka kufanya shughuli zao kwenye maeneo yaliyo rasmi na kuyatunza," alisema.

Aliwasisitiza kuwa wabunifu ili kuvutia wawekezaji na kupata masoko.



Mkuu wa Kitengo cha Biashara Benki ya NMB, Makao Makuu, Donatus Richard, akitoa mafunzo ya biashara kwenye mkutano wa siku moja wa Klabu ya NMB ya wafanyabiashara Mkoa wa Dodoma juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Mahenge aagiza uchunguzi kuhusu huduma za wazee

**Na Mwandishi wetu,**

DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Binilith Mahenge, ameagiza kufanyika uchunguzi kuhusu malalamiko ya wazee kutopata huduma bora kwenye Hospitali ya Rufani ya Dodoma.

Agizo hilo alilitoa jana jijini hapa, baada ya baadhi ya wazee kulalamika kukosa dawa licha ya kuwa na kadi za Bima ya Afya ya Jamii (CHF) iliyoboreshwa na vitambulisho vya wazee vilivyotolewa na jiji, katika kikao chake na wazee wa Dodoma.

Alisema ufanyike uchunguzi endapo kuna watumishi wanaosababisha wazee hao kukosa huduma muhimu za kiafya.

"Sasa kwa mtu mwenye kitambulisho cha aina hii kwenda kununua dawa, uchunguzi ufanyike, wengine wanasema dawa zingine hazipo hasa za wazee, kwanini hospitali msiwe na utaratibu kuhakikisha dawa za wazee na watoto zinapewa kipaumbele kwenye manunuzi," alisema.


Hata hivyo, Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. James Kiologwe, alikiri kuwapo kwa changamoto kwenye matibabu ya wazee.

"Changamoto iliyopo ni aina ya dawa inayotakiwa kuwapo kwenye kituo fulani, kwa mfano kuna dawa hazitakiwi kuwepo ngazi ya zahanati na vituo vya afya, mahali ambapo wazee huenda kutibiwa kwa mara ya kwanza," alisema.

Awali, wazee hao waliwambia Mkuu wa Mkoa kuna wakati wakifika hospitali na kitambulisho cha wazee wanakataliwa kupewa huduma.

Walisema wamekumbana na changamoto katika dirisha la wazee hasa wakati wa kuchukua dawa ambapo huambiwa hazipo.

"Kule kwenye dirisha la msamaha niliposikilizwa na daktari nikaambiwa nikachukue dawa, kuna dawa zingine nilipewa zingine sikupewa nikaambiwa hazipo," alisema mmoja wa wazee hao.





Mbunge wa Jimbo la Simanjiro, mkoani Manyara, James Ole Millya (kulia), akiwasikiliza wawekezaji raia wa China, waliofika kukagua eneo la uwekezaji wa madini ya ulanga katika Mji mdogo wa Mirerani, juzi. **PICHA: GIFT THADEY**

# Watanzania watumishi wa ndani walia kudhalilishwa

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

CHAMA cha wafanyakazi wa nyumbani, kimeonya kuhusu uwepo wa wimbi kubwa la udhalilishaji wa wafanyakazi wa ndani wanaotumikishwa nje ya nchi.

Aidha, kimesema wengi wao wamekuwa wakifanya kazi kwa muda mrefu bila ya mapumziko na kupata malipo kiduchu.

Mratibu wa chama hicho Fransisca Clement, alisema wafanyakazi hao wanadhalilishwa kingono na waajiri wao au familia ya waajiri ikiwamo kulazimishwa kujamiiana hasa katika nchi za Falme za Kiarabu.

Akizungumnza na Nipashe ofisini kwake Kikwajuni Mjini Zanzibar, alisema kuna wimbi kubwa la udhalilishaji kwa wafanyakazi wa majumbani wanaotoka Zanzibar na kwenda kufanya kazi katika nchi za Falme za Kiarabu na wanapofika huko hulazimishwa ngono, ukahaba na hata kulazimishwa kufungishwa ndoa bila ya ridhaa zao.

Alisema kuanzia mwaka 2018 wameshapokea malalamiko ya udhalilishaji 100 kwa wafanyakazi wa majumbani, 15 yakiwa yanatoka kwa wafanyakazi waliopo nchi za Falme za Kiarabu.

Alisema changamoto kubwa ni kwamba kesi hizo zinashindwa kusonga mbele katika vyombo vya sheria kutokana na wafanyakazi waliodhalilishwa kukataa kutoa ushahidi, aidha kwa kutishiwa na waajiri wao au kuondoka Zanzibar na kurudi makwao Tanzania Bara.

Alieleza kuwa baada ya Shirika la Kazi Duniani (ILO) kusaini mkataba wa kupinga vitendo vya udhalilishaji kwa wafanyakazi wa majumbani imani yake ni kwamba Tanzania nayo itaridhia mkataba huo ambao utapunguza wimbi la vitendo vya udhalilishaji wa kijinsia kwa wafanyakazi wa majumbani.

Akizungumzia kuhusu watoto walio na umri chini ya miaka 18 kutumikishwa katika kazi za majumbani, Zanzibar, alisema wapo watoto wanaotoka Tanzania Bara na kuletwa Zanzibar kwa ajili ya kufanya kazi za majumbani, lakini inakuwa vigumu kuwagundua kwa sababu wapo wanaodanganya.

"Kwa kweli hii ni changamoto kubwa maana utapowafuata watoto hao au waajiri wao kitu kimoja ni kutoa maelezo ya uongo kuwa wao si wafanyakazi bali wanalelewa," alisema mratibu huyo.

Aidha, alisema huwashauri watu wanaowachukua watoto walio chini ya miaka 18 kuwatumikisha kuwapeleka watoto hao katika vyuo vya ufundi ili kupata ujuzi mbalimbali kuliko kuwatumikisha.

Mratibu huyo aliomba serikali kuweka udhibiti katika bandari rasmi na zisizo rasmi ili kuepusha wimbi la watoto wanaoletwa Zanzibar kufanya kazi za ndani.

Havi karibu Waziri wa Kazi, Uwezeshaji Wazee, Wanawake na Watoto, Modelin Castico, alisema kuwa wizara imesharejesha watoto Tanzania Bara ambao waliletwa Zanzibar kwa ajili ya kufanya kazi za ndani.

Kwa upande wake Meneja wa Sera na Utetezi wa Chama cha Wanahabari Wanawake (Tamwa), Ofisi ya Zanzibar, Hawra Shamte, alisema juhudi za pamoja zinahitajika katika kupiga vita vitendo vya udhalilishaji.

Alisema wameshapokea malalamiko ya wanawake kudhalilishwa wakiwamo wafanyakazi wa majumbani kwa kuvunjiwa heshima na utu wao.

# Rais ataka watumishi wa umma wabunifu

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Ali Mohamed Shein, amehimiza ubunifu kwani ni muhimu katika utumishi wa umma na chachu ya kuondoa ufanyajikazi kwa mazoea.

Alisema bila ya kuwa wabunifu Zanzibar inaweza kubaki nyuma katika karne hii ya sayansi na teknolojia. Akifungua kongamano la maadhimisho ya Siku ya Utumishi wa Umma Zanzibar jana, alisema kuwa watumishi wa aina hiyo ni lazima wabadilike ili kwenda na kasi ya kutoa huduma zilizo bora.

"Uongozi wa Ofisi ya Rais na Utumishi wa Umma na Utawala Bora kwa kushirikiana na Chuo cha Utawala wa Umma (IPA) mwandae programu za mafunzo ya muda mfupi kwa ajili ya viongozi, watendaji wakuu na watumishi wengine wa serikali," alisema Dk. Shein. Alieleza kuwa utumishi wa umma ulio bora ni chachu katika kuongeza kasi ya maendeleo kiuchumi na kuimarisha ustawi wa jamii hasa kwa kutambua kuwa utumishi wa umma ni kigezo muhimu cha misingi ya utawala bora.

Dk. Shein aliwataka watumishi wa umma kuendelea kufanya kazi kwa kujiamini kwani wanaweza kutekeleza vyema kazi zao na kusisitiza zaidi ubunifu.

Alieleza haja ya taasisi inayoshughulikia serikali mtandao kuwaelimisha wananchi na watumishi wa umma maana ya serikali mtandao na madhumuni yake kwani unarahisisha utendaji kazi. Rais aliwataka viongozi na watumishi wa umma kufanya kazi kwa ushirikiano huku akieleza kuwa serikali inapiga vita rushwa na uhujumu wa uchumi. Alisema kuwa katika kuendeleza juhudi za kuhakikisha kwamba viongozi wa umma wanashikamana na maadili ya umma sambamba na kuwajibika kwa uwazi na kwa kuzingatia misingi ya sheria, kwa lengo la kutoa huduma bora kwa wananchi. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Utumishi wa Umma na Utawala Bora, Haroun Ali Suleiman, aliahidi kuendelea na jitihada za kuimarisha utumishi wa umma.

Kwa upande wake Naibu Waziri wizara hiyo Tanzania Bara, Mary Mwanjelwa, alitumia fursa hiyo kuipongeza Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa kufanya maadhimisho hayo kwani yana faida nyingi kwa utumishi wa umma.

# Mamlaka yakusanya mamilioni leseni za uvuvi

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

MAMLAKA ya Uvuvi wa Bahari Kuu imekusanya takribani Dola milioni 12.8 mapato yanayotokana na utoaji wa leseni za uvuvi.

Akizungumza na wanahabari katika semina iliyoandaliwa na mamlaka hiyo, kuzungumzia majukumu yake, Mkurugenzi Mkuu, Dk. Islam Seif, alisema fedha hizo zilikusanywa tangu ilipoanzishwa. Alisema uvuvi wa bahari kuu kwa kiasi kikubwa unashughulika na samaki wa jodari na jamii zake ambao wakati mwingine wanatabia ya kuhama kutoka nchi moja kwenda nyingine.

Alisema mamlaka imekamilisha maandalizi ya rasimu ya sera ya uvuvi wa bahari kuu na mikakati ya utekelezaji wake pamoja na kufanya mapitio ya sheria iliyopo yamefanyika pia.

"Rasimu hizo pia zimefanywa tathmini ya mkakati wa kimazingira," alisema Mkurugenzi Seif.

Aidha, alisema ni mategemeo ya mamlaka ni kuwa na sera na sheria mpya zitakazowavutia wawekezaji wazawa na wageni.

Mkuu wa Kitengo cha Leseni kutoka cha taasisi hiyo, Daniel Kawiche, alisema meli 469 zenye uwezo wa kuvua bahari katika ukanda wa bahari kutoka mataifa mbali mbali zimepatiwa leseni za uvuvi huo na mamlaka.

Alieleza kuwa kati ya meli hizo, 269 zinatumia uvivu wa njia za kisasa na 201 zinatumia mishipi (mikanda) iliyoboreshwa kitaalamu zaidi.

Alisema miongoni mwa meli ambazo wamesajili ni kutoka nchini China, Tanzania, Kenya, Ufaransa na Komoro.

Alisema kabla ya meli hizo kupatiwa leseni hizo, mamlaka huzikagua kitaalamu ikiwamo kujua uwezo wa kuvua,vifaa, hatia na uhalifu.

Mkuu wa Udhibiti wa Mamlaka ya Uvuvi wa Bahari Kuu, Christina Mzowa, alisema katika kuhakikisha hakuna meli inayokwenda kinyume na taratibu za bahari kuu, taasisi hiyo inafanya kazi kwa kushirikiana na nchi mbalimbali duniani.

Alisema wakibaini meli ina tatizo au wakiwa na mashaka nayo hufanya mawasiliano na nchi nyingine kujua ukweli wa meli husika.

# Leseni za biashara sasa kimtandao

**Na Yasmine Protace,** MKURANGA

WANANCHI wametakiwa kuhakikisha wanapata vitambulisho vya uraia ili kuwasaidia kurahisisha urasimishaji wa majina ya biashara na kampuni, hali itakayowasaidia kuondokana na usumbufu unaoweza kujitokeza wakati wa usajili.

Hayo yalisemwa na Bakari Mketo, Mkurugenzi wa Utawala na Fedha kutoka Wakala wa Leseni na Biashara (BRELA) wakati akizungumzia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao katika mafunzo yaliyotolewa juzi kwa wafanyabiashara Wilaya ya Mkuranga mkoani Pwani.

Mketo alisema mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao utawasaidia wafanyabiashara kwa kuondoa urasimu kwa wateja na watakuwa wanafanya kazi zao kwa usalama na uaminifu.

"Zamani kabla hatujaanza kutumia mfumo wa usajili kwa njia ya mtandao tulikuwa tukitumia makabrasha kwenda makao makuu, kwa sasa makabrasha hayatotumika watu watatumia kusajili biashara zao kwa njia ya mtandao wakiwa katika maeneo yao mbalimbali ya biashara bila kuingia gharama zozote za kufuata huduma hiyo makao makuu, alisema. Aliongeza kuwa Wilaya ya Mkuranga imekuwa na mwitikio mkubwa wa wafanyabiashara na maofisa biashara ambapo zaidi ya wafanyabiashara 200 wamejitokeza kushiriki mafunzo hayo kwa njia ya mtandao.

Alisema katika usajili lazima vitambulisho vya taifa vinatumika hiyo inasaidia kuondoa kampuni hewa. Mketo alisema kuwa mpaka sasa kampuni 149,926 zimesajiliwa, huku majina ya biashara yaliyosajiliwa ni 456,122.

Alisema kampuni zilizosajiliwa kwa mfumo wa mtandao toka Februari mwaka jana mpaka sasa ni 16,205.

Alisema kwa alama za biashara zilizosajiliwa ni 64,700, huku leseni za viwanda zilizosajiliwa ni 7,130 na leseni za viwanda zilizosajiliwa kwa mfumo ni 182.

Akizungumzia changamoto, alisema kuwa elimu ya mfumo kwa baadhi ya wafanyabiashara wamekuwa na uoga ambapo elimu imeanza kutolewa ili kuwawezesha wafanyabiashara waweze kuitumia na kuwasaidia kufanya mambo yao kwa haraka.



Mkurugenzi Mtendaji wa Benki ya Maendeleo ya Kilimo Tanzania (TADB), Japhet Justine (kulia), akizungumza na baadhi ya wafanyakazi wa kiwanda cha kahawa cha Tanica. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Kagera, Brigedia Jenerali Marco Gaguti, baada ya kutembelea kiwanda hicho mjini Bukoba hivi karibuni. TADB imeahidi kukiongezea nguvu kiwanda hicho ili kiongeze uzalishaji zaidi. **MPIGAPICHA WETU**

# Takukuru Ilala yawaburuza kortini 10 kesi za ufisadi 6 miezi mitatu

**Na Mary Geofrey**

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (Takukuru) Mkoa wa Ilala, jijini Dar es Salaam, imefungua kesi mpya sita mahakamani zinazohusu watuhumiwa 10 wanaojihusisha na rushwa katika kipindi cha miezi mitatu kuanzia Aprili hadi Juni mwaka huu.

Watuhumiwa waliofikishwa mahakamani ni diwani mmoja, watumishi wawili wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), vyombo vya ulinzi viwili, watumishi wawili wa Mamlaka ya Majisafi na Majitaka (Dawasa), mtumishi mmoja wa Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (Tamisemi) na mfanyabiashara mmoja.

Kamanda wa Takukuru, Mkoa wa Ilala, Christopher Myava, alitoa taarifa hiyo jana kwa waaandishi wa habari na kueleza kuwa, wametekeleza jukumu hilo kwa mujibu wa Kifungu cha 7 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya Mwaka 2007.

Aidha, alisema katika kipindi hicho pia Takukuru mkoa huo, waliendelea kufanya uchunguzi wa tuhuma mbalimbali kwa kufungua majalada ya uchunguzi 19, yanayohusu uhujumu uchumi, ukwepaji kodi, hongo, ubadhirifu wa mali ya umma na ujenzi wa miradi ya maendeleo chini ya kiwango. "Uchunguzi wa majalada haya upo katika hatua mbalimbali. Katikakipindi hiki, pamoja na utekelezaji wa majukumu yetu ya uchunguzi, utafiti pamoja na uelimishaji umma," alisema Myava.

Alisema pia walifanya ufuatiliaji wa kukagua miradi ya maendeleo na walifanikiwa kukagua miradi yenye thamani ya zaidi ya Sh. bilioni 38 inayoendelea katika Mkoa wa Ilala. Alisema na kupitia ukaguzi huo walijiridhisha iwapo kuna thamani ya fedha katika utekelezaji wa miradi hiyo ili kudhibiti matumizi mabaya ya fedha za serikali zinazotolewa kutekeleza miradi hiyo.

Alitaja miradi waliyofuatilia ni ya ujenzi wa barabara zilizoko maeneo yasiyopimwa katika Kata ya Ukonga na mradi wa ujenzi wa barabara zilizoko maeneo yasiyopimwa katika kata ya Kiwalani.

"Katika ufuatiliaji huu, ilibainika kuwa kulikuwa na upungufu katika utoaji wa malipo ambapo baadhi ya kazi mathalani uwekaji wa zege la lami, zililipwa tofauti na ilivyoidhinishwa katika mkataba," alisema. Alieleza kuwa walibaini kuwa mkandarasi alilipwa takribani Sh. bilioni 1.477 zaidi ya fedha zilizotakiwa alipwe katika ujenzi wa barabara za Kiwalani.

Pia alisema zipo barabara zilionekana kuwa na urefu mfupi tofauti na ilivyokuwa kwenye mkataba.

## DC asaidia wanahabari

**Na Boniface Gideon,** TANGA

MKUU wa Wilaya ya Tanga, Thobias Mwilapwa, ametoa msaada wa shilingi milioni moja katika ofisi ya Klabu ya Waandishi wa Habari mkoani Tanga (TPC), kama sehemu ya kuunga mkono jitihada zinazofanywa na waandishi wa habari mkoani hapa.

Akikabidhi fedha hizo kwa mwenyekiti wa klabu hiyo, alisema ameguswa na kazi nzuri inayofanywa na waandishi wa habari wa Mkoa wa Tanga katika kuhakikisha wanaandika habari za uchunguzi na zenye kuuletea mkoa maendeleo.

Mwilapwa ambaye pia ni mwanahabari kitaaluma, alisema ataendelea kuwapa ushirikiano waandishi wa habari katika masuala ya nyanja mbalimbali na kuwaasa kuendelea kuandika habari zenye kuzingatia weledi na maadili.

Meya wa Jiji la Tanga, Alhaji Mustafa Selebos, alisema kama watatumia kalamu zao vyema na kufikisha habari za maendeleo katika utekelezaji wa ilani ya chama hicho, chini ya Rais Magufuli anaamini wananchi watazipata vyema habari hizo.

"Habari zozote mnazoziona kwa viongozi mnapaswa kuziandika, kwani kiongozi ni kioo cha jamii... anatakiwa awe mfano bora wa kuigwa," alisema na kuongeza:

"DC (Mwilapwa) leo ni mfano mwema kuonyesha wana-Tanga wana kila sababu ya kumuunga mkono katika hili ili kuwasaidia wanahabari kuwa na vitendea kazi vya kisasa na ofisi bora."

Alisema kwa hicho kidogo DC alichokitoa kinapaswa kuwa chachu ya maendeleo kwa wengine na kumuomba mwenyekiti wa klabu hiyo kutumia vyema msaada huo kwa kazi iliyokusudiwa, kwani lengo lao ni kuona wanahabari wa Tanga hawawi ombaomba.

Kwa upande wake Mwenyekiti wa Klabu hiyo, Hassan Hashim, alishukuru kwa msaada huo na kuahidi kuzitumia vyema fedha hizo kama zilivyokusudiwa ili kukuza tasnia hiyo.

Alitumia nafasi hiyo kuwaomba viongozi hao kuingilia kati mgogoro wa kiwanja cha klabu hiyo kinachotarajiwa kujengwa ofisi za zake kilichoko eneo la Mwakidila ili shughuli za ujenzi ziweze kuanza mara moja.

Hashimu alisema ataendelea kusimamia vyema tasnia hiyo na kuhakikisha waandishi wanaandika habari zenye kufuata maadili na weledi.

# Mke wa mtawala wa Dubai akimbilia mafichoni

**DUBAI,** Falme za Kiarabu

MKE wa mtawala wa Dubai, Sheikh Mohammed Al Maktoum, Haya Bint al- Hussein, yuko mafichoni jijini London Uingereza akidaiwa kuhofia usalama wa maisha yake baada ya kumtoroka mumewe.

Sheikh Mohammed (69) ambaye ni bilionea aliandika uteuzi wenye hisia za hasira kwenye ukurasa wake wa Instagram akimshutumu mwanamke ambaye hakufahamika kwa vitendo vya udanganyifu na usaliti.

Mke wa kiongozi huyo mzaliwa Jordan (45), aliolewa na Sheikh Mohammed mwaka 2004 na kuwa mke wa sita kama mke mdogo.

Sheikh Mohammed ana watoto 23 kutoka kwa wake zake. Haya alikimbilia Ujerumani mwaka huu kutafuta hifadhi.

Hivi sasa Haya anadaiwa kuishi kwenye nyumba ya thamani ya pauni milioni 85 Kensington Palace Gardens, katikati mwa Jiji la London, akijiandaa kufungua mashtaka kwenye mahakama ya juu.

Vyanzo vya karibu vinaeleza kuwa, Haya hivi karibuni alibaini ukweli ambao ulimshitua kuhusu kurejea kwa Sheikha Latifa mjini Dubai mwaka jana, mmoja wa mabinti wa mtawala huyo.

Inaelezwa kuwa Haya alitoroka Jumuiya ya falme za kiarabu kwa njia ya baharini akisaidiwa na mwanaume mmoja mfaransa lakini alinaswa na watu wenye silaha kwenye pwani ya India na akarudishwa Dubai.

Mamlaka za Dubai zimesema kuwa Sheikha Latifa alikuwa akipitia vitendo vya unyanyasaji na alikuwa salama Dubai

Lakini mawakili wa watetezi wa haki za binaadamu walisema alichukuliwa kwa nguvu.

Tangu wakati huo inadaiwa kuwa Haya alijua ukweli kuhusu tukio hilo na kwa sababu hiyo hakuwa na mahusiano mazuri na familia ya mumewe na alikuwa akifanyiwa visa hadi alipoona kuwa hayuko salama tena.

Chanzo kilicho karibu naye kimesema kuwa Haya anahofu kuwa na yeye huenda atachukuliwa kwa nguvu na kurejeshwa Dubai.

Ubalozi wa Jumuia ya falme za kiarabu jijini London umekataa kutoa kauli yoyote kuhusu suala hilo walilosema kuwa ni masuala binafsi baina ya watu hao wawili.

Haya, ambaye alipata elimu yake nchini Uingereza, na kusoma chuo cha Oxford nchini humo amepanga kuishi Uingereza. **BBC**

# Akamatwa akipanga njama za kumuua Makamu Rais

**NAIROBI,** Kenya

ALIYEKUWA Mkurugenzi wa mawasiliano ya kidijitali katika Ikulu ya Kenya, Denis Itumbi anashikiliwa na Jeshi la Polisi kuhusu barua ya njama ya kumuua Makamu Rais wa nchi hiyo, Willium Ruto.

Itumbi alikamatwa jana na wapelelezi wanaochunguza tuhuma za njama ya kumuua Makamu wa Rais, William Ruto.

Gazeti la The Standard nchini humo limeeleza kuwa Itumbi anashikiliwa katika makao makuu ya Idara ya Upelelezi mjini Nairobi, linaripoti gazeti la The Standard.

Itumbi amekamatwa ikiwa zimepita siku kadhaa baada ya kuwapo kwa taarifa kuwa chanzo cha barua hiyo ghushi kimetambulika, barua iliyozusha tuhuma za kutaka kuuawa Ruto.

**Wiki iliyopita, mawaziri kadhaa nchini Kenya walituhumiwa kupanga njama za kumuua Ruto, hali iliyosababisha upelelezi kuanza ili kuwabaini wahusika.**

Wiki iliyopita, mawaziri kadhaa nchini Kenya walituhumiwa kupanga njama za kumuua Ruto, hali iliyosababisha upelelezi kuanza ili kuwabaini wahusika.

Waziri wa Biashara wa Kenya, Peter Munya alikana shutuma za kupanga mauaji ya Ruto, vyombo vya habari nchini humo vimeripoti.

Waziri Munya alikuwa akizungumza nje ya Makao Makuu ya ofisi ya Mkurugenzi wa uchunguzi wa makosa ya jinai (DCI) ambako aliitwa sambamba na mawaziri wengine, akihojiwa kuhusu shutuma kuwa walimtishia Ruto.

Mawaziri hao wameshutumiwa kufanya vikao vya siri, lakini Munya aliwaambia waandishi wa habari kuwa hawajapeleka taarifa polisi kwa kuwa Ruto hajapeleka malalamiko rasmi.

Gazeti la Daily Nation la Kenya lilimnukuu Waziri Munya akisema kuwa Ruto alidai kuwa mawaziri hao walikuwa wakifanya vikao vya siri na maafisa wengine. Ruto ana mipango ya kuwania urais mwaka 2022. **BBC**




Wakimbizi kutoka Congo wakiwa mpakani wakivuka kuingia Uganda kukwepa vurugu za kikabila. **PICHA: REUTERS**

# Wacongo 8,000 wakimbilia Uganda

**KINSHASA,** Congo

MAELFU ya wakimbizi kutoka Jamhuri ya Kidemocrasia ya Congo (DRC) wanavuka ziwa Albert kwa boti na kuingia Uganda kukwepa vurugu za kikabila.

Ongezeko hilo la idadi ya wakimbizi wanaoingia Uganda kutoka DRC katika kipindi cha mwezi mmoja uliopita, limesababisha mashaka kuhusiana na shughuli za kuwahudumia.

Mashirika ya huduma kwa wakimbizi pamoja na serikali ya Uganda wanaelezea kwamba ikiwa mwenendo huu utaendelea bila wahisani kutoa misaada, Uganda hawataweza kukidhi mahitaji ya wakimbizi hao.

"Wakimbizi zaidi wanawasili Uganda kutoka DR Congo, na mwisho wa hali hii haujulikani. Hili limesababisha uhaba wa msaada wa dharura, suala linalotishia afya na maisha ya wakimbizi," alisema Kaimu Mkurugenzi Mkaazi wa Baraza la Wakimbizi la Noeway (NRC), Melchizedeck Malile.

Kulingana na takwimu za baraza hilo, idadi ya wakimbizi waliovuka mpaka kutoka DRC na kuingia Uganda mwezi wa Juni imeongezeka kutokana na ghasia za kikabila pamoja na ugonjwa wa Ebola.

Katika taarifa yake ya kila mwezi, Baraza la Norway la wakimbizi linakadiria kuwa zaidi ya wakimbizi 3,000 walivuka mpaka kwa mitumbwi kutoka Congo katika kipindi cha mwezi mmoja.

Taarifa zaidi zinaeleza kuwa vituo vya kupokelea wakimbizi nchini Uganda vinaelemewa kutokana na wimbi hili jipya. Katika mwezi uliopita wastani wa idadi ya kila siku ulikuwa wakimbizi 145 kwa siku.

Tangu wakati huo, idadi ya wakimbizi wanaowasili imeongezeka maradufu hadi kufikia 302 kwa siku.

"Kwa ogezeko hili jipya la wakimbizi wanaowasili, tunayasihi mashirika ya hisani ya kimataifa na jumuiya ya kimataifa kuongeza msaada kwa wakimbizi nchini Uganda. Wakimbizi wanaowasili wanahitaji msaada wa haraka wa malazi, maji safi na huduma za usafi. Tukiwa na ufadhili zaidi, tutaweza kuokoa maisha zaidi," alisema Malile.

Mpango wa wakimbizi wa mwaka 2019 kwa ajili ya Uganda unaomba kiasi cha dola bilioni 1.03 katika msaada wa kusaidia watu, lakini ni dola milioni 147 tu zilizotolewa mpaka sasa.

Nakisi za nyuma katika ufadhili zimesababisha kufungwa kwa programu za kuokoa maisha.

Uganda, taifa ambalo ni dogo lisilo na njia ya bahari linahifadhi wakimbizi wapatao milioni 1.3 kwa sasa, wengi wao kutoka Sudan Kusini, DRC na Burundi. **DW**

# Baba matatani tuhuma kuunguza mke, mtoto

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JESHI la Polisi mkoani Dodoma, linamshikilia mkazi wa kijiji cha Mlazo, Elias Warioba kwa tuhuma za kumjeruhi kwa moto mkewe, Mkami Mbarahi (19) akiwa na mwanaye wenye umri wa miezi mitatu mgongoni.

Kamanda wa Polisi mkoani Dodoma, Gilles Muroto alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kusema mtuhumiwa anashikiliwa na polisi kwa mahojiano zaidi.

"Tunamshikilia, njoo kesho nitazungumza na waandishi wa habari," alisema Muroto.

Nipashe, ilifika katika Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma na kumkuta mama huyo na mwanaye wakiwa wamelazwa wodi 16, kwa kujeruhiwa vibaya na moto baada ya mumewe kudaiwa kumpiga na chupa yenye mafuta ya petroli kichwani, huku akiwa anapika.

Mkami alisema akiwa jikoni akiandaa chakula cha usiku huku akiwa amembeba mwanaye mgongoni alifika mume wake aliyekuwa amebeba chupa ya plastiki ikiwa na mafuta ya petroli ambayo hutumika kwenye pikipiki.

"Alipofika aliniuliza kwa nini ninapikia kuni na kuhoji je, nikiunguza kibanda cha watu?nilimjibu kwani mimi sina akili mpaka niunguze," alisema.

Alieleza kuwa baada ya majibu hayo mumewe alimrushia chupa yenye mafuta kichwani ambayo ilimwagikia mafuta yeye na mwanaye na moto ukawalipukia.

Mama huyo alisema baada ya hali hiyo alianza kukimbia akipiga kelele kuomba msaada kwa majirani, huku mumewe akiondoka bila kutoa msaada wowote kwao.

"Nimeungua maeneo ya kichwa hadi kifuani na mwanangu ameungua maeneo ya usoni, mikononi, tumboni na miguuni," alisema.

Alipoulizwa kama walikuwa na ugomvi wowote, mama huyo alisema hawakuwa na ugomvi wowote kwa siku hiyo, isipokuwa siyo la mara ya kwanza kumfanyia vitendo vya kikatili.

"Nina miaka sita sasa mume wangu amekuwa akinipiga mara kwa mara," alisema.

Mganga wa Hospitali hiyo, Dk. Ernest Ibenzi alithibitisha kuwapo kwa majeruhi huyo wa moto na mwanaye ambao wamelazwa wodi namba 16, na kueleza kuwa wanaendelea vizuri.

Naye, Dk. Hindi Mastai alisema majeruhi hao walipokelewa Juni 28, mwaka huu wakiwa na hali mbaya.

Hata hivyo, alisema mtoto kwa sasa hawezi kunyonya maziwa ya mama yake kutokana na hali aliyonayo. "Tunampa maziwa ya kopo ili aendelee kuishi," alisema.



Makamu wa Rais, Samia Suluhu Hassan (wa tatu kulia), akisikiliza maelezo ya bidhaa zinazotengenezwa na mmoja wa wajasiriamali wakati akitembelea banda la Benki ya NBC katika Maonyesho ya 43 ya Kimataifa ya Biashara ya Dar es Salaam katika Viwanja vya Sabasaba yaliyofunguliwa rasmi jijini Dar es Salaam juzi. Kulia kwake ni Mkurugenzi Mtendaji wa benki hiyo, Theobald Sabi na Waziri wa Viwanda na Biashara, Innocent Bashungwa. NBC ilitwaa tuzo ya mshindi wa kwanza ya mwoneshaji bora katika kundi la Taasisi za Fedha. **NA MPIGAPICHA WETU**

# Neema Shinyanga ujio bomba la mafuta

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WANANCHI mkoani Shinyanga wameaswa kutumia vyema fursa ya kuanza kwa mradi mkubwa wa ujenzi wa bomba la mafuta kutoka Hoima nchini Uganda kwenda mkoani Tanga ambalo litapita mkoani hapa kwa kufanya shughuli mbalimbali za kiuchumi zitakazowaingizia kipato.

Waziri wa Nchi Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Bunge, Kazi, Vijana, Ajira na Watu wenye Ulemavu, Jenista Mhagama, alisema hayo jana mjini hapa alipokuwa akifungua warsha ya siku mbili ya majadiliano ya wadau kuhusu ushiriki wa Watanzania katika sekta ya uzinduaji wa ujenzi wa bomba hilo la mafuta.

Mhagama alisema mradi wa bomba la mafuta ghafi (Eacop) kutoka Uganda ni moja ya miradi mikubwa ambao una manufaa mengi kwa Tanzania katika kuzalisha ajira na kuendeleza urithishaji wa ujuzi wa teknolojia.

"Natoa wito kwa Watanzania hasa wakazi wa maeneo ambayo bomba hili litapita kuhakikisha wanashiriki ipasavyo kwenye shughuli za kuwaingizia kipato, kama ilivyo katika miradi ya sekta za ujenzi na madini. Bomba hili lina urefu wa kilometa 1,443 kati ya hizo kilometa 296 ziko Uganda na 1,147 zipo Tanzania," alisema Mhagama.

"Mikoa ambayo itapitiwa na bomba hili ni Kagera, Geita, Shinyanga, Tabora, Singida, Dodoma, Manyara na Tanga. Wananchi mnatakiwa kuchangamkia fursa hiyo ikiwamo kufanya biashara mbalimbali na kuomba ajira," aliongeza.

Naye Mkuu wa Mkoa wa Shinyanga, Zainab Telack, aliwashukuru waandaaji wa warsha hiyo kwa kuamua ifanyike mkoani hapa na kwamba elimu itakayotolewa itawafumbua macho wafanyabiashara na wananchi wengine wanaoishi eneo ambalo bomba hilo litapita na kujipatia kipato.

Mwenyekiti wa Bodi ya Hakirasilimali, Donald Kasongi, alisema ni muhimu kwa Watanzania kuanza kujenga utayari wa kufanya shughuli mbalimbali na kuinuka kiuchumi, kutokana na ujio wa mradi mkubwa wa bomba hilo la mafuta kutoka Uganda.

# Waziri asisitiza gesi matumizi ya kupikia

**Na Enock Charles**

WATANZANIA wametakiwa kuchangamkia fursa za matumizi ya gesi ya mafuta (LPG) kama nishati mbadala ya mkaa na kuni ambazo zimedaiwa kuwa si rafiki wa mazingira.

Waziri wa Nishati, Dk. Medard Kalemani, aliyasema hayo jana jijini Dar es Salaam wakati akifungua Mkutano wa Kimataifa wa Matumizi ya Gesi ya Mafuta. Alisema matumizi ya gesi yatapunguza athari za mazingira kwa kuwa ni teknolojia rafiki kwa mazingira.

"Mkutano huu unalenga kuhamasisha uwekezaji katika gesi ya LPG katika matumizi ya ndani na katika magari," alisema Kalemani.

Aidha, Dk. Kalemani aliwataka wawekezaji wa gesi nchini kupeleka nishati hiyo vijijini kwa kuwa matumizi yake yatapunguza ukataji wa miti. Pia aliwataka wawekezaji hao kujenga viwanda kwa ajili ya kupata vifaa muhimu ikiwamo mitungi ya gesi badala ya kuagiza vifaa hivyo kutoka nje kwa gharama kubwa.

Kuhusu matumizi ya gesi hiyo katika vyombo vya usafiri, Waziri Kalemani alisema Tanzania imeanzisha vituo maalum kwa ajili ya magari yenye mfumo wa matumizi ya gesi katika Chuo cha Taifa cha Usafirishaji (NIT) na Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (UDSM).

"Tanzania tumeanza kusambaza gesi majumbani, lakini hata katika magari kwa Dar es Salaam tuna kituo pale DIT (Taasisi ya Teknolojia Dar es Salaam) pale Chuo cha Usafirishaji lakini pia pale Chuo Kikuu Dar es Salaam. Vile vituo tumeviweka mahsusi kwa ajili ya magari yenye mfumo wa kutumia gesi kubadilishwa kutoka kwenye mfumo wa petroli," alisema.

Waziri Kalemani alisema serikali ina mpango wa kuweka vituo vingine sita miaka miwili ijayo katika mikoa ya Mwanza, Arusha, Dodoma, Mbeya ambavyo vitakuwa tembezi na kutakuwa na matangi makubwa.

Mmoja wa washiriki wa kongamano hilo kutoka Kenya, Elizabeth Muchiri, alisema ni muhimu wadau wa mazingira na elimu kuhamasisha matumizi ya nishati ya gesi ili kuondokana na athari zilizopo za matumizi ya kuni na mkaa hasa kwa vijana na wanawake.

## TANGAZO

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

### ELIMU/ MASOMO

**NAFASI ZA MASOMO,** Chuo cha Uuguzi na Ukunga MASSANA kilichopo dar es Salaam, Mbezi Beach Goba Road. Kinatangaza nafasi za masomo kwa ngazi ya Diploma na cheti yatakayoanza mwezi wa September 2019. Njoo tukujazie Form Kupitia Mtandao wa Nacte: 0713 321260/0769 666880

### NAFASI ZA KAZI

**TANGAZO LA KAZI,** Wanahitajika IT – Diploma, Sales Lady, Messenger – awe mvulana. Elimu kidato cha nne/cha sita. Wawe wazoefu wa kutosha. Mawasiliano: 0715 885533. Email: jmtofficetraders96@gmail.com au jmtofficetraders@gmail.com.

### MCHANGANYIKO

**TOVUTI YA HADITHI ZETU,** www.hadithizetu.co.tz ni tovuti inayokuwezesha kusoma hadithi nzuri kutoka kwa waandishi mbalimbali, karibu uburudike. Mawasiliano: 0762 489789.


**NIPASHE NI JIBU LAKO**

**NJOO UTANGAZE NASI**

**BIDHAA YAKO KWA BEI NAFUU SANA**



### KUPOTEA KWA CHETI



**Pauline Saimon Kaseba** anatangaza kupotelewa na result yenye **index namba S.5121/0034** iliyotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2018 katika shule ya Sekondari Hope nad Joy. Yeyote atakaekiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **OB/RB/96688/2019**

115305302

### PASSPORT IMEPOTEA




Anaitwa **ADAM MOHAMED ADAM** amepotelewa na paspot ya kusafiria yenye namba **AB114749.**

Yeyote atakaeiona anaombwa atoe taarifa katika kituo chochote cha polisi,Taarifa ya polisi; **MOR/MOR/RB/100317/2019.**

115306302

### KUPOTEA KWA VYETI



**Llilian Mushobozi** anatangaza kupotea kwa vyeti vifuatavyo cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S0428-0016** kilichotolewa na Baraza la mithihani la taifa mwaka 1998 katika shule ya Sekondari Mpechi, Cheti kingine cha kidato cha nne chenye **index namba P0386-0031** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2007 katika shule ya Sekondari Geita na cheti cha kidato cha sita chenye index namba **P0321-0546** kilichotolewa na Baraza la Mithihani la Taifa mwaka 2009 katika shule ya Sekondari Kinondoni . Yeyote atakaeviona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi Taarifa: **PWA/BAG/RB/102109/2019**

115307402


### KUPOTEA KWA CHETI



**MARTHA BENARD BURTON** ANATANGAZA KUPOTELEWA NA CHETI CHA KIDATO CHA NNE CHENYE **INDEX NAMBA S0748/0043** KILICHOTOLEWA NA BARAZA LA MITIHANI MWAKA 2016 KATIKA SHULE YA SEKONDARI KAWAWA JKT.YEYOTE ATAKAYEKIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI KILICHO KARIBU.TAARIFA YA POLISI **MBE/RB/89460/2019.**

115307802

### KUPOTELEWA NA RESULT SLIP



**HUSNA SOLA** anatangaza kupotelewa na Result Slip ya kidato cha nne yenye **index namba S.2153/31** iliyotolewa na **AQUINAS SEKONDARI** mwaka 2018. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **MBW/RB/8112/2019.**

115307902

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika mahakama ya mwanzo: MJINI MOROGORO**

**Usimamizi wa mirathi No;141/2019**

**Ombi la RASHID HAMSINI MGAZA Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu HAMSINI MGAZA MADENGE**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 10/07/2019 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia ya marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 02/07/2019.

115306402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA WILAYA YA ILALA**

**USIMAMIZI WA FOMU NA II**

**SHAURI LA MIRATHI NO. 33 2018**

**JINA LA MWOMBAJI ..........HOPE DAUDI ALIBALIO**
**JINA LA MAREHEMU .........DAUDI NTEGEIZE ALIBALIO**

TANGAZO linatolewa kwa watu /mtu yoyote wanaodai kuwa na uhusiano na marehemu na wanataka kupinga uteuzi wa Mwombaji kuteuliwa kusimamia Mirathi ya Marehemu DAUDI NTEGEIZA ALIBALIO kuja na kuhudhuria Mahakamani tarehe 18 Julai 2019 saa 3.00 asubuhi.

Endapo hakuna atakayefika Mahakama hii itamteua muombaji kuwa msimamizi wa Mirathi tajwa.

Hati hii imetolewa na mimi leo tarehe 02 Julai, 2019.

115306102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI 2)**
**Katika Mahakama ya mwanzo MJINI -TANGA**

**Usimamizi wa Mirathi NAMBA 97/2019**

**Ombi la SHEKHA SEIF MBAROUK kuteuliwa Msimamizi wa mirathi marehemu AHMED ISSA ALLY**

**Kwa YEYOTE ANAYEHUSIKA**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 22/7/2019 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.

Wosia wa marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 02/7/2019

HAKIMU
MAHAKAMA YA MWANZO
MJINI TANGA

215307302

---

**FORM II**

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**

**MAHAKAMA YA MWANZO KAWE**

**USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M. 1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**

**Katika Mahakama ya Mwanzo: KAWE**

**Usimamizi wa Mirathi No. 108/2019**

**Ombi la JOSHUA ROBERT OGUDA kuteuliwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu HERIETH AMEDEUS RINGIA**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja na kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 15/07/2019.

kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo ya **HERIETH AMEDEUS RINGIA.**

Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe ...............................................................

115304902

---

### HATI YA KIAPO

**CHA KUKIRI KUPOTELEWA NA OFFER YENYE USAJILI WA PLOT NO. 228 KITALU "R' MABAWA YENYE JINA LA RUKIA S/O SAIDI:**

Mimi **OMARI RAMADHANI SHEKIHIYO** wa S.L.P 178, Tanga, Muislam, mtu mzima na mwenye akili zangu timamu, Nathibitisha katika kiapo changu hichi na kuyatamka haya yafuatayo na kama ifuatavyo:-

Kwamba ndiye mmiliki halali kwa sasa wa Kiwanja Na. 228 Kitalu **"R"** Kilichoko katika eneo la Mabawa, Kata ya Mabawa, Tanga Mjini, (Kupitia Mikataba husika).

Kwamba nimejaribu kuitafuta kwa juhudi zangu zote sikufanikiwa, Nimetoa taarifa Polisi na kupatiwa **TAN/RB/3916/2019 ya tarehe 13/05/2019.**

Kwamba Naiomba Ofisi ya Mipango Miji Mkoa wa Tanga itambue upotevu huu na ninathibitisha imepotea mikononi mwangu mimi muapaji, na niko tayari kulipia gharama na kodi zote husika za serikali.

115306502

---

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**VALENCE JOHN MTONGOLE** Anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba **T. 951 BZF** aina ya **TOYOTA HARRIER** yenye Chassis namba **SXU10-0009666.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo cha polisi kilichopo karibu yake. Taarifa ya Polisi **MZ /TR/RB/ 475 /2019.**

115308202

### KUPOTELEWA NA KADI YA PIKIPIKI.

**VENANCE ANTHON CHILANGAZI.** anatangaza kupotelewa na kadi ya pikipiki aina ya **HONDA** yenye namba za usajili **MC 614 AHE.** Chassis namba **LALPCJ0D4D3142955.** Engine namba. **SDH152FMI3D3325663.**Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **RB/DOM/TR/2350/2019.**

115308402

### KUPOTEA KWA KADI

**Francis Joseph Assenga** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye usajili wa namba **T351 ADS aina MARK II GX81.** Yenye chasis namba **GX8163888880.** Yeyote atakaeiona atoe taarifa kituo chochote cha Polisi. Polisi taarifa: **DAR/OST/RB/97714/2019**

115305202

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**PAULO CONSTATINE TEMBA** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari aina ya **TOYOTA LANDCRUISER PRADO** yenye namba za usajili **T 448** ARB. Chassis namba **KZJ950140143.** Engine namba **1KZ0706896.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **DAR/BUG/RB/98063/2019.**

115306202

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**BAHATI BONIPHACE KAZUZU** anatangaza kupotelewa na kadi ya gari yenye namba za usajili **T 262 DMD TOYOTA RAUM.** Kadi ya gari yenye namba za usajili **T 873 DCQ TOYOTA** PRADO. Yeyote atakayeziona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya polisi: **KMR/RB/6847/2019.**

115305902


**Uza, Chenye Thamani Kubwa Kwa Kutangaza Nasi**

**Kwa Bei Poa Tupigie 0767 223311**

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI MICHEZO

# GUARDIOLA KURUDI BARCA



**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola, amesema kuwa bado ana mpango wa kurudi Barcelona siku moja.

Kocha huyo mwenye miaka 48, ambaye aliiongoza Man City kupata mataji matatu msimu uliopita, amekuwa pale Etihad kwa miaka mitatu sasa.

Kocha huyo mzaliwa wa Katalunya, ambaye pia ametwaa ubingwa wa Ligi Kuu England mara mbili, ataingia msimu wa tatu akiwa na Man City na amebakiza miaka miwili katika mkataba wake.

Guardiola aliweka wazi kwamba anaweza kuongeza mkataba, lakini sasa ameibuka tena na kutamka, anatamani kurudi kwao na kuifundisha Barcelona kwa mara nyingine.

Siku za karibuni alitamka; "Nitakaa Man City kwa miaka miwili zaidi kama wananihitaji. Ninafurahia maisha hapa."

Hata hivyo, ameibuka upya na kutamka; "Nitarudi Barcelona hivi karibuni. Nimeshatembea klabu nyingine, nimefanya vizuri, nadhani bado ninahitajika Barcelona. Nitarudi huko."

## De Gea aitesa Man Utd



**MANCHESTER,** England

KLABU ya Manchester United imeongeza ofa kwa golikipa wake, David De Gea ili kumshawishi kuongeza mkataba ndani ya kikosi hicho kwa mujibu wa ESPN FC.

Kipa huyo ambaye kwa sasa yupo kwenye mwaka wake wa mwisho wa mkataba wake, tayari alishakataa kusaini mkataba mpya ambao ungemuwezesha kulipwa kiasi cha pauni 350,000 kwa wiki.

Chanzo kutoka ndani ya Man United kimeidokeza ESPN FC kwamba United wanafanya kila njia kuhakikisha kwamba wanambakiza De Gea ili kuendelea kukaa na miamba hao.

Kwa mujibu wa chanzo hicho, bado De Gea hajafikia makubaliano na kusaini mkataba huo na kwamba, yeye mpango wake ni kutaka kuondoka.

Licha ya United kuendelea kumshawishi De Gea kubakia hapo, lakini pia inawafuatilia kwa karibu, kipa wa Atletico Madrid, Jan Oblak, Gianluigi Donnarumma wa AC Milan na Andre Onana wa Ajax.



## *Real kumgeuza Bale chambo kwa Pogba*

**MADRID,** Hispania

KLABU ya Real Madrid bado inaendelea na mpango wake wa kutaka saini ya kiungo wa Manchester United, Paul Pogba kipindi hiki cha majira ya joto, huku Gareth Bale akitajwa kuwa chambo.

Bale, mshindi mara nne wa Ligi ya Mabingwa Ulaya, hayupo kwenye mipango ya kocha Zinedine Zidane pale Bernabeu msimu huu, na hivyo wanataka kumtumia kuwa chambo ya kupelekwa pale Old Trafford ili kumpata Pogba.

Kwa mujibu wa Gazeti la Marca, Real wapo tayari kumfanya Bale kama kiungo muhimu kwa kubadilishana na Pogba pamoja na fedha. Taarifa zaidi zinaeleza kuwa, wakala Mino Raiola amesafiri kwenda jijini Manchester mara mbili ili kuhakikisha kwamba, Pogba anatua pale Madrid.

Tatizo kubwa la Bale ni kuacha mshahara anaolipwa pale Real Madrid kuwa inaonekana itakuwa kikwazo kikubwa cha yeye kutua Man United.

Taarifa zaidi zinasema kwamba, Bale mwenyewe ameshaweka msimamo wa kutotaka kuondoka Real Madrid.

Mara baada ya kutua kwa Zidane pale Madrid kwa mara ya pili na Bale kuambiwa wazi kuwa hana nafasi kwenye kikosi chake, mchezaji huyo wa kimataifa wa Wales alibainisha wazi kwamba hana mpango wa kuondoka.

Hiyo inamaana kwamba, Bale anataka kumaliza mkataba wake na miamba hao wa Uwanja wa Santiago Barnabeu ili aondoke akiwa huru na kuchagua wapi pa kwenda.

Zidane ameshatamka wazi kuwa Bale hayupo katika mipango yake kwenye kikosi hicho na hivyo ana nafasi ya kuondoka.

# Arsenal yajipanga kumnasa Fekir

**LONDON,** England

KLABU ya Arsenal imeripotiwa kwamba imewasiliana na Nabil Fekir kwa ajili ya kumsainisha mkataba kipindi hiki cha majira ya joto.

Fekir amekuwa akitajwa kutua kwenye Ligi Kuu ya England tangu kipindi cha majira ya joto kilichopita, kwani dili lake la pauni milioni 53 kutua pale Liverpool lilishindikana msimu uliopita.

Kwa mujibu wa Gazeti la L'Equipe, 'Washika Bunduki' hao wamejitosa kuitaka sahihi ya mshindi huyo wa Kombe la Dunia akiwa na Ufaransa ili waweze kumtoa kiungo wao, Mesut Ozil.

Ozil amekuwa akionekana ni 'mzigo' pale kwenye Uwanja wa Emirates hasa kutokana na mshahara wake wa pauni 350,000 kwa wiki na kocha, Unai Emery amekua akihaha kutaka kumuuza.

Arsenal wanataka kumtumia Ozili ili kupata fedha za usajili wa kipindi hiki kutokana na bajeti yao ya usajili kuwa ndogo.

Hadi sasa bodi ya Arsenal imetoa kiasi cha pauni milioni 48 kwa ajili ya usajili wa kipindi hiki cha majira ya joto, kiasi ambacho kinaonekana kuwa hakitoshi.

Miamba hao wa Ligi Kuu ya England hadi sasa wamefanikiwa kuipata sahihi ya kinda wa Brazil, Gabriel Martinelli mwenye umri wa miaka 18 kwa pauni milioni sita.

Kinda huyo hivi karibuni aliitwa katika kikosi cha Taifa cha Brazil ambacho kinashiriki michuano ya mataifa ya America Kusini, Copa America.





# BAYERN YAKAMILISHA USAJILI KINDA WA CHELSEA

**MUNICH,** Ujerumani

BAYERN Munich wamekamilisha mchakato wa kumsainisha mkataba kinda wa Chelsea, Jamal Musiala.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 16, ambaye anacheza nafasi ya ushambuliaji tayari ameripotiwa kufikia makubaliano ya maslahi binafsi na mabingwa hao wa Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga.

Musiala kwa sasa ana uraia pacha wa England na Ujerumani ameshazichezea timu za taifa za nchi zote mbili za chini ya umri wa miaka 16.

Kinda huyo aliyezaliwa Fulda nchini Ujerumani, alisajiliwa na Chelsea mwaka 2011 akitokea TSV Lehnerz.

Musiala ameichezea mara tatu timu ya vijana ya Chelsea chini ya umri wa miaka 18 tangu alipojiunga na timu hiyo Septemba mwaka 2018.

# *Martinez atakiwa kuinoa Newcastle*

**NEWCASTLE,** England

KLABU ya Newcastle inapanga kumchukua kocha wa timu ya Taifa ya Ubelgiji, Roberto Martinez kama kocha wao mpya baada ya kuondoka kwa Rafa Benitez.

Kwa mujibu wa Gazeti la The Sun, mmiliki wa Klabu hiyo, Mike Ashley anataka kumchukua kocha mwenye uzoefu wa Ligi Kuu ya England na Martinez ndio anayeonekana kufiti katika nafasi hiyo.

Shirikisho la Soka la Ubelgiji limeripotiwa kwamba linatarajia kupokea ofa kutoka kwa Ashley ndani ya siku chache zijazo ili kumuachia kocha huyo.

Hiyo imekuja baada ya siku chake kuondoka kwa Benitez ambaye ameteuliwa kuwa kocha wa klabu moja nchini China.

Benitez aliamua kuachana na timu hiyo baada ya kushindwa kufikia makubaliano ya kutia saini mkataba mpya hapo kwenye dimba la St James' Park.

Martinez ambaye alikuwa kocha wa Swansea kabla ya kuhamia Wigan ambako alishinda Kombe la FA mwaka 2013, anaonekana kuwa ana uzoefu wa kutosha na Ligi Kuu ya England.

Kocha huyo mwenye umri wa miaka 45, pia aliifundisha Everton na kuiwezesha kumaliza nafasi ya tano kwenye msimamo kabla ya kuteuliwa kuwa kocha wa Ubelgiji mwaka 2016.

Ashley pia anatajwa kuwa anawawania Steven Gerrard, Patrick Vieira, Mikel Arteta na Eddie Howe kuchukua mikobba hiyo ya Benitez.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# MESSI SASA AWEKA WAZI HATIMA YAKE ARGENTINA

## ●●● Ni baada ya Jesus, Firmino kuiongoza Brazil kuwachapa nusu fainali Copa Amerika, asema...

**BELO HORIZONTE,** Brazil

LIONEL Messi amewatoa mashabiki hofu kuhusu uwezekano kwamba anaweza kutundika daluga kimataifa kwa mara ya pili baada ya Argentina kutolewa kwenye michuano ya Copa America.

Argentina ilichapwa mabao 2-0 na Brazil kwenye mechi ya nusu fainali iliyopigwa Belo Horizonte usiku wa kuamkia jana, na kutolewa huko kunaendeleza rekodi mbaya kwa mshindi huyo mara tano wa tuzo ya Mchezaji Bora wa Dunia ['Ballon d'Or'] ya kutoshinda taji lolote kubwa akiwa na timu yake ya taifa.

Ni mwezi uliopita tu Messi alitoa mashaka kuhusu nafasi yake ya kucheza fainali za Kombe la Dunia za Qatar mwaka 2022 - wakati atakapokuwa na umri wa miaka 34- lakini baada ya kukatishwa tamaa katika michuano ya kimataifa, mshambuliaji huyo wa Barcelona agalau amethibitisha majukumu yake wakati huo huo.

**“Kitu fulani kipya kipo katika upeo wa macho,” aliwaambia wanahabari, akiongeza kuwa anatumai mashabiki nyumbani watatambua juhudi za kikosi hicho wakati wa michuano hiyo.**

“Ninatumai tunaheshimika na si kukosolewa. Wanapaswa kuiacha timu kuwa na kuendelea kukua.

“Ukweli ni kwamba nimekuwa vizuri na kundi hili la wachezaji na ikiwa ni napaswa kuisaidia kwa namna fulani nitapenda. Hili ni kundi kubwa ambalo linakua na kama ninaweza kujiunga nalo nitafanya.”

Messi hivi karibuni alistaafu mechi za kimataifa mwaka 2016, baada ya kukosa penalti wakati wa hatua ya matuta kwenye mechi ya fainali ya Copa America dhidi ya Chile.

Na baadaye alirudi kundini kwa wakati na kuisaidia timu yake kufuzu fainali za Kombe la Dunia 2018, lakini mara kadhaa tangu wakati huo amekuwa akisema wakati wake wa kuiwakilisha nchi yake unaelekea ukingoni.

Messi ndiye kinara wa ufungaji wa wakati wote Argentina, akiwa na mabao 68 katika wasifu wake kisoka kimataifa.

Katika mechi hiyo ya nusu fainali usiku wa kuamkia jana, Brazil iliizamisha Argentina na kutinga fainali yake ya kwanza ya Copa America tangu mwaka 2007, mabao yakifungwa na Gabriel Jesus dakika ya 19 na Roberto Firmino (71).

## ZISIKUPITE

### BALE CHAMBO YA POBGA REAL

REAL Madrid inakaribia kumjumuisha mshambuliaji wa Wales, Gareth Bale, 29, katika dili la kuinasa saini ya kiungo wa Manchester United na Ufaransa, Paul Pogba, 26. ***(Mail)***

### KUMRITHI GRIEZMANN

ATLETICO Madrid inavutiwa kuipata saini ya mshambuliaji wa Arsenal na Ufaransa, Alexandre Lacazette, 28, ili kuziba pengo la raia mwenzake anayewindwa na Barcelona, Antoine Griezmann, 28. ***(Mirror)***

### UMTITI AMPELEKWA SOKONI

BARCELONA ipo tayari kusikiliza ofa ya beki wao wa kati, Mfaransa Samuel Umtiti, 25, ambaye anawindwa na Manchester United. ***(Sport, via Mirror)***

### MAGUIRE KUVUNJIWA BENKI

MANCHESTER United itapaswa kuilipa Leicester City zaidi ya pauni milioni 90 ili kuipata huduma ya Harry Maguire - hivyo kumfanya mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 26, kuwa beki ghali zaidi wa wakati wote- kama inataka kuipata saini ya Muingereza huyo majira haya ya joto. ***(Telegraph)***

### COCU KUMRITHI LAMPARD DERBY

DERBY County itaziba nafasi ya kocha Frank Lampard, 41, anayejiunga na Chelsea kwa kumpa mkataba kiraka wa zamani wa Barcelona na Uholanzi, Phillip Cocu, 48, ambaye yupo huru baada ya kuondoka Fenerbahce mwaka jana. ***(Guardian)***

### UNITED YAMFUATA OLMO

MANCHESTER United imetoa ofa kwa kiungo wa Dinamo Zagreb na Hispania U-21, Dani Olmo. ***(Mail)***

### PALACE KUIKOMOA ARSENAL

CRYSTAL Palace haitaki kumuuza winga wa kimataifa wa Ivory Coast, Wilfried Zaha, 26, kwa Arsenal kwa hasira kwa sababu wanaamini 'Gunners' wameandaa kwa makusudi kumnasa mchezaji huyo anayetaka kuondoka. ***(Mirror)***

### AKE ANUKIA MANCHESTER CITY

BEKI wa Bournemouth, Mholanzi Nathan Ake, 24, kuna uwezekano akatia saini majira haya ya joto kuitumikia Manchester City. ***(L'Equipe, via Manchester Evening News)***

### TREZEGUET LULU ASTON VILLA

ASTON Villa inamtaka kiungo wa Kasimpasa na Misri, Mahmoud Trezeguet, 24. ***(Sun)***

### AZIKATAA LIVER, BAYERN

WINGA wa Barcelona na Ufaransa, Ousmane Dembele, 22, anataka kuendelea kubaki Nou Camp licha ya kuivutia Liverpool na Bayern Munich. ***(L'Equipe)***

### ARSENAL YAWEKEWA KIGINGI

CELTIC inajaribu kuizuia Arsenal kumnasa beki wa pembeni Mscotland Kieran Tierney, 22, kwa kuongeza dau hadi pauni mioni 25. ***(Star)***

### CHEEK, CHELSEA WAKUBALIANA

CHELSEA imekubaliana mkataba wa muda mrefu na kiungo Muingereza Ruben Loftus-Cheek, 23. ***(Telegraph)***

HABARI MICHEZO

## KMC na matumaini Kombe la Kagame

**Na Shufaa Lyimo**

TIMU ya KMC FC, leo alfajiri imesafiri kuelekea nchini Kigali Rwanda kwa ajili ya kwenda kushiriki mashindano ya Kombe la Kagame yaliyoandaliwa na Baraza Vyama vya Soka la nchi za Afrika Mashariki na Kati (Cecafa) yanayotarajiwa kuanza Juai 6-21, mwaka huu.

Katika mashindano hayo, KMC imepangwa Kundi A na timu za Rayon Sports (Rwanda), TP Mazembe (DRC) pamoja na Atlabara ya Sudan Kusini na itaanza kurusha karata yake ya kwanza dhidi ya Wasudan hao Julai 7, mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, asubuhi mara baada ya kumaliza mazoezi kocha mkuu wa kikosi hicho, Jackson Mayanja aliahidi kurudi na matokeo mazuri kutokana na namna alivyowaandaa wachezaji wake tangu alipokabidhiwa timu hiyo.

Hata hivyo, Mayanja alisema wachezaji wake wote wanaendelea vizuri kila mmoja akiwa na morali ya juu kuhakikisha anarudi na matokeo mazuri nyumbani na kudai hana mchezaji yeyote majeruhi ambaye atashindwa kusafiri na timu.

Licha ya kundi lao kudaiwa kuwa la 'kifo' kutoka kujumuisha timu zenye viwango vya juu, Mayanja amesema hana hofu katika hilo kwa kuwa wachezaji wake amewapa mbinu ambazo zitawasaidia pindi watakapokutana na mpinzani yeyote dimbani.

Kwa upande wake msemaji wa timu hiyo, Anuari Binde alisema jana msafara wa wachezaji 20 pamoja na viongozi watano ndio waliotarajiwa kuondoka leo alfajiri kuelekea Rwanda.

## JWTZ kushiriki michezo ya majeshi Dunia

**Na Faustine Feliciane**

JESHI la Wananchi la Tanzania (JWTZ), litatuma wanamichezo kushiriki michezo mitatu tofauti katika michuano ya Dunia ya Majeshi itakayofanyika nchini China kuanzia Oktoba 18 hadi 27, mwaka huu.

Katika michezo hiyo itakayoshirikisha wanamichezo 10,000 kutoka nchi wanachama wa Baraza la Dunia la Michezo ya Majeshi (CISM), Tanzania itashiriki michezo ya riadha, ngumi na mieleka.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Mwakilishi wa Tanzania CISM lililo na makao makuu nchini Ubelgiji, Kanali Joseph Bakari, alisema Baraza hilo litasaidia baadhi ya gharama ya timu hiyo ya JWTZ.

Alisema kwa upande wa baraza hilo, kwa sasa wapo kwenye kipindi cha maandalizi mpaka mwishoni kwa mwezi huu.

"Kwa kuwa mimi ni mwakilishi wa nchi yetu kwenye baraza hili na kitengo changu kinahusika na michezo hii, nafahamu Tanzania itashiriki kwenye michezo hiyo mitatu," alisema Kanali Bakari.

# AZAM WAAHIDI KURUDI NCHINI NA KAGAME LAO

**Na Shufaa Lyimo**

MABINGWA watetezi Klabu Bingwa Afrika Mashariki na Kati maarufu Kombe la Kagame, Azam FC, wameondoka usiku wa kuamkia leo kuelekea Kigali, Rwanda kwenye michuano hiyo huku wakieleza wamekwenda kurudi na taji lao.

Azam ambao wameondoka saa tisa usiku kwa Shirika la Ndege la Rwanda Airways, kwenye Kundi lao la B linalojumuisha timu ya Bandari FC ya Kenya, KCCA (Uganda) na wenyeji Mukura Victory, ambao wataanza nao Julai 7, mwaka huu kwenye Uwanja Huye.

Akizungumza na Nipashe jana, Afisa Habari wa timu hiyo, Jafari Idd alisema kocha wa kikosi hicho, Etienne Ndayiragije amechukua baadhi ya wachezaji kutoka kikosi chao cha vijana na kuwaingiza kuwanoa vema kwa ajili ya michuano hiyo.

**Aidha, alisema kocha amependekeza kutumia yosso hao kutokana na baadhi ya nyota wake kuwa katika majukumu na timu zao za taifa kwenye fainali za Mataifa ya Afrika (Afcon) 2019 zinazoendelea nchini Misri.**

Alisema kwa mujibu wa mapendekezo ya kocha, nyota hao wakiwamo waliokuwa na kikosi cha Taifa Stars ambao wanatarajiwa kurejea leo wakitokea Misri baada ya kuaga michuano hiyo, wamepewa mapumziko na kwamba watawasubiri wenzao mpaka watakaporudi ndipo waungane nao tayari kwa maandalizi ya msimu ujao wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michuano ya kimataifa.

"Kwa wale wachezaji wetu ambao wapo kwenye kikosi cha timu ya Taifa tutawapa mapumziko tutaungana nao tutakaporudi kwa ajili ya kujiandaa na mashindano yajayo ya Ligi Kuu na Kombe la Shirikisho Afrika," alisema Jafari.

Aliongeza kuwa kikosi kilichoondoka mbali na yosso hao wa Timu B, pia kinajumuisha nyota wapya waliosajiliwa msimu huu, hivyo wanauhakika wataweza kurejea na kombe lao.




Mtendaji Mkuu wa Simba, Crescentius Magori, akimtambulisha aliyekuwa nahodha wa Yanga, Ibrahimu Ajibu (kulia) aliyerejea Simba akitokea Yanga baada ya jana kutia saini mkataba wa miaka miwili wa kuitumikia klabu hiyo. **PICHA: SIMBA**

# *Yanga rasmi mawindoni msimu mpya*

**Na Shufaa Lyimo**

JESHI kamili la kikosi cha Yanga linatarajiwa kuanza kuripoti kambini leo kujiwinda na msimu mpya wa Ligi Kuu Tanzania Bara pamoja na michuano ya Ligi ya Mabingwa Afrika


Akizungumza na Nipashe jana, Kaimu Katibu Mkuu wa klabu huyo, Dismas Ten, alithibitisha wachezaji kuarifiwa kuanza kuripoti kambini leo huku akieleza kuwa mazoezi rasmi yataanza Jumapili wiki hii.

"Kesho (leo) wachezaji wetu wataanza kuripoti kambini huku tukiendelea na zoezi la usajili na moja kwa moja Jumapili wiki hii wataanza mazoezi kwa ajili ya kujiandaa na msimu ujao wa Ligi kuu Tanzania Bara pamoja michuano ya Ligi ya Mabingwa,"alisema Dismas.

Alisema kikosi chao kitaendelea na mazoezi Jijini Dar es Salaam mpaka hapo uongozi wa juu utakapoamua kuhamisha kambi ili kuwaweka fiti wachezaji wao wote waliosajiliwa na wale ambao wataendelea kuwasaini kuitumikia klabu hiyo.

"Kuhusu suala la kuweka kambi nje ya Mkoa wa Dar es Salaam hilo bado sijalifahamu na siwezi kulizungumzia kwa sababu kuna watu ambao wanahusika na masuala hayo ila naamini mtapata taarifa kuelezwa kile kinachoendelea pindi kambi itakapokuwa imeanza," alisema.

Michezo
Alhamisi Julai 4, 2019
Nipashe



## Messi aweka wazi hatima yake Argentina

UKURASA 30



Kiungo mkabaji wa Brazil, Carlos Henrique Casimiro, akihaha kumzuia mshambuliaji wa Argentina, Lionel Messi wakati wa mechi ya nusu fainali ya Copa America iliyopigwa Belo Horizonte usiku wa kuamkia jana na Brazil kushinda 2-0. **HABARI UK. 30**

## Guardiola apanga kurudi Barcelona

**MANCHESTER,** England

KOCHA wa Manchester City, Pep Guardiola amesema kuwa bado ana mpango wa kurudi Barcelona siku moja.

Kocha huyo mwenye miaka 48, ambaye aliiongoza Man City kupata mataji matatu msimu uliopita, ameku-wa pale Etihad kwa miaka mitatu sasa.



HABARI UK 28

# AJIBU TAYARI SIMBA SC, SAA 7 YA GADIEL YAJA

## Aidindia Yanga, Msimbazi yachungulia dili, Nipashe yanasa mchongo mzima baada ya...

**Na Mwandishi Wetu**

HATIMAYE mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Bara, Simba wamefanikiwa kumrejesha nyumbani kiungo mshambuliaji wao na aliyekuwa nahodha wa Yanga, Ibrahim Ajibu kufuatia jana kumtangaza akisaini mkataba wa miaka miwili na klabu hiyo ya mtaa wa Msimbazi jijini Dar es Salaam.

**Hata hivyo, kutua kwa Ajibu kunaelezwa kuwa kutafuatiwa na beki kisiki wa kushoto, Gadiel Michael ambaye naye anatarajiwa kutangazwa hivi karibuni baada ya kushindwana na waliokuwa waajiri wake, Yanga.**

Simba ambayo imekuwa na utaratibu wake wa kutangaza wachezaji wapya na waliongeza mkataba kila ifikapo saa saba mchana, jana katika ukurasa wake wa Instagram ilimtangaza Ajibu akiwa na Mtendaji Mkuu wa klabu hiyo, Crescentius Magori baada ya kusaini mkataba wa kuitumikia.

"Safari ya mtoto kuishi mbali na nyumbani imefikia ukingoni. Ibrahim Ajibu ameamua kufanya maamuzi sahihi ya kurudi nyumbani Msimbazi, ndio amerudi na amesaini mkataba wa miaka miwili kucheza na kuwapa furaha Wanasimba. Karibu nyumbani Ajibu #Amerudi #Ajibu #Nguvu Moja," ilisomeka taarifa hiyo ya Simba.



Ajibu ambaye msimu uliomalizika akiwa Yanga ameongoza kwa kutoa pasi za mwisho nyingi (18) Ligi Kuu Bara huku akifunga mabao sita, anakuwa mchezaji mpya wa nane kusajiliwa Simba na wa tatu mzawa baada ya kipa Beno Kakolanya kutoka Yanga pia na beki Kennedy Juma kutoka Singida United.

Wachezaji wengine watano ni wa kigeni, ambao ni mabeki Wabrazil Gerson Fraga Vieira kutoka ATK ya Ligi Kuu ya India na Tairone Santos da Silva kutoka Klabu ya Atletico Cearense FC, mshambuliaji Wilker Henrique da Silva kutoka Bragantino, zote za Daraja la Nne nchini Brazil na viungo Msudan Sharaf Eldin Shiboub Ali Abdalrahman aliyetokea Al Hilal ya Sudan na winga Deo Kanda kutoka TP Mazembe ya kwao, DR Congo.

Kuhusu Gadiel, taarifa zilizolifikia Nipashe jana zimeeleza kuwa saa saba zilizosalia kabla ya dirisha la usajili kufungwa Julai 31, mwaka huu hazitamwacha salama kabla ya kutangazwa kumalizana na Simba.

"Ni muda tu unasubiriwa kabla ya Gadiel kutangazwa Simba kwani anatarajiwa kuja kuchukua nafasi ya Mghana Asante Kwasi ambaye alikuwa anasaidiana na Tshabalala (Mohamed Husseni)," kilieleza chanzo chetu jana.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka ndani ya uongozi wa Klabu ya Yanga, Gadiel alipewa saa 24 kuanzia jana kusaini mkataba mpya na kama hakusaini basi klabu hiyo ilikuwa tayari kumsainisha mchezaji mwingine katika nafasi hiyo.

"Gadiel anataka zaidi Sh. milioni 50 ili kusaini mkataba wa miaka miwili, jambo ambalo klabu haiafiki, hivyo alipewa saa 24 kusaini vinginevyo asajiliwe mchezaji mwingine," kilieleza chanzo chetu.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042
9 770856 541002